

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kumi - Tarehe 24 Juni, 2003

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 90

Utaratibu wa Kujaza Fomu za Mali

MHE. LEKULE M. LAIZER aliuliza:-

Kwa kuwa kuna utaratibu wa kujaza fomu za mali kwa Kamishna wa Maadili, lakini baadhi ya watumishi wa Halmashauri hawajazi fomu za mali zao, wakati wanafanya kazi kwenye nafasi zenye fedha au mali za Halmashauri:-

Je, kuna tofauti gani kati ya watumishi wengine ambao wako pamoja kwenye Ofisi hizo na wanajaza fomu na wale ambao hawajazi fomu na kwamba watajulikana vipi endapo mali zao zitaongezeka?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kujaza fomu za Tamko la Mali kwa Viongozi na watumishi wa Serikali za Mitaa umeainishwa kwenye Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Namba 13 ya mwaka 1995. Watumishi walijotajwa kwenye Sheria hii ni Wakurugenzi wa Halmashauri zote. Hawa ni Watendaji Wakuu wa Halmashauri na kwamba wanayo madaraka makubwa ambayo ni muhimu kuyawekea utaratibu wa kuyadhibiti ili wasiweze kuyatumia vibaya kama vile kujilimbikizia mali isivyo halali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ukimwondoa Mkurugenzi Mtendaji, watumishi wa Halmashauri waliobaki hawajazi fomu za tamko ya mali zao, ingawa wanafanya kazi kwenye nafasi zenyenye fedha au mali za Halmashauri. Hii ni kwa sababu hawakuainishwa kwenye Sheria ya Maadili ya Viongozi. Hata hivyo, haina maana kwamba wanaweza kujilimbikizia mali na kuachwa bila kudhibitiwa, viro vyombo vinavyosimamia utendaji wao wa kazi wa siku hadi siku. Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Kamati za kudumu za Halmashauri na Baraza la Madiwani ndio wenye jukumu la kwanza la kusimamia utendaji kazi na uadilifu wa Watendaji wote wa Halmashauri.

Chombo kingine ni Taasisi ya Kuzuia Rushwa ambayo hivi sasa imefungua Ofisi katika Mikoa 20 na Wilaya na Ofisi 46. Moja ya sababu ya kufungua Ofisi hizo ni kusimamia maadili ya Watanzania kwa ujumla wakiwemo watumishi wa Halmashauri zetu.

Aidha, chini ya Kifungu cha ya 27 cha Kanuni ya Serikali za Mitaa Maadili ya watumishi za mwaka 2000 mtumishi ye yeyote atakayejiingiza kwenye shughuli yenyenye mgongano wa Halmashauri hana budi kujaza fomu ya Tamko la Mali zake. Utaratibu huu upo kwa lengo la kusimamia maadili katika utendaji kazi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho Mdhibiti Mkuu wa Maadili ya mtumishi ye yeyote wa umma ni mwananchi ambaye anahudumiwa na watumishi wa Halmashauri. Ningependa kutumia nafasi hii kuwashukuru sana wananchi ambao wamesaidia sana nchi yetu kutoa taarifa mbalimbali juu ya utendaji kazi wa watumishi katika Halmashauri zetu. Hivyo naendelea kutoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa hizi kwenye vyombo husika ili tuweze kuimarisha utendaji katika Halmashauri zetu.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika kila Halmashauri kuna Mweka Hazina na baadhi yao wanajenga katika maeneo wanakoarifiwa, kila wanapoarifiwa wanajenga na sehemu nyingine wanajenga, je, mtu kama huyu si mngekuwa na namna ya kumbana?

Swali la pili, kwa kuwa Madiwani hawana fedha, wanakusanya ni watu wanaokuja tu kwenye vikao. Je, hawa wanaowawekea utaratibu wa kujaza fomu na kuwaacha Waweka Hazina, hamwoni kwamba ni suala potofu kabisa kumdhiliti mtu ambaye hana fedha?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, inawezekana wako baadhi ya Watendaji wachache ambao hapa na pale wanaweza kuwa wanaonyesha dalili ambazo Mheshimiwa Mbunge analieleza. Lakini kama nilivyosema kazi kwa kweli imekuwa ya kuwaumbua watu wa aina hiyo ni yetu sisi sote pamoja na Mheshimiwa Mbunge. Kama anazo taarifa nzuri kama hizo basi mimi namshauri tu kama azilete kwetu kwa sababu wapo ambao wameshaleta na tutachukua hatua. Tuletee au peleka katika vyombo vingine

vinavyohusika. Lakini kuhusiana na mtu kama huyu kutowekwa katika orodha ya watu ambao wanapashwa kujaza fomu, narudia kusema tu kwamba wakati inatungwa Sheria hii hapa Bungeni wakati huo hamkuona umuhimu wa kuwaweka watu hawa katika orodha.

Lakini inawezekana vile vile ilitokana na ukweli kwamba chombo hiki ni kidogo na hakina uwezo wa kuweza kuzitawanya nguvu zake kwa nchi nzima. Nadhani ndiyo maana mkaona kwamba hawa watu wabaki na wahudumiwe kwa utaratibu ambao nimeueleza.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya swali la msingi lililoulizwa. Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali lifuatalo.

Kama alivyokiri ni kwamba njia mojawapo ni ya kupata msaada kwa vyombo vya Serikali iweze kuchunguza maadili ya watumishi ni wananchi wenyewe. Sasa ningeomba kuuliza kwamba Serikali ina mpango gani katika kuweka wazi suala hili na kurekebisha Sheria ili mali za watumishi na viongozi ambao wanatajwa katika fomu husika ziwe zinawekwa wazi katika Gazeti la Serikali na vyombo mbalimbali vya habari ili wananchi wenyewe waweze kufuatilia kina nani wanajaza fomu za uongo na ni nani wanajaza fomu za ukweli?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, mimi nina hakika Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba umuhimu wa utunzaji wa baadhi ya maeneo yanahusiana na usiri wa mambo ya mtu binafsi ni jambo ambalo wote tunapashwa kulienzi.

Kwa utaratibu tulionao sasa sheria mliyoitunga hapa kwamba Kamati ya Maadili ndiyo inayohusika na kuchukua fomu hizi na kuzifanyia kazi kwa lengo la kuweza kuchukua hatua ambazo zinastahili. Sasa kana tutafikia hatua kwamba tuyatangaze majina hayo kwenye magazeti, nina hakika kabisa huenda pengine tukaanza tena kugongana na Katiba yetu.

Na. 91

Matatizo ya Barabara ya Mbalizi-Namkukwe

MHE. PAUL E. NTWINA aliuliza:-

Kwa kuwa kuna tatizo la kutotengenezwa kwa barabara ya Mbalizi-Galula-Magamba-Namkukwe na kwa kuwa barabara hiyo imekuwa kero kubwa kwa wananchi wa Kata za Galula; Totowe na Namkukwe na kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa ahadi za kuitengeneza barabara hiyo kidogo kidogo hasa kwa barabara ya Galula-Namkukwe, lakini haijatekeleza ahadi hiyo:-

Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuitengeneza barabara hiyo na ni lini itapewa kipaumbele cha matengenezo kama barabara nyine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI
ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba kwa taarifa tulizonazo barabara anazozitaja Mheshimiwa Mbunge ni barabara mbili tofauti. Barabara hizo ni Mbalizi-Galula-Mkwajuni hadi Makongolosi yenye urefu wa kilomita 117.8 na barabara ya Galula-Magamba-Namkukwe, yenye urefu wa kilomita 57. Barabara zote zinahudumiwa na Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Mbeya (*TANROADS*).

Mheshimiwa Spika, kwa sasa barabara ya Mbalizi-Galula-Mkwajuni ni barabara nzuri na mwaka huu wa 2002/2003 barabara hiyo ilitengewa kiasi cha shilingi milioni 245,259 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida (70 kilomita), matengenezo ya sehemu korofi (kilomita 10) na ukarabati (kilomita 15). Barabara ya Galula-Magamba-Namkukwe ndiyo yenye matatizo. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali inaona umuhimu wa barabara hiyo na ndio maana mwezi Machi, 1999 Mhandisi wa Mkoa wakati huo aliwasilisha Wizarani makisio ya kujenga barabara hiyo, ikiwa ni pamoja na makalvati yanayotakiwa kwa kiwango cha changarawe. Mapendekezo hayo yalikuwa ni ya kubadilisha mpitio wa barabara (*Road Alignment*) na kupitia katika vijiji vya Ilembo, Magamba, Malangali, Muheza hadi Namkukwe badala ya ile ya zamani. Gharama halisi ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe zinakadirwa kufikia shilingi 16 bilioni.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2001 Serikali kuptitia kwa Wakala wa Barabara *TANROADS* Mkoa wa Mbeya iliitisha zabuni kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwa barabara zenye matatizo na hii ikiwemo. Gharama za upembuzi yakinifu zilifikia shilingi milioni 21.2 lakini fedha zilizokuwepo ziliikuwa ni shilingi milioni 7.5 tu. Kwa hiyo, upembuzi yakinifu haukuweza kufanyika.

Serikali bado inaendelea kufanya juhudhi za kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwa maeneo hayo yote. Hata hivyo, pamoja na kwamba Serikali inaendelea na juhudhi za kutafuta fedha ili barabara hiyo ya Galula-Namkukwe iweze kufanyiwa upembuzi yakinifu na hatimaye kutengenezwa. Serikali kama ilivyokuwa imetoa ahadi yake ya kutoa fedha kidogo kidogo imekuwa ikitekeleza ahadi hiyo. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2002/2003 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 16.3 kwa ajili ya barabara hiyo.

MHE. PAUL E. NTWINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa barabara hii ni muhimu na matarajio ya wananchi hata kwa kipindi chote ambacho niko Bungeni wamekuwa wakinaka ijengwe. Je, Waziri atakubaliana nami kuwa hili suala la kutengeneza kidogo kidogo lingeweza kusaidia kwa sababu ya uhaba wa pesa? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa shukrani ambazo ningependa ziifiki Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kutekeleza Ilani yake hasa kwa upande wa Jimbo la Songwe. Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, haoni umuhimu kuwa hii barabara kama itajengwa itaunganisha Jimbo la Songwe na Wilaya ya Mbozi? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kuongeza majibu mazuri ya Naibu Waziri wa TAMISEMI.

Kwanza nitoe taarifa kwamba barabara hii tulirithi baada ya wananchi kuwaomba sana *NORAD* waitengeneze barabara hii ambayo walikuwa na mradi huko. Wao walibuni na sisi tukairithi kwa sababu wao walishindwa kuitengeneza kwa upungufu wa fedha.

Kwa hiyo, ndiyo maana tuliahidi kwamba tutatengeneza kidogo kidogo na kweli ni barabara muhimu kwa kuunganisha majimbo mengine lakini ili tuweze kufanya hivyo inabidi lazima tukamilishe barabara hii ambayo inataka fedha kiasi cha shilingi bilioni 12.

Kwa hiyo, ningewomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Songwe watuvumilie tutengeneze barabara hii pole pole ili ikamilike na hivyo tutawenza kuunganisha. Kwa sasa hivi tingoje labda Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi itasema vipi.

Na. 92

Price Stabilization Fund na STABEX

MHE. STANLEY H. KOLIMBA aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya mikakati ya kupambana na umaskini ni pamoja na hatua za kuwashimiza wakulima wadogo wadogo kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wakulima katika kuanzisha mfuko maalum (*Price Stabilization Fund*) kwa ajili ya kutoa fidia kwa wakulima pale ambapo bei za mazao yao zinapoporomoka hadi kufikia kiwango cha mkulima kushindwa kufikia gharama za uzalishaji?

(b) Kwa kuwa kwa utaratibu wa sasa, matumizi ya fedha za *STABEX* yanalenga kuendeleza huduma kwa wakulima katika kuboresha miundombinu, viwanda vya kukoboa na kusindika kwenye maeneo yao; je, ni lini fedha hizo zitatolewa kwa

wakulima wa kahawa wa Wilaya ya Ludewa ili waweze kukamilisha ujenzi wa vinu vya kukobolea kahawa *Pulpary Mini-Coffee Machines* ambavyo vilitelekezwa na kushindikana kukamilishwa baada ya mradi wa uboreshaji wa kahawa kusimamishwa mwaka 2001 katika vijiji vya Madunda, Kiwe, Lupande Mawenzi, Kimata na Kitewe?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa mifuko ya kuwafidia wakulima kunapotokea tatizo la bei ya mazao kushuka sana (*Price Stabilization Funds*). Mifuko ya aina hiyo ni rahisi zaidi kuanzishwa kwa mazao ya biashara yenye mikondo maalum ya kuyauza, kuliko ilivyo kwa mazao ya chakula.

Kwa wakati huu, hatuna utaratibu wa kufidia bei kwa zao lolote na kuna ugumu wa kuweka utaratibu kama huo kwa kuwa bei za mazao karibu yote ziko chini sana, kiasi kwamba wakulima hawataweza kuchangia kuanzishwa kwa mifuko hiyo. Mazingira yaliyopo sasa yatakapobadilika, Serikali itaangalia uwezekano wa kuanzisha *Price Stabilization Funds* kwa mazao yenye uwezekano wa kuwa na utaratibu huo.

(b) Ni kweli kwamba fedha za *STABEX* zitatumika kuendeleza huduma kwa wakulima katika kuboresha miundombinu. Fedha hizo zimegawanywa katika maeneo makuu matatu; *Euro* milioni 9 zitatumika kwenye utafiti wa kahawa kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania, iliyoko Lyamungo, *Euro* milioni 10 zitatumika kwa matengenezo ya barabara kupitia *TANROADS* na *Euro* milioni 18 zitatumika kugharamia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Aidha, *Euro* milioni 1.44 zitatumika kwa maandalizi, usimamizi na ufuataliji wa utekelezaji. Fedha hizi zitatumika katika muda wa miaka mitatu, kuanzia mwaka wa 2003/2004. Fedha za *STABEX* zitatolewa baada ya mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwenye Wilaya kupokelewa, kuchambuliwa na kukubaliwa. Kwa upande wa Wilaya ya Ludewa, nawashauri muweke ujenzi wa *central pulperies* kwenye mipango yenu.

MHE. STANLEY H. KOLIMBA: Mheshimiwa Spika, naomba niulize swal moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inafahamu wazi kwamba zao la kahawa miaka ya nyuma kutokana na *Lome Agreement* walikuwa wakulima wanapewa mbolea na zana nyingine za madawa kwa ajili ya wakulima wa kahawa. Je, sasa hivi haoni kwamba itafika mahali mkulima atang'oa kahawa? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kama tutafuata huu utaratibu wa kutengeneza *hand pulpery* na ukikamilika kama tunavyoshauri, ubora wa kahawa utakuwa umeongezeka na kwa hiyo, watapata bei nzuri. Hivyo nashauri wasing'oe mikahawa.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa hizi fedha za *STABEX* zilitolewa pamoja na mambo mengine kwamba bei ya wakulima imeteremka kwa hiyo wafidiwe. Kwa hiyo, ilikuwa ni sawa sawa na fedha za rambirambi. Sasa Serikali kwa kutokuleta angalau kidogo ikawagawia wakulima wale mmoja mmoja ni sawasawa na mtu aliyetoa rambirambi mtu akaitafuna?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninavyoolewa mimi fedha hizi hazikutolewa sawasawa na rambirambi au shughuli nyingine. Zimetolewa maalum kwa ajili ya kuboresha kilimo cha kahawa kusudi wawze kupata bei nzuri. Bado nasisitiza kuwa Wizara inapendekeza, tutekeleze haya yaliyomo, ndio yajibu kwenye swalii. Bei ikiongezeka na watapata bei nzuri na hakuna haja ya kulipia mmoja mmoja kwanza hazitatosha kwa shughuli hiyo kama anavyofikiri.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa fedha hizi zimetolewa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa kahawa na kwa kuwa bei ya pembejeo na kahawa ni kubwa sana. Je, Serikali isingefikiria kutumia sehemu ya fedha hizi kwa ajili ya ku-subsidize bei ya pembejeo? (*Makofii*)

WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hizi ni fedha zinazotolewa na Jumuiya ya Ulaya na mwanzoni fedha hizi zilikuwa zinatumika kuwafidia wakulima kutokana na bei ndogo ya kahawa. Lakini kutokana na soko huria kubadilika utaratibu wakaamua kwamba fedha hizi sasa zitumike kujenga huduma katika Sekta ya Kilimo ikiwa ni pamoja na utafiti, barabara na kuihudumia Sekta ya Kilimo.

Kwa hiyo, Serikali kwa kweli haina uamuzi katika fedha hizi isipokuwa kutekeleza makubaliano hayo tuliyofikia. Kwa hiyo, naomba wakulima waelewe hivyo na Waheshimiwa Wabunge waelewe hivyo. Ahsante sana. (*Makofii*)

Na. 93

Hadhi ya Idara ya Kilimo Ngazi ya Wilaya

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH (k.n.y. MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA) aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipa Idara ya Kilimo katika ngazi ya Wilaya hadhi kama ile inayotolewa kwa Idara ya Ujenzi, Maji, Elimu na Afya ambazo mishahara yao na fedha za matumizi mengineyo hutolewa na Serikali Kuu moja kwa moja kwa njia ya ruzuku?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Ismail Iwvatta kwamba katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya, Idara ya Kilimo ina hadhi sawa na Idara za Ujenzi, Maji, Elimu na Afya na kwamba fedha kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo hutolewa na Serikali Kuu kama ruzuku kwa utaratibu ule ule unaotumika kugharamia Idara nyingine alizozitaja.

MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo sana kwamba pamoja na kwamba fedha hizo zinatolewa sawasawa na watumishi wengine, Serikali haioni umuhimu kwamba hawa watumishi wa Kilimo kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania kuwapa motisha ili kuweza kuona kwamba wao wanafanyakazi hii ngumu kuliko wengine. Kwa hiyo, wao wataendelea zaidi katika suala hili? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, ni kweli watumishi wa Kilimo wanafanyakazi kubwa sana inahusiana na uti wa mgongo kwa uchumi wetu. Lakini huko vijijini wao si peke yao wanaoishi. Hiyo ni moja.

Pili, ni kwamba tukianza kubagua huyu anafanyakazi muhimu na hali ya uchumi ndiyo hii iliyopo. Bado tunasisitiza kwamba tuhudumie wananchi popote tulipo kwa uwezo wetu wote bila kutegemea kulipwa zaidi kuliko wengine.

Na. 94

Taasisi ya Waathirika wa Akili Mirembe

MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA aliuliza:-

Kwa kuwa Taasisi ya Mirembe iliyoko Mkoani Dodoma inafanya kazi nzuri ya kutibu na kurekebisha waathirika wa akili wakiwemo wale waliokuwa wanatumia madawa ya kulevyta na kwa kuwa Taasisi hiyo huchukua pia wafungwa waliofanya makosa yanayosababishwa na matatizo ya akili mfano mauaji, ubakaji na kadhalika:-

(a) Je, ni matatizo gani na mangapi ambayo Taasisi hiyo imeshayapata na ingali ikipata kwa kuchanganya waathirika hawa wa aina mbili tofauti, yaani wafungwa au wahalifu na waathirika wa madawa ya kulevyta?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kazi nzuri inayofanywa na Taasisi hiyo inaweza isiwe na matokeo mazuri ikiwa wagonjwa hao wa aina tofauti hawatatengwa?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha vituo au Taasisi kama hiyo kila Mkoa hasa ikizingatiwa kuwa hivi sasa miji yote nchini wapo vijana walioathirika na madawa ya kulevyta?

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Isanga haijapata matatizo yanayotokana na kuwachanganya waathirika wa dawa za kulevyta na wagonjwa wa akili wahalifu. Kuna uanganlizi wa kutosha unaohakikisha makundi tofauti ya wagonjwa yanapata uchunguzi wa tiba kwa kuzingatia aina ya matatizo yao. Wagonjwa wanaokuja kwa uchunguzi hukaa kwa wastani wa siku 42 na wale waathirika kwa dawa za kulevyta hutibiwa kwa wastani wa miezi 6. Sehemu kubwa ya tiba ni mbinu za kisaikolojia ikiwa ni pamoja na ushauri nasaha juu ya athari za dawa za kulevyta na njia za kuepukana nazo. Ikibidi waathirika hupewa dawa za kuwatuliza.

Wagonjwa waliofutiwa mashitaka kutokana na kuonekana walitenda makosa wakiwa na matatizo ya akili, hutibiwa kwa muda usiopungua miaka mitatu na muda mwangi hupewa tiba ya kazi za mikono kulingana na fani zao kwa mfano kilimo, ufugaji na uselemala.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya awali katika kipengele (a) hapo juu hakuna ulazima wa kuwatenganisha wagonjwa kwa sasa hasa tukizingatia uwezo mdogo wa Serikali wa kujenga vituo maalum kwa wagonjwa hawa.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuanzisha vituo maalum vya tiba ya waathirika wa dawa za kulevyta kwa kila mkoa kwa sababu gharama zake ni kubwa mno ukilinganisha na uwezo wa Taifa letu. Mikakati ya muda mfupi na mrefu inatekelezwa na Wizara yangu ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo na nyenzo za kuboresha stadi za kuwahudumia waathirika wa dawa za kulevyta katika ngazi mbalimbali za utoaji huduma za afya.

Wizara inatayarisha miongozo ambayo itawawezesha watendaji wa hospitali, vituo vya afya na zahanati kutoa huduma nzuri zaidi kwa waathirika wa dawa za kulevyta. Mafunzo ya mara kwa mara kazini (*In Service Training*) yanategemewa kuboresha uwezo wa wataalam wa Sekta ya Afya kuwahudumia waathirika wa dawa za kulevyta kwa ufanisi zaidi.

Pia ipo mikakati ya muda mrefu ya kusomesha wataalam zaidi wa huduma za afya ya akili, watakaoimarisha uwezo wa Sekta ya Afya kukabiliana na madhara ya dawa za kulevyta. Kulingana na uwezo wa Serikali kifedha na upatikanaji wa wataalam wa tiba za matatizo ya dawa za kulevyta, vituo maalum vitajengwa kwa hatua. Kwa mfano, katika jiji la Dar es Salaam inaonyesha kuwa kituo kama hicho kinahitajika haraka sana na juhudzi zinafanywa kwa kushirikiana na Tume ya Kuthibiti dawa za kulevyta nchini, ili kuwezesha utekelezaji wake.

MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa na nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza ningependa kufahamu kwa kipindi cha mwaka 2001 hadi sasa ni vijana wangapi walioathirika na madawa ya kulevyta waliopatiwa tiba na wamepona wamerudi makwao?

Swali la pili, ningependa pia kufahamu kwa kipindi hicho hicho 2001 hadi sasa, je, kuna wangapi vijana wetu ambao wamepokelewa katika Taasisi hiyo? Ahsante Mheshimiwa Spika. (*Makofsi*)

SPIKA: Sijui kama Mheshimiwa Waziri anazo takwimu hizo hapa? Lakini endelea kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ametaka kupata takwimu si rahisi kuwa nazo sasa hivi, lakini nataka nimhakikishie kwamba takwimu za maswali yote mawili nitampatia.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hospitali ya Mirembe, madaktari wanaohudumia vichaa katika hospitali ile sijui Serikali inawawekea kinga gani, maana yake kunakuja vichaa ambao wanawapiga mpaka madaktari? (*Kicheko/Makofsi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, mafunzo wanayopewa Waganga wanaohudumia wagonjwa wa akili ndiyo yanawafanya waweze kuepukana na matatizo yanayotokana na wagonjwa hao. Kwa maana hiyo, hakuna kinga maalum bali wamefundishwa jinsi gani ya kuwatibia wagonjwa hawa ili wasiweze kupata madhara haya.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, swali ambalo nilikuwa niulize ndiyo hilo limeulizwa. Kwa hiyo, naomba radhi.

SPIKA: Nashukuru!

Na. 95

Ugonjwa wa Ukimwi

MHE. JOHN L. MWAKIPESILE aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa Ukimwi hauna tiba wala kinga; na kwa kuwa dawa za kuongeza maisha ya watu walioathirika ni haba na ni za gharama sana:-

(a) Je, ni lishe ya aina gani inayohitajika kila siku ili mwathirika aweze kuishi kwa kipindi kirefu zaidi?

(b) Je, kuna ukweli gani kwamba wanawake waliokeketa hawaambukizwi ugonjwa wa Ukimwi kwa urahisi?

(c) Je, Serikali itaanza lini kusambaza dawa za kuongeza uhai kwa waathirika kwenye hospitali zake za Wilaya?

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lishe bora ni muhimu sana kwa watu wote ili kupata afya bora. Kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi, lishe bora ina umuhimu mkubwa zaidi kwani huboresha kinga ya mwili ambayo husaidia kuepusha magonjwa ya kutegeshea (*Opportunistic Disease*) na pia huchlewesha mwili kuonyesha dalili za Ukimwi baada ya kupata maambukizi ya virusi. Tafiti zinaonyesha kuwa lishe duni huchangia vifo vya watu wenyе Ukimwi kwa kiwango cha asilimia 60 - 80.

Lishe bora ni yenyе chakula cha mchanganyiko, kilichokamilika na kutosheleza kama ifuatavyo:-

(1) Protini, hii ni muhimu kwa kujenga mwili wa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi wanaongezeko la mahitaji ya protini kwa asilimia 50 hadi 100.

(2) Wanga (*Carbohydrates*), vyakula hivi hutoa nguvu mwilini na kuupa mwili joto. Watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi wanaongezeko la mahitaji ya wanga kwa asilimia 10 hadi 15.

(3) Vitamini, hivi ni virutubisho ambavyo kazi yake ni kulinda mwili usishambuliwe na magonjwa. Vitamini za A, B, C na E ndio muhimu zaidi.

(4) Mwili unahitaji *Micronutrients* hususan Zinc ambayo hupatikana kwenye nyama, samaki, kuku na *Selenium* ambayo hupatikana kwenye nyama, mayai na nafaka zisizokobolewa.

(b) Mheshimiwa Spika, hakuna ukweli wowote kuwa wanawake waliokeketa hawaambukiziwa ugonjwa wa Ukimwi kwa urahisi. Kitendo cha kukeketa kikifanywa katika hali isiyo takaswa (*Sterile*) kinaweza kuchangia kuenea kwa Ukimwi. Kwa maelezo hayo ni wazi kuwa tabia ya kukeketa wanawake haina nafasi yoyote katika udhibiti wa ugonjwa wa Ukimwi na ni hatari sana kwa afya ya uzazi wa mama. (*Makofifi*)

(c) Mheshimiwa Spika, kuna aina mbili kuu za dawa za kurefusha maisha ya watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi. Dawa hizo ni zile za kutibu magonjwa ya kuegeshea yaani *Opportunistic Diseases* na zile zinazolenga virusi vya Ukimwi moja kwa moja yaani *anti-retrovirals*. Aina ya kwanza ya dawa zinapatikana kwenye hospitali zote za Wilaya ikiwa ni pamoja na dawa za Kifua Kikuu na dawa nyingine za aina ya *Antibiotics* na *Anti-fungal*.

Kuhusu dawa ya aina ya pili yaani *Anti-retrovirals*, ambazo hazipatikani kwenye hospitali za Wilaya kutokana na bei zake kuwa za juu sana. Dawa hizi hugharimu wastani wa dola moja ya Marekani kwa siku kwa kila mgonjwa na zinabidi zitumike kwa maisha yote ya mgonjwa.

Aidha, yanahitajika maandalizi mengi ya mfumo wa afya ikiwa ni pamoja na kununua vifaa vya kuwapa mafunzo watumishi wa afya ili waweze kusimamia matumizi salama ya dawa hizo pamoja na ufuatiliaji wa *CD4 Cells* kwa kuelewa hali ya mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali inawasiliana na wahisani mbalimbali ili kuona uwezekano wa kugharamia shughuli zote hizo zinazohusiana na matumizi ya madawa ya *Anti-retrovirals*. Pindi juhudzi za Serikali zikifanikiwa, basi usambazaji wa dawa hizo utaanza na Hospitali za Rufaa, Mikoa na hatimaye za Wilaya. Utaratibu wa namna hii ni lazima kwa vile ngazi zote hizo zitakuwa na majukumu yake ambayo yanategemeana na lazima uwepo mfumo wa rufaa ili kushughulikia matatizo mbalimbali ambayo yanaweza kujitokeza kutokana na matumizi ya dawa hizi. (*Makofi*)

MHE. JOHN L. MWAKIPESILE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Ningependa vile vile kuishukuru Serikali kwa juhudi zake inazozifanya ili kuwashudumia hawa wagonjwa wa Ukimwi. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa kuna *NGOs* nyingi sana zilizojitokeza Mikoani na Wilayani ambazo zinapata pesa nyingi, mamilioni ya pesa kutoka kwa wafadhili nchi za nje ili kuweza kuwashudumia wagonjwa wa Ukimwi; na kwa kuwa *NGOs* nyingi zikipata pesa kazi kubwa ambazo zinaifanya ni kununua *T-shirt*, kofia na kuendesha semina nyingi soko kubwa likiwa ni jinsi ya kutumia kondom badala ya kuwashudumia wagonjwa; je, Serikali kwa kutumia Sheria ya *NGOs* ambayo tuliipitisha mwaka 2002, haiwezi kuanza kuratibu shughuli za hizi *NGOs* ili fedha zote wanazopata kutoka kwa wafadhili kutoka nje ziweze kuwashudumia wagonjwa moja kwa moja badala ya kununua *T-shirt* na kofia? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, katika mapambano dhidi ya Ukimwi kuna njia za aina tatu ambazo zinaweza kutumika. Kuna njia zinazolenga kinga, kuna njia zinazolenga tiba na kuna njia zinazolenga huduma kwa wale walioathirika au watoto yatima.

Ninavyofahamu ni kwamba kuna *NGOs* zinazofanya kazi katika maeneo yote hayo. Sasa zile *NGOs* ambazo zinafanya kazi katika maeneo ya kinga, ni wazi basi moja ya kazi zinazofanya katika kinga ni kutoa semina ili kuwaelimisha watu juu ya ugonjwa wenyewe na vile vile kuhakikisha ya kwamba wanatoa maelezo kuhusu matumizi ya *condom* na vitu kama hivyo. Hizo ndiyo kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, wapo wanaoshughulika na tiba na pia wapo wanaoshughulika na *care* au tuseme malezi ya watoto yatima na kuwaangalia wale walioathirika. Kwa hiyo, kila mtu ana eneo lake katika mapambano haya. (*Makofit*)

MHE. ROSEMARY H. K. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba, lishe inasaidia kuongeza muda wa maisha ya muathirika na pia inasaidia kuongeza muda kabla hajaanza kutumia *Anti-retrovirals*; je, Serikali haioni ni muhimu kwamba itangaze elimu hiyo ya lishe kwa juhudhi sana kuliko hasa ile au kama ile ya kutumia *condoms*; na pia ikishirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula hicho chakula kiweze kuzalishwa na kutumiwa kwa waathirika hasa ukizingatia ya kwamba gharama ya kusambaza *Anti-retrovirals* ni kubwa sana, yapata zaidi ya shilingi bilioni 700 kwa mwaka? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba lishe ina kazi kubwa katika kuhakikisha muathirika hapati yale magonjwa yanayosababishwa na udhaifu wa kinga. Lakini naomba ieleweke kwamba tunapozungumza lishe, tunazungumza mtu ambaye tayari amekwishaathirika. Mkakati mkubwa wa Serikali ni kuhakikisha ya kwamba kwanza tuna kinga kabla hatujatibu aidha, kwa kutumia dawa au kutumia lishe. Ndiyo maana mtaona ya kwamba kinga inapewa umuhimu zaidi na matangazo na elimu kuhusu *condom* inapewa kipaumbele zaidi kwa sababu inasababisha mtu akingwe, hivyo anaweza kuwa haitaji aidha, lishe au madawa tuliyoyazungumza.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi, nataka niseme tu kwamba lishe imepewa kipaumbele vile vile lakini ieleweke kwamba haina umuhimu kuliko kinga kwa sababu kinga ni bora kuliko tiba mara zote na ina gharama nafuu ndiyo maana tumekuwa tunaweka msukumo mkubwa katika kinga. Lakini kwa sababu nchi yetu sasa hivi waathirika tayari wamekwishakuwa zaidi ya milioni 200 kwa hiyo, kipaumbele vile vile kitapewa katika masuala ya lishe ili wananchi walioathirika waweze kupunguza ule muda au kuongeza muda kabla hawajaanza kupata magonjwa.

Na. 96

Kambi ya Wakimbizi ya Mkuyu

MHE. JUMA S. KIDUNDA aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Kimataifa linalohudumia wakimbizi (*UNHCR*) limekuwa likiwahudumia wakimbizi kutoka Somalia katika Kambi ya Mkuyu iliyoko Handeni ya zamani kwa zaidi ya miaka kumi sasa; na kwa kuwa baada ya kufahamika kuwa wakimbizi hao wangehamia kwenye kambi nyingine, Uongozi wa Wilaya ya Handeni ya zamani ulifanya mazungumzo na Shirika la *UNHCR* kuhusu misaada na vifaa mbalimbali

kutoka kwenye shirika hilo ili uanzishwaji wa Shule ya Sekondari inayotarajiwa katika majengo ya kambi hiyo ufanyike kwa ufanisi:-

(a) Je, ni vifaa gani ambavyo shirika hilo limeshawishika na kuamua kuviacha Mkuyu kama mchango wake katika kuimarisha shule hiyo?

(b) Je, ni misaada gani mingine ambayo Shirika limetoa au limeahidi kutoa zaidi ya vifaa vilivyopo Kambini?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Juma Kidunda, Mbunge wa Kilindi, swalii lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya uamuzi wa kuanzishwa kwa Kambi ya Mkuyu kule Handeni kwa ajili ya wakimbizi wanaotoka Somalia wenyewe asili ya Kizigua mwaka 1992, Shirika la *UNHCR* lililazimika kufanya ukarabati wa majengo yaliyokuwepo. Majengo haya yalikuwa yanamilikiwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na iliamuliwa yatumike kama mabweni ya wakimbizi. Wakati huo huo, *UNHCR* ilijenga majengo mapya kwa ajili ya kuanzisha kituo cha polisi, nyumba za askari, shule ya msingi, zahanati na huduma nyingine za msingi kuwawezesha wakimbizi kuishi katika eneo hilo.

Aidha, kuanzia mwezi wa Aprili, 2003 wakimbizi wa Somalia walihamishiwa katika makazi mapya katika Kijiji cha Chogo huko huko Handeni na sasa yanafanyika maandalizi ya kukabidhi majengo na eneo la Kambi ya Mkuyu kwa Uongozi wa Mkoa wa Tanga ili litumike kuanzisha Shule mpya ya Sekondari. Pamoja na majengo yanayokabidhiwa vile vile vifaa vifuatavyo ambavyo vimeachwa na *UNHCR* vitakabidhiwa. Vifaa hivyo ni pamoja na Mashine ya kusukuma maji, aina ya *Lister Peter (3 piston)* na vifaa vingine vya mfumo wa kusambaza maji, vile vile kuna *generator* kubwa ya umeme yenye kilovoti 16, jengo ambalo limejengwa kwa makontena yenye ukubwa wa futi 20 ambalo linaweza kutumiwa kama ofisi na kuna madawati 201.

(b) Mheshimiwa Spika, *UNHCR* Ofisi ya Dar es Salaam inawasiliana na Makao Makuu ya Shirika hilo Geneva ili kuomba kibali cha kuruhusiwa kutoa misaada mingine kama gari, kompyuta na kadhalika kwa ajili ya kusaidia shule ya sekondari itakayoanzishwa hapo Mkuyu. (*Makofi*)

MHE. JUMA S. KIDUNDA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swalii moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa kukaa katika Kambi hii kwa muda wa miaka zaidi ya kumi wakimbizi wamefyeka misitu yote ambayo inazunguka Ziwa la Mkuyu na kulifanya ziwa hilo sasa liwe linakauka kila baada ya miaka michache; je, Serikali ikishirikiana pamoja na Shirika la *UNHCR* ina utaratibu gani wa kurejesha mazingira ya misitu inayozunguka bwawa hili ili kusudi hali yake ya awali irejee? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu mazingira yaliyoharibiwa na wakimbizi katika eneo la Mkuyu, nataka nimhakikishie ya kwamba tumeipokea na tutawasiliana na *UNHCR* kuona namna ya kutatua tatizo hili. (*Makofi*)

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inatambua ya kwamba wakimbizi hawa kutoka Somalia wana asili ya Kizigua, kabilia lililopo Tanzania, hali inayoonyesha ya kwamba wakimbizi hawa wamerudi katika nchi yao ya asili; je, Serikali ina mpango gani wa kuhalalisha uraia wao? (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba hawa wakimbizi wa Somalia ni wa asili ya Tanzania, ni Wazigua pamoja na kukaa Somalia kwa miaka 300, walikwenda kama watumwa, lakini mpaka leo bado wanazungumza vizuri tu Kizigua na ndiyo maana hatukuwapeleka waliko wakimbizi wale wa Burundi na Rwanda, kule hatukuwapeleka, tuliwapeleka Handeni kwa kutambua asili hii, kwa Wazigua wenzao.

Kwa hiyo, kwa sababu walishapoteza uraia wa Tanzania baada ya kukaa kule Somalia kwa miaka 300, wakawa raia wa Somalia, hivi sasa wanatakiwa waombe rasmi uraia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria zetu. Nina hakika watayatazama vizuri tu maombi yao kama yakiletwa. (*Kicheko/Makofi*)

Na. 97

Walinzi wa Jadi - Sungusungu

MHE. LUCAS L. SELELII (k.n.y. MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA) aliuliza:-

Kwa kuwa walinzi wa Jadi - Sungusungu kwa muda mrefu wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya kudhibiti hali ya wimbi la wizi na kulinda usalama wa raia katika sehemu mbalimbali nchini hivyo kuleta hali ya amani na utulivu mionganoni mwa jamii; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais alitoa wito kwa wananchi kujilinda wao wenyewe kwa maslahi yao na ya Taifa kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali inatambua na kuthamini kuwepo kwa Sungusungu kama sehemu muhimu ya ulinzi wa usalama wa raia?

(b) Ikiwa Serikali inalitambua hilo; je, haioni kuwa ni vyema kuwepo kwa Sheria ndogo itakayowalinda walinzi hawa wa jadi dhidi ya maonevu au migongano na Askari Polisi ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa kutoelewana na walinzi hao?

(c) Je, kwa nini Sungusungu wasipewe kila aina ya ushirikiano na Serikali pamoja na Jeshi la Polisi ili wasaidie katika kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chegeni R. Masunga, Mbunge wa Busega, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na inathamini sana kazi nzuri za Sungusungu wanazozifanya huko Vijiji na mitaani pamoja na wananchi kwa ujumla wanaoshiriki katika ulinzi wa umma ambao ni chimbuko muhimu la kufichua wahalifu ndani ya jamii. Ni kutokana na mchango mkubwa wa walini wa Sungusungu, Taifa letu limeweza kuendelea na hali ya utulivu, usalama na amani iliyopo hivi sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa kuhusu migongano au maonevu wanayofanyiwa walini wa Sungusungu na Jeshi la Polisi. Inachojua Serikali ni kuwapo kwa uhusiano mzuri kati ya vyombo vya ulinzi na usalama ikiwa ni pamoja na Sungusungu. Ili kuweka wazi majukumu ya ulinzi wa Sungusungu Sheria Na. 25 ya mwaka 1975 ilitungwa ili kuwapa wana mgambo uhalali wa Kisheria. Sheria hii ilirekebishiwa na Sheria Na. 9 ya mwaka 1989. Sheria hii inawapa walini wa Sungusungu na wanamgambo madaraka ya kutosha kabisa na kwa sasa hakuna haja ya kutunga Sheria nydingine. Sheria hii pia imewapa walini wa Sungusungu uwezo wa kufanya kazi za ulinzi bila kugongana na Polisi, Sheria hiyo inatoa mipaka ya madaraka ya walini wa Sungusungu wanapokuwa kazini. Katika hali hiyo, migongano na Polisi inaweza kutokea tu pale mmojawapo anapokiuka utaratibu wa Sheria.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kiwango kikubwa upo ushirikiano mzuri kati ya Jeshi la Polisi na walini wa Sungusungu katika kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu kuhusu mbinu za ulinzi na Sheria kwa walini wa Sungusungu kuititia mafunzo ya mgambo ili kuwasaidia kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao katika kusimamia Sheria chini ya dhana ya Utawala Bora.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanaeleza kwamba migongano hakuna. Lakini kwa utaratibu wa Serikali, muda mrefu ambapo kunakuwa na amani yaani majambazi hakuna na wizi umepungua, Sungusungu huwa wanakuwa kama wamesahaulika lakini majambazi yakizidi au uhalifu ukizidi Serikali huwakumbuka Sungusungu na kusema wao wajilinde; na katika hilo hutokea migongano pale ambapo Askari wa Sungusungu wanapotekeleza ndiyo maana kuna wafungwa ambao wamefungwa katika migongano hiyo; je, Serikali ipo tayari kutambua katika kazi wanayoifanya Askari wa Sungusungu, yapo makosa yanayoweza kutokea hivyo migongano ikasuruhishwa ndani kwa ndani ili kuacha kuondoa ari ya walini hao wa usalama wanaojitolea?

Mheshimiwa Spika, pili, wizi wa mifugo umekomeshwa na walini hao wa Sungusungu katika Mikoa yetu ya wafugaji; lakini bado majambazi ya sasa yanatumia silaha kali ambazo ni tishio kwa walini wanaotumia upinde na mapanga; je, Serikali ipo

tayari kuungana na angalau askari wawili au watatu katika kundi la Sungusungu ambao watakuwa tayari kuwa na silaha ili kujilinda wao wenyewe? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya kwanza bado nasisitiza kwamba hakuna mgongano wala uhusiano mbaya kati ya Polisi na Sungusungu katika ujumla huo. Inapotokea kwamba Sungusungu amefungwa si kwa sababu ya mgongano kati ya Polisi na Sungusungu, ni kwa sababu tu huyo Sungusungu katika kutekeleza majukumu yake amepitiliza na amekiuka Sheria. Hilo si kwa Sungusungu tu ila hata Polisi naye vile vile katika kutekeleza majukumu yake akivunja Sheria vile naye anapata adhabu hiyo hiyo mbele ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu zana za kutumia Sungusungu, nataka kumhakikisha Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu kwamba, katika yale maeneo ambapo kuna Vituo vidogo vya Polisi huko Vijijini, tumetoa maelekezo ya kwamba Sungusungu wanapokwenda katika ulinzi wao basi waungane na Polisi wenyе silaha katika kufanya doria.

Na. 98

Uhamasishaji wa Pato la Taifa

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI (k.n.y. MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na tuhuma kuwa Pato la Taifa linavushwa kwenda nje ya nchi:-

(a) Je, Serikali inafanya udhibiti upi ili kuhakikisha kuwa wawekezaji hawahamishi pato la Taifa?

(b) Je, Serikali inawadhibiti vipi wafanyabiashara wenyе asili ya Kiasia ili kuhakikisha kuwa hawahamishi faida yote wanayoipata katika biashara wanazozifanya hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wawekezaji katika uchumi wako wa aina mbili. Kuna wawekezaji wageni na wawekezaji raia.

Katika sera ya Taifa ya uwekezaji, wawekezaji wageni wamekaribishwa kuwekeza hapa nchini ili kuongeza pato la Taifa. Njia kubwa ya kuwavutia ni kuhakikisha kuwa hali ya uchumi wetu ni tulivu na endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika nchi nydingi ambazo zina matatizo ya kiuchumi, Pato la Taifa linaweza kuhamishwa na kupelekwa nje. Hii inatokana na hofu inayojijenga baina ya wawekezaji kuhusu matumaini finyu ya kiuchumi katika nchi hizo. Pia nchi ambazo zina matatizo ya kisiasa ambayo husababisha kukosekana kwa amani, nazo pia hupata matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni Tanzania imenufaika sana na ukuaji wa raslimali toka nje, tofauti na hapo zamani ambapo raslimali zetu ziliwu zinotoroshwa kwenda nje. Hii inaonyesha kuwa hatua zilizochukuliwa na Serikali kurekebisha uchumi, zimesaidia sana kupunguza kasi ya uhamishaji wa Pato letu la Taifa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango mwingine maalum wa kuwadhibiti wafanyabiashara wenye asili ya Kiasia au wowote wale ili kuhakikisha kuwa hawahamishi faida wanayopata. Sera na Sheria za Serikali haziongozwi na Utaifa au asili ya mwekezaji.

Serikali inatoa Uhuru kwa wawekezaji wa Mataifa ya kigeni kuitumia faida wanayoipata kutokana na shughuli zao popote pale wanapotaka, ikiwa ni pamoja na hapa hapa Tanzania. Wawekezaji wa Tanzania hata hivyo, hawaruhusiwi Kisheria kuhamisha faida ya biashara zao na kuipeleka nje ya nchi, isipokuwa kwa kibali maalum cha Benki Kuu.

Kwa hiyo, wafanyabiashara wenye asili ya Kiasia ambao ni Watanzania wanatawaliwa na Sheria hii kama Watanzania wengine wote. Serikali kuitia vyombo vyake vya dola, inahakikisha kuwa Sheria hii haivunjwi.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili mazito ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, japo swalii liliwu linaliliza kwa ujumla wake; na kwa kuwa uvushaji wa Pato la Taifa kama wanavyofanya wale wenye ndege binafsi wanaokuja kwenye migodi na hakuna anayezikagua; na kwa kuwa wengine wanasomba mchanga kwa hiyo wanaweza wakaacha mabonge makubwa makubwa kama ya tani mbili kwenye mchanga huo, ndicho kitu tulichokuwa tunakisema kwamba Serikali imekichunguza?

Mheshimiwa Spika, pili, pamoja na ujumla wa swalii hili, Serikali iko tayari kumkaribisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na mimi ili tukae wote tuwaeleze ni vitu gani vinavyohamishwa na baadaye tuvifanyie utafiti? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, swalii ambalo limeulizwa katika sehemu ya kwanza na Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alieleza katika hotuba ya Bajeti na kwamba suala la madini linafanyiwa uchunguzi na utafiti mpya kuangalia maeneo gani na ndiyo maana suala la msamaha wa kodi wa *subcontracts* lilifanyiwa marekebisho kulingana na hali halisi. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema ana ushahidi

unaoonyesha ni jinsi gani Pato la Taifa linapelekwa nje kinyume cha Sheria, basi tuko radhi kuongea naye na tutayafanyia kazi hayo aliyonayo. (*Makofit*)

Na. 99

Matumizi Mabaya ya Misamaha ya Kodi

MHE. MGANA I. MSINDAI (k.n.y. MHE. LEONARD M. SHANGO) aliuliza:-

Kwa kuwa sababu kubwa iliyomsababisha Waziri wa Fedha kufuta Misamaha ya Kodi kwa manunuzi ya Halmashauri na Mashirika ya Kidini wakati akiwasilisha Bajeti ya mwaka 2002/2003 ni matumizi mabaya ya Misamaha ya Kodi hiyo:-

(a) Je, Serikali inakubaliana nami kuwa kwa kufuta misamaha ya kodi kwa manunuzi ya Halmashauri ni sawa na kuwaadhibu kwa kuwabebesha mzigoto wa kodi (*Indirectly Shifting Tax Incidence*) wananchi wa kawaida na kuzorotesha maendeleo Vijiji ni kwani Halmashauri zitafanikisha manunuzi ya vifaa muhimu kwa bei ya vifaa vinavyohitajika pamoja na kodi zote za Serikali kulipwa?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuutazama upya uamuza wake wa kufuta misamaha ya kodi kwa Serikali na Taasisi zake kwa lengo la kurejesha misamaha ya kodi kwa manunuzi ya vifaa muhimu hasa vinavyohitajika kwa kufanikisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii kwenye Halmashauri?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka 2002/2003 Serikali imefuta misamaha ya kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), ushuru wa forodha na bidhaa kwenye bidhaa zote zinazoagizwa na Serikali pamoja na asasi zake zikiwemo Halmashauri za Jiji, Miji, Wilaya na Manispaa. Kutokana na mabadiliko yaliyofanywa Wizara, Idara na Halmashauri zinatakiwa sasa kuandaa Bajeti inayojumuisha malipo ya kodi.

Aidha, siyo kweli kwamba Mashirika ya Kidini yamefutiwa misamaha bali yataendelea kupata misamaha hiyo kama ilivyokuwa siku za nyuma. Hata hivyo, Serikali itaongeza mbinu za kudhibiti misamaha ya mashirika hayo ili isitumiwe vibaya kinyume na ilivyokusudiwa. Sambamba na jitihada hizi, Serikali pia imeweka utaratibu utakaowezesha mashirika yasiyo ya Kiserikali wala ya kidini (*NGOs*) ambayo yamesamehewa kodi kuagiza bidhaa na kutumia Vocha za Hazina (*Treasury Voucher*) kupata bidhaa hizo kwa ajili ya miradi mbalimbali inayolenga kutoa huduma za jamii bila kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa Mashirika na Taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali katika kupanua huduma za jamii. Kwa upande wake Serikali imekuwa inatoa msamaha wa kodi kwa Mashirika na Taasisi zisizo za Kiserikali ili kutoa unafuu kwa vyombo hivyo na kuboresha huduma kwa kiwango cha juu.

Hata hivyo, Serikali imegundua kwamba utoaji huo wa misamaha bado unaiongezea Serikali mzigo kwani athari zake zimejionyesha waziwazi baada ya kuwepo kwa uvujaji wa mapato na kuharibu mfumo mzima wa uchumi. Kwa mfano, baadhi ya Taasisi hizi zinapendelea zaidi kununua bidhaa kutoka nje ya nchi kwa sababu zinapata msamaha wa kodi, kuliko kununua bidhaa hizo nchini kwa bei zinazojumuisha kodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swal la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kufuta misamaha ya kodi ya *VAT* kwa manunuza ya *NGOs*; Serikali itakuwa inajenga uwezo wa kifedha utakaoziwezesha kugharamia mipango ya kawaida na ya maendeleo katika maeneo ya Miji na Vijijini.

(b) Mheshimiwa Spika, kurejesha misamaha hiyo ya kodi itakuwa kinyume cha sera ya Serikali ya kupambana na ukwepaji kodi uliokuwa unafanywa na watu wasio waaminifu. Nia ya Serikali ni kuona kuwa misamaha ya kodi inapunguzwa kwa kiasi kikubwa au kufutwa kabisa na kwamba kila raia anatimiza wajibu wake wa kulipa kodi.

Aidha, kutokana na Serikali kuanzisha utaratibu wa kutumia *Voucher* za Hazina, udhibiti wa baadhi ya misamaha ya kodi umeimarika. Utaratibu huu kwa kiwango kikubwa umesaidia kudhibiti wimbi la maombi ya misamaha ya kodi kutoka kwenye mashirika ya kujitolea pamoja na watumishi wa Serikali. Katika kipindi cha miezi sita ya utekelezaji wake yaani kuanzia mwezi Januari hadi Juni, 2003, misamaha yenyenye thamani ya shilingi 1,500 milioni ndiyo inayotegemewa kutolewa, ikilinganishwa na makisio ya shilingi 13,500 milioni kwa kipindi hicho, hii ni sawa sawa na asilimia 11 ya makisio.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha itaendelea kushirikiana na Wizara na Idara nyininge za Serikali Kuu na pia Serikali za Mitaa ili kufanikisha lengo la Serikali kulipa kodi na kubana au kufuta kabisa misamaha isiyo ya lazima.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swal moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri zote zilishakubali mtindo huu wa kulipa kodi na kwa kuwa sasa hivi mapato ya Halmashauri yameshuka sana baada ya vyanzo vyao vingi kuondolewa, je, Serikali itakuwa tayari kuwatafutia ruzuku ili waendelee kununua bidhaa na kulipa kodi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha imeeleza na

imeainisha vyanzo vya kodi ambavyo vimefutwa ikiwa ni pamoja na Kodi ya Maendeleo lakini kuna utaratibu ambao umeandaliwa kwa ajili ya kufidia pengo hilo kutoka Serikali Kuu.

Kwa hiyo, itakayotolewa ni *top up* kama ruzuku kwa maana ya kwamba kile chanzo cha mapato ambacho kimeondolewa kutokana na kodi hii inayofutwa basi Serikali Kuu itatoa fedha kwa Halmashauri zote kufidia pengo hilo. Lakini haina kwamba basi kwa *top up* hii Halmashauri hizi ziache kulipa kodi, zitaendelea kulipa kodi kama kawaida na *top up* itakayokuwa imetolewa itatolewa tu kwa kodi ambazo zitakuwa zimefutwa lakini sio kwa kodi ambazo zinatakiwa zilipwe na Halmashauri.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ni chombo cha wananchi kwa faida ya wananchi na kwa kuwa Serikali yenewe ndio inakusanya kodi, hivi kuna mantiki gani tena Serikali yenewe ikalipa kodi, inatoa wapi pesa nyingine kama sio zile zile zinajirudia?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, Serikali ni mdau wa uchumi kama wadau wengine katika jamii, kwa hiyo kama Watanzania wanalipa kodi, *NGOs* zinalipa kodi, mashirika yanalipa kodi na Serikali kama mdau katika uchumi inabidi ilipe kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa Serikali kutolipa kodi ilikuwa inainyima Serikali mapato mengi kwa sababu watu walikuwa wanajificha kwa kusema kwamba hii ni ya Serikali, hii ni ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeseme Serikali italipa kodi na kwa Serikali kulipa kodi tumengudua kwamba sasa kodi inakusanya kwa wingi zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Japokuwa ni mkono ule ule unachukua kwa mkono mmoja unatoa kwa mkono mwagine lakini inasaidia Serikali kuhakikisha kwamba kodi inakusanya na sasa inakusanya kwa wingi zaidi kuliko huko nyuma. Mafanikio ya ukusanyaji wa kodi yametokana pia na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali la msingi, nilisema kwamba utaratibu ambao umeanzishwa wa *voucher* za Hazina, katika kipindi cha miezi sita toka Januari mpaka Juni, ilikuwa imekisiwa kwamba Serikali ingetoa misamaha ya shilingi milioni 13,500 kulingana na takwimu za huko nyuma lakini kiasi hasa kilichosamehewa ni shilingi milioni 1,500.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inaonyesha ni jinsi gani kwa utaratibu huu wa *voucher* na utaratibu wa Serikali kulipa kodi kumeweza Serikali kubana mianya ya ukwepaji kodi na pia sasa kodi zinalipwa kwa wingi zaidi. Ni matumaini yetu kwamba katika mwaka ujao wa fedha kiasi cha makusanyo ya kodi yataongezeka zaidi kwa kiasi kikubwa kuliko ilivyo sasa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha, hakuna matangazo, kwa hiyo, moja kwa moja tunaendelea na *Order Paper*, Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 - Ofisi ya Waziri Mkuu

(*Majadiliano Yanaendelea*)

MHE. ANATORY K. CHOYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii asubuhi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa namna ya pekee, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri yenyenye mwelekeo. Kwa kweli imeonyesha namna anavyojali yale yote ambayo Watanzania wamekuwa wakiyahitaji ili wafanyiwe na Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nijielekeze kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kufutwa kodi. Kodi hii ya Maendeleo kwa namna moja au nyingine ilikuwa ni kero kwa wananchi, lakini Mwenyezi Mungu ameijalia Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kero hii inaondolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki sio kipindi cha malumbano kwamba ni nani ameshiriki katika kuiondoa Kodi ya Maendeleo. Sasa hivi Watanzania hatupaswi kuanza kuvutana kuhusu itikadi, itikadi haina maana yoyote katika nchi zinazoendelea. Wanaopaswa kugombania na kuvutana kwa ajili ya itikadi ni wale waliokwishaendelea sisi tunatafuta mambo ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kati yetu ni nani ambaye hajui timu mbili zinapokuwa zinacheza mpira hata kama una uwezo wa kupiga chenga kwa utaratibu upi, hata kama utapeleka mpira wako kichwani lakini ukiufikisha kwenye goli kabla ya kufunga goli hautapata sifa? Chama cha Mapinduzi ndicho kimefunga goli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tusiendekeze sana haya malumbano ya itikadi na nawaasa Watanzania wenzangu kwamba kipindi hiki sio cha kulumbana, cha msingi ni kuhakikisha tunatafuta maendeleo. Watanzania wenzangu msifuatilie sana wale wanaolumbana tufuate ile methali ya wahenga wetu unapoona kundi na kundi wanalumbana, kiongozi mmoja na mwingine wanalumbana wewe chukua jembe lako nenda kalime watakapatana hebu chukua kikapu ukavune.

Hawa wanaolumbana Waheshimiwa Watanzania wenzangu mnaonisikiliza wanaonekana wameshiba, kama hujashiba huwezi kulumbana na mtu. Kwa hiyo,

Watanzania kamwe msifuate malumbano. Kipindi hiki ambacho Kodi ya Maendeleo imefutwa ni wakati muafaka kuhakikisha tunafanya kazi kwa bidii, juhudhi, maarifa na malengo ili tuondokane na umaskini ambao umekithiri mionganoni mwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Watanzania sasa tumeshapata ile hali ya utulivu wa moyo, utulivu katika maisha yetu, ni wakati wa kuutumia ili tusije kuujutia kwa sababu Mtanzania siku zilizopita alikuwa anaishi bila raha, matokeo alikuwa hafanyi kazi za kujitegemea. Kwa kipindi hiki Mtanzania yeoyote ahakikishe anafanya kazi kwa bidii ili afidie ule muda aliokuwa anaupoteza wakati alipokuwa anakwenda kujificha kukimbia Kodi ya Maendeleo.

Watanzania walijificha, walikosa raha kwa sababu ya Kodi ya Maendeleo. Sasa huu ni wakati ambapo Waisraeli wametoka Misri wanakwenda kwenye nchi inayofuka asali na maziwa. Hiyo nchi inayofuka asali na maziwa Watanzania hatutaifikia bila kufanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hiki baada ya Kodi ya Maendeleo kufutwa, nawaomba Waheshimiwa Madiwani tusaidiane kuwaelekeza Watanzania mahali pa kwenda. Kipindi hiki ni kipindi cha kufanya mambo mawili yafuatayo.

Kwanza, Waheshimiwa Madiwani wamekuwa wakilalamika kwamba posho zao ni ndogo, ni kweli zilikuwa ndogo ambapo zilikuwa haziwasaidii kuhakikisha wanatimiza majukumu yao. Kigezo kilichokuwa kinatumwa katika kuhakikisha kwamba Waheshimiwa Madiwani wanalipwa posho kilikuwa ni kigezo cha mapato ya Halmashauri na mapato ya Halmashauri yalipatikana kutokana na Kodi ya Maendeleo ambapo ndio chanzo kikubwa cha mapato ya Halmashauri sasa Kodi ya Maendeleo imefutwa na Serikali Kuu ita-top up kwa hiyo, sasa hivi lazima kwa uwezo wa kufikiri na kutenda wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa uwezo wa kufikiri na kutenda, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, kwa uwezo wa kufikiri na kutenda wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa huu ni wakati muafaka wa kukaa na kutafakari kwa kina na kwa namna ya pekee kabisa yakafanya *review* ya posho ya Madiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Madiwani wamekuwa wakilalamika na malalamiko yao ni ya kweli tupu. Kwa mfano katika Kata yangu ya Nyamigogo ukitoka barabara kuu kwenda Kata ya Nyamigogo mpaka Kasozibakaya mahali ambapo kuna Mheshimiwa Diwani mmoja anaitwa Peter Mashenji, ili afike Wilayani kufuata hiyo posho anatakiwa asafiri kwa baiskeli na kutoka kule mpaka barabara kuu inamchukua zaidi ya saa tano inabidi itakapofika pale karibu na barabara kuu alale kwa sababu ile barabara ya kutoka Kabindi kwenda Kata ya Nyamigogo ni barabara mbaya ambayo hata kuitisha baiskeli mle itabidi ujishauri tairi uliweke wapi.

Kwa hiyo, atakapofika pale Kata ya Kabindi ili aende Biharamulo mjini anatakiwa atumie siku mbili na atakapofika kule Halmashauri atakuta ile posho bado itabidi alale *Guest*, ale chakula hotelini atakaporudi tena vile vile kwa hiyo posho hiyo haitoshi. Mfano mwingine katika Kata moja inaitwa Kigongo ni vile vile kwa

Mheshimiwa Diwani mmoja anayeitwa Mbanda, inabidi alale njiani akifuatilia posho ile. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huu ni wakati muafaka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Waziri wa TAMISEMI kukaa pamoja maana yake huo ni utatu kuhakikisha posho hizo zinapandishwa na kiwe kiwango kimoja kwa Tanzania nzima kwa Madiwani wote kwa sababu hakutakuwepo na kigezo cha mapato ya Halmashauri. Kwa hiyo, ile *top up* lazima ifikirie kwa namna ya pekee kuhakikisha kwamba hizi posho za Waheshimiwa Madiwani zinapandishwa ili nao waweze kutimiza wajibu wao kama wadau wengine wanavyotimiza wajibu wao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimeyasema haya kutokana na uzoefu wa Waheshimiwa Madiwani wanavyolalamika. Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa kwenye vikao Waheshimiwa Madiwani wanalamika na malalamiko yao ni ya kweli tupu kwa sababu hatuwezi kusema malalamiko yao sio ya kweli ni kweli tupu kwa hiyo lazima yafikiriwe kwa namna ya pekee. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda nijielekeze kwenye vyombo vyahabari, lakini kabla sijafika huko, naomba ninukuu maneno ya mtalaam mmoja ambaye alisema hivi: “*Politicians and Journalists share the same fate in that they often understand tomorrow the things they talk about today*”. Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Waandishi wa Habari ni kiungo kizuri sana kati ya Serikali, Wabunge na wananchi. Naomba *ITV* na *TVT* waanzishe vipindi maalum kama Redio Tanzania ionavyofanya. Redio Tanzania ina kipindi kinachoitwa Leo katika Bunge. Kwa hiyo, ndugu zangu wa *ITV* naomba muanzishe kipindi maalum ambacho hakitakuwa ni cha kuonyesha kama mtu labda anawindwa maana yake wananchi kule Majimboni huwa hawatuoni wengine wanauliza hivi Mbunge Choya ulikuwemo kwenye Bunge maana atatokea mara moja au asitokee kabisa. Sasa naomba *ITV* na *TVT* waanzishe vipindi maalum kwa ajili ya ku-cover zile shughuli za Waheshimiwa Wabunge hasa wakati wa kikao cha Bunge ili wananchi waelewe kinachoendelea waone ni namna gani Waheshimiwa Wabunge wanaishauri na kuisimamia Serikali yao. Tunaomba muanzishe vipindi maalum kwa ajili ya kuwaelimisha wapiga kura wetu waweze kuelewa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka nikimbilie kwenye kuhamia Dodoma. Suala la kuhamia Dodoma limekuwa ni kitendawili kama kila mmoja anavyoolewa. Waheshimiwa Wabunge sisi kuhamia Dodoma na kutokuhamia Dodoma sio kosa la Mbunge wala wananchi kila kitu kinalewewka hapa.

Mheshimiwa Mbunge kama kiungo kati ya mwananchi na Serikali anapata taabu wakati anapokuwa anatumwa majukumu fulani fulani kule Dar es Salaam na Wizara nyingi zipo Dar es Salaam. Anapokuwa Dar es Salaam, hivi Mheshimiwa Mbunge anawezeshwaje? Maana anatakiwa anapotoka hapa arudi moja kwa moja Jimboni lakini ametumwa majukumu fulani kwenda kuyafanya kule Dar es Salaam na Wizara zote ziko Dar es Salaam hizi nyingine Wizara ya Ushirika na Masoko, TAMISEMI, Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa mawazo yangu zipo kwa utaratibu fulani lakini anaweza kuja

mwingine akasema hazitakiwi kuwepo kwa sababu ataunganisha tena zikawepo tena nyingine. Sijui kama mmenielewa?

WABUNGE FULANI: Imeeleweka.

MHE. ANATORY K. CHOYA: Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ihakikishe inamwezesha Mbunge anapokuwa Dar es Salaam kufuatilia majukumu ya wananchi kwa sababu kuhamia Dodoma au kutohamia sio kosa langu. Ninapokuwa natumwa na wananchi kwenda kushughulikia masuala yao nikiwa Dar e Salaam natakiwa nipeleke majibu. Sasa nisipopeleka majibu nianze kumsukumia nani tatizo hilo? Basi itabidi tuanze kunawa mikono kwa kusema kwamba mimi nilikuwa naweza kwenda kufuatilia kule Dar es Salaam lakini sikuwezesha!

Mheshimiwa Spika, ninapokuwa hapa natakiwa walau nifanye *saving* nitakapokuwa narudi nyumbani watoto wapokee mkate wasipokee makaratsi. Sasa nitakapokwenda kule Dar es Salaam itabidi nihakikishe nimetumia kila *saving* ambayo niliifanya nikiwa Dodoma nitakaporudi kule nyumbani kwa kweli haitakuwa furaha kwamba baba yetu au Mbunge wetu amerudi mikono mitupu nikawapelekea haya makabrasha, watanishangaa sana. Kwa hiyo, naomba Serikali ituwezeshe kuhakikisha tunafanya kazi zetu vizuri tukiwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuzungumzia kuhusu makambi ya JKT. Kawaida imekuwa ni utaratibu kwa wale wanaotaka kujiunga na JKT wapitim kwenye Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ili wawe *screened* baada ya hapo inabidi tena waende Mikoani na kule tena wanakuwa *screened*, hivi utaratibu huu wa kuwachekecha mara mbili unatokea wapi? Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zinatosha. Nafikiri Mheshimiwa Profesa Phillemen Sarungi, angekuwepo angelichukua hili.

MBUNGE FULANI: Yupo.

MHE. ANATORY K. CHOYA: Tuhakikishe kwamba Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ndizo ziwe ni chombo chenye maamuzi ya mwisho.

(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kumalizika)

MHE. ANATORY K. CHOYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya kwa kuchaguliwa kwao kuja hapa Bungeni. (*Makofî*)

(Hapa King'ora cha Tahadhari ya Moto Kililia)

SPIKA: Hatari imekwisha, safari hii Spika hakukimbia, endelea Mheshimiwa Dr. William Shija. (*Kicheko*)

MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA: Mheshimiwa Spika, napenda nipewe upya nafasi yangu maana kengele inaweza kulia mapema. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mawazo yangu. Moja kwa moja, kwa niaba ya wananchi wa Sengerema, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wapya waliochaguliwa katika kipindi cha hivi karibuni kuja hapa Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hoja yake nzito kwa sababu inasimamia sehemu kubwa sana ya Serikali kama ndiye msimamizi wa utekelezaji wa mambo mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mapema kabisa, napenda kupendekeza kwamba katika kipindi kijacho hoja hii iwe inajadiliwa sambamba na hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mfumo ambao naufikiria ni kama ule wa asubuhi kusoma hotuba ya Mipango na mchana hotuba ya Bajeti. Majadiliano ya namna hiyo yangeweza kuja vizuri sana kwa maana ya kuoanisha mambo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu anayafanya, lakini yanahusiana sana na TAMISEMI. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nina mambo matatu na napenda kuyazungumza haraka haraka kwa sababu muda tuliopeana ni mchache la kwanza ni haki, utawala bora na kukua kwa uchumi. Pili, ni vyombo vya habari na tatu ni nafasi ya Bunge katika utawala bora.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza linalosema kwamba haki, Utawala Bora na kukua kwa uchumi vinahusiana sana katika mtiririko wa shughuli za wananchi wanaojaribu kujikombua katika umaskini ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Bajeti yetu inaonyesha kwamba sehemu kubwa sana ya bajeti huchukuliwa na Serikali Kuu na kuacha sehemu ndogo kwa Bunge na Mahakama kama nguzo mbili nyingine za utawala na uongozi wa nchi. Kwa kuwa tumekubaliana kwamba kiongozi ni vema akawa kiongozi mtumishi, ni bora siku zizazo tutazame namna ya uwiano wa Bajeti au mgawanyo wa Bajeti kati ya Serikali Kuu, Bunge na Mahakama ili tuweze kutoa nafasi zinazofanana katika utekelezaji wa kazi zake Kikatiba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kiongozi anapokuwa anashughulika na kazi zake vijiji, anasimamia watu kadhaa. Moja, anasimamia familia yake iweze kufanya kazi ili iweze kupata chakula pamoja na vitu vingine lakini ndani ya kijiji, Kata, Tarafa na Wilaya kuna viongozi ambao tumewaamini kwenda kusimamia ili wananchi waweze kufanya kazi zao na kuishi kwa ufanisi na tumepeana nafasi za uongozi katika vijiji, Kata mpaka kwenye Taifa na tulikubaliana kabisa tangu mwaka 1995 kwamba nidhamu, rushwa, kodi na utawala wa sheria ndio vitu ambavyo tutavifatilia kwa makini.

Nimegundua kwamba katika ngazi ya Wilaya ambapo wananchi wengi ndio wana mategemeo ya kupewa miongozo na kusaidiwa katika kazi zao mbalimbali ziwe za kilimo, katika shida zao za mambo ya afya na elimu, ni vema tukaimarisha uongozi na

usimamizi wa shughuli kule. Tulipotoa nafasi kwa Halmashauri zetu ziwe zinafanya shughuli zake bila kuwa na wahimili katika ngazi ya Mkoa na Wilaya, mawazo yangu yametuma kwamba tulikosea. Ni vema tukatazama upya sheria ile ili kusudi Wakuu wa Mikoa na Wilaya wakapata nafasi ya uhimili kwa sababu hali ya Halmashauri zetu nydingi ni mbaya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli Waheshimiwa Madiwani kule Wilayani wanafanya kazi nzuri wanajitahidi kama Mheshimiwa Anatory Choya, alivyomaliza kuzungumza, lakini bado katika Halmashauri kuna mambo mengi yanafanya kwa maana ya vituko. Mahali pengine utakuta Mkurugenzi wa Maendeleo au Mkurugenzi Mtendaji anafanya anavyoona pengine amewaweka baadhi ya Madiwani mfukoni wanatumia rushwa na vigezo vingine katika kufanya mambo ambayo sio sahihi kisheria.

Pia unaweza kukuta mahali Mwenyekiti wa Halmashauri amekuwa kama Mkurugenzi Mtendaji. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Serikali za Mitaa, anaweza kutueleza mambo mengi amegundua ambayo yanastahili kutazamwa kwa maana ya kusimamia Halmashauri zetu kwa namna mpya kwa sababu huko ndiko mwananchi anapoonyeshwa kwamba je, kuna Serikali ya Utawala Bora au hakuna. Hilo niliona ni lazima niliseme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lingine katika suala la Utawala Bora pamoja na haki, niseme mambo machache tu ambayo utakuwa ni mchango wangu kwa sababu tunapokuja hapa tunapenda kumpongeza Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kwa sababu tunajua ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, lakini vile vile kama Bunge tuna haki ya kutazama na kukosoa maeneo mbalimbali bila woga.

Kwanza, utaratibu wa ubinafsishaji na haraka haraka za ubinafsishaji unaofanywa na Serikali yetu, sisi wengine tumezungumza hapa Bungeni kwamba haufai. Ni muhimu baadhi ya maeneo makubwa haya yakaletwa Bungeni yakajadiliwa na kwa sababu hapa ndipo wawakilishi wa wananchi walipo. Hilo la kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la pili, suala la kuuza nyumba za Serikali na kusema kwamba Bunge liliidhinisha, sio Utawala Bora. Hata kama tutasemwa kwamba tuna wivu, hata kama ilisemwa hapa Bungeni kwamba sisi ambao tumekaa *backbencher*, sio sahihi. Nadhani jambo hili Mheshimiwa Waziri Mkuu, angelisimamia ili tukapata mtiririko mzuri wa namna ya kushughulika na suala la kuuza nyumba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuzungumza kirefu hapa Bungeni, nadhani tungeweka utaratibu wa kwamba kwenye mwezi wa Februari hivi Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake wangetuletea taarifa ya utekelezaji kwa miezi iliyokwisha ili tukapata nafasi ya kuzungumza juu ya mtiririko wa utekelezaji na mambo ya kiuchumi na kuandaa misingi ya Bajeti ijayo. Jambo hili nalizungumza kila mwaka na mwaka huu sipendi kuliacha, katika Mkutano wa Februari, kila mwaka tungeweka hata ukawa mrefu zaidi ili tukazungumza mambo ya kiuchumi na mipango na kukubaliana kipaumbele na hatimaye kuweka misingi ya Bajeti na hilo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ingeweza kufanyika Wizara sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutowaandaa vizuri viongozi wa ngazi za Wilaya na vijiji sio Utawala Bora. Hapa nina maana kwamba unapoteua Wakuu wa Wilaya unajua kabisa kwamba hawa bado hawajafundishwa mbinu kadhaa za utawala inawezekana wamepita mahali fulani fulani kisiasa na kadhalika lakini hawajafundishwa namna ya kutawala watu na kuwasimamia katika uongozi.

Kwa hiyo, ni busara tungkuwa tunawaweka katika utaratibu wa kuwafundisha wengine bado ni vijana wasifike kwenye Wilaya wakafikiri kwamba Mbunge ndiye adui yake. Mkuu wa Wilaya hawezi kuwa na adui Mbunge kwa sababu wanafanya kazi ya kuwasaidia wananchi lakini baadhi ya maeneo Wabunge wameonekana kama wanashindana na Mkuu wa Wilaya, sidhani hilo kama ni sahihi na wala sio Utawala Bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba kutosambaza Kitaifa haki ya uongozi sio Utawala Bora. Hapa nina maana tuangalie sana Taifa letu tumewekewa misingi mizuri na Baba wa Taifa, Marehemu Julius Nyerere, tusije kufika mahali Mikoa fulani ndio ikawa inatoa viongozi, wengine wanakuwa kama waongozwa tu. Hilo nalizungumza kwa sababu linazungumzwa huko *backbencher* na mimi nimeamua nilifumue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, wenzangu wamezungumza, tuna Bunge lako ambalo kwa uongozi wako tumejitahidi sana kufanya kazi kwa uadilifu pamoja na kusakamwa na vyombo vyaya habari mara kwa mara kwamba tuna mamilioni kumbe tuna madeni tu na *Salary Slip* zetu zinatoka na shilingi 15,000/= au shilingi 40,000/= kwa sababu ya kulipia vitu mbalimbali. Mimi nadhani Kikatiba tungekubaliana kwamba Mbunge lazima awezeshwe sasa kwa namna mpya na mfumo wa Bunge kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia waliyosema wenzangu lakini ni vizuri niyarudie. Mbunge amekuwa akifanya kazi kwa shida kweli kweli, maswali ya Bunge yanaonyesha kwamba hata Majimboni kwetu ofisi hatujajenga, hapa penyewe hatujatengeneza. Kwa nini basi zile shilingi 500,000,000/= za Chimwaga tusizitoe huko tukaziongezea kwenye ufanisi wa Bunge ili taasisi hii iweze kufanya kazi yake vizuri. Hata itifaki yake utakumbuka ilitutuma sisi wengine kazi, nayo bado ni duni. Lakini kwa uongozi wako sasa hivi tunapiga hatua na mimi nashukuru kwamba pengine hivi karibuni mambo yanaweza kuanza kuimarika kwa maana ya kuhudumia Bunge kwa namna mpya na kwa namna ya kuliimarisha ili liweze kuchangia katika kazi zake katika maendeleo ya Taifa letu bila udhaifu.

Mheshimiwa Spika, hili nimelisema kwa sababu bila kuimarisha vyombo hivi pamoja na chombo cha Mahakama ni kweli kabisa tunaweza kuwa tunasema tupo pamoja kumbe hatujajiimarisha kupitia nguzo zetu hizi tatu. Kwa sababu tuna mashindano hata ndani ya Afrika Mashariki au katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) basi ni lazima tuonyeshe kwamba tunapeana mawazo ya kushindana kikweli kweli ndani ya umoja huo. Kwa sababu ndani ya Afrika Mashariki si kwamba tunasubiri tu kwamba ahaa basi tutakuwa sawa, hapana. Tunashindana ndani ya Afrika

Mashariki na ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja ni lazima kuwe na ushindani katika elimu, viwanda, kilimo hata michezo kwani utakubaliana nami kuwa bado sisi Tanzania tuko duni.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niseme katika vyombo vyoma vya habari tumepiga hatua kubwa sana tangu Uhuru. Mwaka 1993 tukapata sera mpya na sasa hivi tunajaribu kusaidia kuimarisha vyombo vyetu.

Mimi napenda niseme tu kwamba kwa sera ambayo inaanaliwa ingekazania basi uhusiano kati ya Kurugenzi ya Mawasiliano ambayo imeanzishwa Ikulu halafu Ofisi ya Waziri Mkuu na vyombo vyake vya habari na Maeleo ikiwepo na vyombo binafsi. Tutatengenezaje hiyo sera ili iweze kuonyesha kwamba sasa tunaimarisha mambo ya mafunzo na taarifa pamoja na utafiti ili tuweze kupeleka habari nzuri za maendeleo ya kuwasaidia watu waweze kuhimili mambo ya utandawazi na kadhalika?

Niseme kwa kupendekeza kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, taarifa yake ya utekelezaji ingewasilishwa katika Mkutano wa Februari kila mwaka, tungepata nafasi nzuri sana katika Bunge hili Tukufu ya kujadili mambo ya msingi ambayo tunaweza kuwa tunakubaliana au hatukubaliani na hatimaye kufikia muafaka kwa sababu Taifa hili lazima twende pamoja mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama katika kipindi hiki basi napenda kuwapongeza wale wote walioingia katika Bunge hili kwa kuititia chaguzi ndogo, wale wa Chama cha Mapinduzi na Chama cha CUF tunawakaribisha, karibuni sana Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, ni kwamba mimi nadhani hotuba ya Waziri Mkuu imechanganua kila kitu kwa sababu hiyo ndiyo kazi yake na namshukuru Waziri Mkuu pamoja na Ofisi yake kwa hotuba hii iliyokuwa fasaha kabisa inayoeleza kila kitu. Lakini ningependa iende mbele zaidi ya hapo mimi nadhani Waziri Mkuu ni Waziri Mkubwa kama vile tukilinganisha katika shule kuna makaka na madada halafu kuna kaka mkubwa. Kwa hiyo, Waziri Mkuu ni Waziri mkubwa ambaye nafasi yake ni kana kwamba anawaangalia Mawaziri wengine wote shughuli zao na utendaji wao ukoje ingawa Mawaziri hao wanawajibika kwa Rais ambaye ndiye aliyewachagua. Lakini kiutendaji Waziri Mkuu nadhani ingelikuwa kwake kila kitu kinaoanishwa na kinaratibiwa kama *Coordinating Officer* wa shughuli zote za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hii basi mimi nampongeza sana Waziri Mkuu kwa kazi anayoifanya hapa Bungeni ya kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni. Akiona jibu lolote la Waziri ye yeyote aidha, Waziri kamili au Naibu Waziri, kidogo haliletu ule ufanisi basi Waziri Mkuu anaingilia ili kuweka sawa mambo kwa sababu ni kwamba ye ye ndiyo kazi yake.

Kwa hiyo, mimi ningetegemea kwamba Wizara zote ambazo zinafanya shughuli zake basi zipeleke habari zake katika Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa ni kiungo kwa Serikali nzima vinginevyo kutakuwa kuna utendaji ambao kila Wizara inatenda kivyake.

Mheshimiwa Spika, ningeweza kutoa mfano, Wizara ya Elimu na Utamaduni, inaweza kutenda kivyake kinyume ukilinganisha na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Kuna takwimu ambazo kusema kweli zinakosana kosana baina ya Wizara ya Elimu na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Pia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Ushirika na Masoko, Wizara ya Kilimo na Chakula inakuwa inahimiza mipango ya kilimo pamoja na umwagiliaji lakini baada ya hapo masoko hakuna.

Kwa mfano, sisi katika zao la korosho tumekuwa na tatizo hilo la masoko. Pia tulikuwa na mpango wa kusema kwamba tubangue korosho zetu kabla ya kuzisafirisha nje, lakini kutokana na viwanda vile vyta kizamani karibu viwanda kumi na moja vingine havikuweza hata kubangua kilo moja, kwa hiyo mpaka sasa hivi sehemu kubwa ya korosho inasafirishwa nje hivyo hivyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nasema kuna hali ya kutoweza kuwa na uwiano na kutokuwa na uratibu baina ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Ushirika na Masoko pia Polisi na Mahakama. Utaona Mahakama inataka kuhukumu lakini Polisi hajakamilisha uchunguzi, uchunguzi unakwenda miaka saba au nane maana yake nini? Sasa ni kwamba vitu hivi vingeonishwa pengine kungekuwa na utendaji bora tu mzuri na manung'unico mengi yangekuwa yameondoka kutokana na kuoanisha na kuratibu shughuli hizi.

Mheshimiwa Spika, mtu ambaye anaweza kufanya shughuli hii ni Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, mimi naomba Waziri Mkuu aende mbele zaidi kuliko hii kazi nzuri ambayo ameifanya na mimi nafahamu kwamba Waziri wetu Mkuu ni mtaalam mkuu wa kilimo.

Mimi nilipokuwa Kenya kule nafundisha Chuo Kikuu cha Nairobi nilikuwa na mwenzangu Profesa Kaniki, tulikuwa tunasifiwa sana Mheshimiwa Waziri Mkuu amepitia Egertone pale, ana sifa kemkem na tunazijua. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mwenzangu Profesa Kaniki, amekwenda kule Kusini na mimi niko hapa, tunajua Mheshimiwa Frederick Sumaye, amefanya kazi nzuri akiwa kule Egertone. Sasa atusaidie katika masuala ya kilimo. Yeye mwenyewe amekuwa Waziri wa Kilimo na Chakula hapa. Kwa hiyo, basi atusaidie akiwa Waziri Mkuu ili kilimo cha umwagiliaji kiwe kinakwenda mbele na kipambe moto. Tunashukuru hili nalo litakuwa limefanya kazi nzuri ikiwa Waziri Mkuu ataoanisha shughuli hizi ziwe katika hali ya mtiririko mzuri. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, halafu pengine kutakuwa na takwimu zisizokuwa za kuwiana, Wizara ya Viwanda kwa mfano na Wizara ya Kilimo inawezekana ikatoka takwimu au maelezo ambayo hayaendi pamoja. Kwa hiyo, mimi nataka nimalizie hili suala nisiende mbele zaidi ili niende katika suala lingine kwamba Waziri Mkuu tunaomba

iwe ni *One Stop Centre*. Mambo ya Wizara zote iwe mtu akitaka kujua takwimu zilizo sahihi aende katika Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwa ni kilimo, viwanda na biashara au afya na nini, akute habari sahihi na kila kitu katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu yeye ndiye *Head Prefect* au tuseme ndiyo mwoanishaji na mratibu wa shughuli zote za Serikali katika Tanzania. Mimi ningeomba suala hilo lishughulikiwe hivyo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo nataka kuzungumzia ni juu ya Ibara ile ya 76 ya hotuba ya Waziri Mkuu. Kusema kweli amezungumza kitu kilichokuwa sahihi kabisa. Amesema Tanzania ina raslimali nyingi lakini ni maskini. Kwa nini iendelee kubakia maskini, ameeleza vizuri sana na sitaki kurudia hayo aliyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ilivyo ni kwamba, mfano, mtu ana shamba la mahindi yeye mwenyewe anashindwa kuvuna anamwalika mtu au mtaalam wa kufanya kazi ya kuvuna. Nani anastahili awe na mahindi zaidi, mwenye shamba au mvunaji? (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, bila shaka yoyote ni mwenye shamba ndiye ambaye anastahili awe na mahindi zaidi. Kwa hiyo, suala la madini, *natural resources* zote tulizokwa nazo wale tunaowaita waje kutusaidia kwa sababu sisi wenyewe hatuwezi kuvuna wala kuchimba madini sisi ndiyo tunastahiki tuwe na sehemu kubwa ya mavuno kuliko yule anayevuna, kuliko yule aliyejukua kufanya utaalam pale.

Kwa hilo, mimi nataka kukumbusha msemo ule wa marehemu Mwalimu, kumbuka kuku wa Mwalimu yule alikuwa yuko pale anapekua pekua, ana jiwe la dhahabu au almasi, lakini yeye hajui kama lina thamani. Sasa amekuja mtu akaliona lile jiwe, yule kuku kalitagia pale au kaliatamia, akalichukua akaenda kulisafisha na kuliiza. Baada ya kuliiza hakukumbuka kumpa yule kuku hata senti moja au angalau punje moja tu ya mahindi ili aweze kufaidika kwa sababu yeye ndiye aliyechokora chokora dhahabu ikaonekana pale.

Mheshimiwa Spika, ndiyo tatizo hilo, kuku wa Mwalimu kusema kweli Mwalimu ingawa hakuweza kuleta makampuni makubwa hapa kuchimba dhahabu, almasi na nini alikuwa na maana hiyo. Jamani huyu mwenye dhahabu ni yule ambaye aliyekaa pale Mwadui kwa Mheshimiwa Leonard Derefa, hebu tuijilize anafaidika nini? Watu wanachukua tu yeye amekaa pale, hana chochote anachopata, siyo kuku wa Mwalimu huyu? Kuku wa Mwalimu tukumbuke ambapo leo tunasema tuko karne ya 21, sawasawa Mwalimu amefariki lakini je, huyu kuku wa Mwalimu tutamsaidia vipi ili nae apate chochote kutokana na kile ambacho alikipekua pekua au pale alipoatamia?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema umaskini wetu utaondoka ikiwa kweli sisi tutajua maana hiyo ya Mwalimu na kwamba yule anayekuja kutusaidia ili tuchimbue dhahabu au almasi kutoka ardhini basi n kwamba yeye ana sehemu tu ya ujuzi wake au ya uwezo wake kuliko sehemu ile kubwa ambayo sisi wenyewe itatusaidia kujenga nchi yetu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, mimi nashukuru sana utaratibu huu wa Wakuu wa Mikoa na Ma-RAS kuja hapa ili kusikia kwa sababu wao ndiyo tunaofanya nao kazi huko iwe Mikoani au Wilayani na kwamba mimi naupongeza utaratibu huu. Naomba uendelee

si kwa Ofisi ya Waziri Mkuu tu, ikiwezekana hata Bunge zima waje ili tuweze kushirikiana nao katika masuala hayo ili waweze kuelewa tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja hii, lakini Waziri Mkuu awe yeye ni kiungo kwa Wizara zote na Wizara zote katika utendaji ziwajibike kwake. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, mimi nataka nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwanza aliyetupa uwezo wa kutufikisha hapa kwenye Bunge lako Tukufu tukiwa na hali ya amani, utulivu na mshikamano. Kwa kweli ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuweza kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Waziri Mkuu iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nataka tena kuchukua nafasi hii kumpongeza mwenyewe Waziri Mkuu pamoja na Wizara yake yote na wataalam wake kwa kuichambua hotuba yake hii kwa kina na kugusa nyanja zote. Kwa maana hiyo hata kuchangia sana itakuwa vigumu isipokuwa labda kuongezea nyama tu kidogo sehemu zile zilizokuwa na kasoro ndogo ndogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuchangia naomba nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri Mkuu kidogo. Mwaka 2001 alifanya ziara ya kuja Pemba na kwa kweli alitembelea baadhi ya Majimbo. Baada ya hapo alituahidi kwamba kwa yale Majimbo ambayo alikuwa hakuwahi kuyatembelea likiwemo Jimbo langu moja la Kiwani alisema kwamba atafanya ziara tena kama hiyo kabla ya kumaliza kipindi hiki cha mwaka 2005. Lakini naona bado mpaka leo hii hajaweza kulitekeleza suala hilo. Ningewomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na kazi zake ngumu za Kitaifa alizonazo lakini atufikirie na sisi tunahitaji kwani wananchi wetu wanahitaji kumwona Waziri Mkuu na kumjua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka nimwombe tena Waziri Mkuu kwa vile yeye ni kiongozi wa juu kwenye Serikali yetu ya Muungano basi si vibaya na yeye kuwa na Ofisi yake pale Zanzibar ili wananchi wetu wakitaka kumwona wasipate usumbufu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo sasa nataka nianze kuchangia, katika ukurasa wa nne mpaka wa sita unaozungumzia hali ya kisiasa. Mimi nataka nikubaliane na Waziri Mkuu kwamba kwa kweli hali ya kisiasa katika nchi yetu imefikia mahali pazuri. Lakini kama mwenyewe alivyosema kwamba kuna baadhi ya dosari ndogo zetu sisi viongozi zinajitokeza pale.

Kwa hiyo, mimi namwomba Mheshimiwa Waziri azitupie macho sana kwa sababu kwa kweli hasa kwa kule kwetu Visiwani bado siasa sijui niseme kwa sisi viongozi au kwa nani lakini mimi nasema hasa ni sisi wenyewe viongozi. Kwa sababu

mimi naamini kwamba iliundwa Kamati ya Muafaka hapa na ilipoundwa walichaguliwa viongozi wa huku na huku, lakini cha kusikitisha hivi sasa mimi naona kwa mawazo yangu kwamba labda kuna baadhi ya Vyama waliona ule muafaka kwa kweli ni wa upande mmoja tu. Kwa sababu kuna baadhi ya Vyama wakiona kuna kitu kilichozungumzwa pengine kitakuwa na manufaa kwa upande wao zaidi basi kile hukivalia njuga zaidi wakisema hiki ni chetu.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu juzi tu tulipokuwa tukipitisha Bajeti ya Serikali hapa na wakati siku zote Serikali yetu ilikuwa ikitisemi kwamba tutakwenda na wakati, kila tutakapofikia mahali tukaona hapa sasa hali inatuendea vizuri tutakuwa tukipunguza kero ndogo ndogo za wananchi. Juzi tu tuliondoa kodi ya maendeleo lakini kuna baadhi ya Vyama walisema hii ni sera yetu, Chama cha Mapinduzi wanatuiga tu. Hivi kweli jamani siku zote hatusemi mambo kama hayo? Lakini leo imefika wenzetu wanatugeuzia kibao wanasema hii ni sera yao na sisi tunawaiga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka niwaombe viongozi wenzangu tujifunze. Sisi ni viongozi na tunachaguliwa na walio tuchagua ni wananchi, ni watu wenye akili na watu wenye ufahamu. Mimi ningeomba tu kwamba wananchi wetu tutakapowaelimisha, tuwaelimishe kwa ukweli na uwazi. Tusiwe na tabia za kuwalazimisha pengine tukawanyima hata demokrasia yao.

Mheshimiwa Spika, kweli nataka niungane na Waziri kwamba uchaguzi mdogo Pemba umepita kwa salama na utulivu. Lakini kuna mambo madogo madogo yalijitokeza. Kuna watu walinyimwa haki yao kwenye uchaguzi ule, kwa hiyo, walinyimwa demokrasia yao. Kuna watu waliokuwa wakiwaambia watu kwamba hakuna kwenda kupigia kura upande huu, pigieni upande huu la sivyo tutawaleta maruhani, tutawavisha na kuwalisha viapo. Hii si tabia nzuri na nafikiri hawa maruhani sijui walizuka kwa nini kama kweli tunasema tuna muafaka. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tu viongozi wenzangu tujiamini kwamba hivi sasa sisi ni viongozi na tunatarajiwa na wananchi wetu tuwapelekee yale ya ukweli yaliyokuwa na uwazi ndani yake.

Mheshimiwa Spika, nataka niondoke kwenye ukurasa wa nne niende kwenye ukurasa wa kumi na nne mpaka kumi na sita, unaozungumzia hali ya uchumi. Nataka niungane na Waziri Mkuu kwa kweli hali ya uchumi tuliyonayo kwa sasa katika nchi yetu kidogo nitasema ni nzuri na kidogo nitasema ni mbaya. Lakini nafurahishwa sana na hotuba hii ya Waziri Mkuu pale aliposema naomba ninukuu kidogo: “Katika kufanikisha azma hiyo juhudhi zitaelekezwa katika utoaji wa mikopo midogo ili kujenga na kuendeleza ujasirimali kwa mtu mmoja mmoja au vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali na utoaji huduma.”

Mheshimiwa Spika, hapa mimi napenda nimshukuru Waziri Mkuu tena nasema hili basi lianze mara moja kutekelezwa pindi ikionekana kuna uwezo wa kufanya hivi kwa sababu itatusaidia sana kwa wananchi wetu hasa tukitazama na hali yao ngumu ya

maisha waliyonayo. Kama tutaweza kuwapa mikopo hii midogo midogo ama kwa mtu mmoja mmoja ama kwa vikundi nya uzalishaji mali naamini kwamba zitawasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nataka nielekee ukurasa wa 42 pale alipozungumzia sekta ya huduma ya jamii. Mimi nataka nimshukuru Waziri Mkuu, kwa kutuona na sisi wanawake kwa kusema kwamba watapanuliwa Vyuo hivi nya Elimu ya Juu na wataweza kujiunga wanafunzi wa kike waliokuwa na uwezo huo.

Mimi nashukuru, kwa kweli tukilinganisha wanawake tulivyokuwa tuna kazi ngumu na majukumu mengi ambayo mengi hasa ukiffiria yanatuhusu sisi wanawake. Basi kwa vile ni mwanafunzi wa kike atakayekuwa na uwezo wa kuingia Chuo Kikuu aweze kupewa nafasi hiyo ya kuingia Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba hotuba hii ya Waziri Mkuu kwa kweli mwenyewe kaichambua kwenye nyanja zote na wala hakumnyima mtu yeoyote, kwa kweli tunaiona sisi wenye kwamba ni nzuri na inahitajika kuungwa mkono mia kwa mia lakini nataka nijielekeze tena kwenye ukurasa wa 55 amba unazungumzia sekta ya habari.

Mheshimiwa Spika, nakubali utolewe uhuru wa vyombo nya habari kama alivyosema, lakini vyombo hivi viwe na ukweli katika kuandika habari zao, ziwe za ukweli na siyo za kiuchochazi. Mimi nilikuwa nawaomba waandishi wa habari kwamba ni kweli katika kuandika habari zao basi wajitahidi kuziandika ziwe na ukweli na ziwe za wazi. Kwa sababu wakiandika mambo ya uchochazi au ya ngono kama alivyosema Waziri Mkuu basi wakumbuke kwamba hii ni taarifa wanaitangaza kwa dunia nzima, mimi nathubutu kusema hivyo.

Kwa hiyo, nawaomba Waandishi wa Habari wawe na uangalifu wakati wa kuandika habari zao. Pia nakubaliana na nataka niungane na Kamati ya Bunge kama walivyosema kuhusu taarifa za habari zile kwamba zipangiwe vipindi tofauti, zote zisiwekwe kwa wakati mmoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli yangu mimi yalikuwa machache sana, isipokuwa naomba tu Mheshimiwa Waziri Mkuu ayazingatie sana na alikubalie zaidi ombi letu la kututembelea kwenye Majimbo yetu kwa sababu wananchi wetu pia wana wivu au hamu hasa ya kuona viongozi wao wa Serikali ya Muungano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mimi nataka dakika zangu nizisamehe, niwaachie wenzangu. Kwa hiyo, naomba niishie hapo kwa kumalizia kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofî*)

MHE. SOPHIA M. SIMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hiyo. Kabla sijaanza ningependa kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Ningependa pia nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Dar es Salaam hususan wanawake na vijana kuipongeza Serikali kwa kuondoa kodi ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kodi ya maendeleo ilikuwa kero na hasa kwa akinamama, hasa pale wanaume wanapotoa visingizio vya kukimbia majumbani kwa kukimbia kodi hii. Kwa hiyo, kwetu sisi akinamama ni faraja pamoja na kwamba tulikuwa hatulipi kodi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumza machache kuhusu umaskini na kilimo. Tumeambiwa kwamba Pato la Taifa linakua kwa asilimia 6.2 lakini bado hali ya mwananchi wa Tanzania ni mbaya sana kiuchumi na hali duni sana. Sasa katika hotuba za Waziri Mkuu kila mwaka tunazungumzia kilimo. Bajeti iliyopita ya mwaka 2002 tulisema kilimo ni sekta kiongozi, lakini hatukukiona kikubwa kilichotokea. Nyuma yake tuliambiwa kilimo ni ajira mama, vijana wangu wa kule Dar es Salaam walihamasika kweli na hiyo ajira mama, badala yake ikawa tupu. Sasa tunazungumzia mageuzi ya kilimo.

Mimi ningeomba haya mageuzi yaende Mikoa yote pamoja na Mkoa wa Dar es Salaam. Kule tuna maeneo makubwa ya kuweza kulima. Hii mikakati ambayo inapangwa ambayo tumeambiwa kila Wilaya itashughulikia itushughulikie na sisi watu wa Dar es Salaam. Vijana wetu wa Dar es Salaam si kweli kama wanapenda kukaa vijiweni, hapana ila hawana la kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano mdogo tu, Mheshimiwa Charles Keenja, vijana wa Jimbo la Ubungo amewapatia mashamba katika Mkoa wa Morogoro, wamekwenda wamelima, amewapatia zana na vitu vingine. Sasa ule ni mfano mmojawapo mzuri lakini sisi tunafurahi kwamba vijana wa Dar es Salaam wameanza vizuri. Lakini tutashukuru kama utaratibu huo ukienda na kwenye Majimbo mengine pia ya Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wa Dar es Salaam wanaonekana wamekimbia jembe huko walikotoka. Sasa basi waje Dar es Salaam huku wakijua kwamba nako kuna jembe na sidhani kama watakimbia kama kutakuwa na matrekta, Mabwana Shamba wa kuwashauri na kama kutakuwa na mabwawa.

Naomba niliambie Bunge lako kuhusu vijana wetu jinsi wanavyolima. Kule Dar es Salaam tuna uwezo wa kulima mboga mboga kama sehemu zingine zikiwekwa mabwawa. Kwa mfano ukienda Gezaulole kule Kijiji cha Mbutu kuna maeneo mazuri mazuri ambayo unaweza ukaweka mabwawa ya maji, badala yale maji kuingia baharini yatengenezewe mabwawa vijana wa Mbutu, Gomvu, Kimbiji wasaidiwe ili walime mwani, wenzetu wa kule Pemba Mnazi wana maeneo mazuri kabisa ya kulima. Kwa hiyo, naomba wasaidiwe matrekta.

Mheshimiwa Spika, ukienda Kisarawe II, ndiyo utashangaa jinsi ardhi ilivyo nzuri, ila uwezo wa kulima na jembe jamani ni mgumu. Sasa wakati umefika wa

kuwasaidia wananchi hawa. Pia Kibada, Kimbiji, Somangila na Kisarawe II wanataka misaada hii, tuwasaidie haya mambo ya kulima, tusianzie huko Bara. Msifikiri kwamba wanaokaa Dar es Salaam ni watu wa Dar es Salaam peke yao, wapo wengi ambao wamestaafu, wakaondoka wakaenda kununua mashamba pembezoni mwa Dar es Salaam na ndiko makao yao na wangependa waendelee na kilimo hiki. Kwa hiyo, naomba na sisi tupate Mabwana Shamba wa kutuelimisha kuhusu mambo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Dar es Salaam wamesikia haya mambo, wengine wanasema sasa sisi mambo ya mama lishe na baba lishe tutaacha tuingie katika kufuga na kulima. Vipo vikundi maalum ambavyo vinashughulika na ufugaji na kulima mazao mbalimbali pamoja na uyoga. Naomba nao pia wasaidiwe.

Katika Mfuko huu tunaoambiwa wa Pembejeo kuna utaratibu hapa, kwanza huu Mfuko wa Pembejeo siyo mara ya kwanza, utakuta watu wanatumia Mfuko wa Pembejeo kwa kununua magari ya usafiri, mradi yupo katika kilimo tu anakwambia tunasafirisha mazao. Sasa hivi tushughulikie pembejeo kwa maana ya kuhamasisha kilimo na siyo watu wachache kujitajirisha kwa sababu kuna watu tayari wanajua watatajirika sana na Mfuko huu. Hilo ni kuhusu kilimo.

Mheshimiwa Spika, sasa nitakuwa sikuwatendea haki kabisa wananchi wa Dar es Salaam kama sikuongelea utaratibu wa viwanja 20,000. Kwanza, naipongeza sana Serikali kwa kupima vile viwanja 20,000 na ninaamini bado watapima viwanja vingine.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililojitokeza ni kutokushirikishwa kama wananchi wa Dar es Salaam wangeshirikishwa toka mwanzo kuhusu viwanja 20,000 na siyo dakika ya mwisho walivyotaka kuvigawa ndiyo wanawaita viongozi na kuwaambia tunataka kugawa viwanja hivi ili tu-*facilitate* ule utaratibu wa kugawa ndiyo tumeitwa na katika mazungumzo hayo wakawa *so defensive* Wizara haitaki kusikia la mtu.

Mheshimiwa Spika, wenzetu kule Zanzibar walivyokuwa wanagawa yale mashamba walifanya utaratibu mzuri kabisa, naambiwa ilikuwa katika kila viwanja vitatu vinavyogawiwa kiwanja kimoja alipewa mwenye shamba. Sisi huku linapimwa shamba Dare es Salaam mwenye shamba anaambiwa hutalipwa fidia, halafu ununue, mwingine anapata fidia 300,000 hakukuwa na mazao ya kudumu kama minazi au mikorosho, lakini anapewa 300,000 na akitaka kupewa kiwanja alipie 500,000 siyo kunyang'anyang'ana huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa nitahadharishe Bunge letu tuna matatizo tukiuliza maswali hapa tunajibiwa majibu ya haraka haraka tu hapa, wakati mwingine tunaambiwa wivu. Tulipouliza hili suala la viwanja, tukaambiwa aah hatujengi miji ya ukoo hapa. Kauli kama hizo ni ngumu. Hayati Mwalimu Julius Nyerere wakati watu walivyotaka kupima viwanja pale mbele ya jengo lake Msasani kulikuwa na kijiji pale wakataka kupima, marehemu Mwalimu Nyerere alisemaje, aah waacheni waswahili wangu, watahama wenyewe na sasa pale ukienda kuna majengo makubwa makubwa wameuza wenyewe wamehama.

Sasa mimi sikatai upimaji wa viwanja, vipimwe viwanja, Jiji letu lipendeze pamoja na kwamba nchi nyininge wanajenga majengo ya kwenda juu. Sisi uwezo wetu ni hivyo kidogo kidogo, lakini kunyang'anyana siyo haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, humu Bungeni tuliambiwa kwamba hakuna malalamiko. Mimi nataka nitoe mfano mmoja tu, naomba ninukuu mwananchi mmoja ameandika jinsi alivyodhulumiwa. Nanukuu: "Sisi tuliokuwa na viwanja Kisota tumekosa, wamepewa watu wenyewe uwezo kifedha wengi wao Waarabu na Wahindi, tulipokuwa tunaambiwa viwanja vitapimwa walisema tuandike idadi ya watoto na tutapewa fidia inayolingana na mazao yaliyomo na kubwa, wengi tulilipwa 300,000 na wengine chini ya hapo kwa sababu hakukuwa na mazao ya kudumu na si dhambi na mwengine alikuwa akilima bamia tu kila mwaka anauza na anapata kipato chake," anaendelea, "lakini wamepewa wengine, mimi na watoto wangu tumekosa, kwa nini Serikali ilitudanganya kuwa tutapewa kipaumbele wenyewe mashamba. Halafu bei ya chini ya kiwanja kidogo ni shilingi 500,000 nitapata wapi fedha hizo. Kwa kweli Serikali imetudanganya kutupora viwanja kisiasa. Hatukatai kuendeleza Mji, lakini wanyonge tufukuzwe kama makaburu walivyowapeleka wanyonge Soweto." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ardhi ni siasa kama tunalichukulia vibaya suala la ardhi na kuwasogeza sogeza watu bila utaratibu mzuri hii ina hatari yake. Mimi nisingependa kuendelea, lakini suala hili naamini watu wa Dar es Salaam wameridhika na *message* imefika tuwafikirie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia na linahusiana na hivyo hivyo viwanja. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba viwanja hivyo vina watu wenyewe uwezo fulani. Ni dhahiri tunatengeneza matabaka, basi vipimwe na viwanja vyaa watu wa chini, wale akina mama lishe, akina mama ntilie wangependa na wao wapate viwanja au wataendelea kujenga kwenye mabonde. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna bonde siku nyingi pale Msimbazi kwenye Kata yangu ya Upanga Magharibi, wameahidiwa miaka na miaka watapewa viwanja bado wako pale pale na wanaendelea kujenga, walipewa wakati huo wakiambiwa shamba lima hapa, sasa wamefanya makazi yao, wafikiriwe kupimiwa viwanja vyaa watu ambayo hawana kipato kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijagongewa kengele ya pili, ningependa kuzungumzia ujenzi wa barabara, naipongeza sana Serikali kwa kutengeneza barabara kuu zote zinazotoka Dar es Salaam na kwingine.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna tatizo moja kubwa, bomoa bomoa ni kweli tunakubali kuna bomoa bomoa ambazo zimefanywa kwenye sehemu ambazo hawakutakiwa wawe pale, wananchi wengine wako pale miaka 30 na kuendelea. Kwa mfano, watu wamebomolewa nyumba zao katika barabara ya Kilwa, kuanzia Kata ya Mtoni kwa Mheshimiwa Hadija Kusaga, tunakwenda Kata ya Mbagala Kuu, Rangi Tatu, Charamble, hawa wote wamebomolewa nyumba zao, kweli Serikali haiwezi kuwalipa fidia, lakini basi iwapatie viwanja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa tunazungumzia kupunguza umaskini, unapombomolea mtu nyumba, mtu aliye chini ndiyo umemmaliza kabisa anakuwa maskini kabisa. Basi hawa watu idadi yao inajulikana wapatiwe maeneo na hii inaenda mpaka Tuangoma, sielewi sehemu nyingine huko mbele nadhani itakuwa katika Jimbo la Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, kote wamebomolewa nyumba zao. Lakini kikubwa tunaomba wapatiwe viwanja ili waendeleze maisha yao na wajipunguzie umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia suala la Ukimwi na watoto. Kwa kweli sasa hivi tulikuwa tunaangalia wagonjwa wa Ukimwi, lakini watoto wa wagonjwa wa Ukimwi wanaishi katika hali mbaya sana. Unawakuta watoto wanalea wazazi wao ambao wanaumwa Ukimwi, watoto hao sasa hawaendi shule na wale watoto ambao wazazi wamefariki na wao pia wana hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, mimi naishauri Serikali ianzishe utaratibu wa kila kata kuwe na Afisa Ustawi wa Jamii. Kwa sababu wenzetu wa Ustawi wa Jamii wamesomea jinsi ya kushughulikia jamii ili kila familia ijue ina Afisa Ustawi wa Jamii ambaye atajua maeneo yale kuna nini kinachoendelea. Tumeongeza wigo wa Maofisa sasa hivi kuna Afisa Mtendaji wa Mtaa, sidhani kama itakuwa fedha nyingi kama tukiwa na Afisa wa Ustawi wa Jamii katika kila kata. Afisa Maendeleo hana taaluma ya ustawi wa jamii.

Kwa hiyo, tunawahitaji Maafisa wa Ustawi wa Jamii ili tuweze kupata idadi kamili ya hawa ambao wanahitaji msaada kutokana na kuumwa ugonjwa wa Ukimwi. Ilivyo sasa hivi sisi tunazungumzia mambo ya Ukimwi huko juu, lakini mitaani mwetu hata pale Dar es Salaam unaweza ukakuta watoto wanaishi maisha magumu kutokana na gonjwa hili la Ukimwi. Nadhani tunahitaji mipango ya kuona mbali zaidi kuhusu tutawafanyaje hili kundi la watoto yatima amba ni wengi kuliko tunavyotegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa kuungana mkono na Mheshimiwa Anatory Choya, aliyezungumzia kuhusu posho ya Madiwani ifikiriwe kuongezwa kwa sababu kazi wanayoifanya ni kubwa sana. Lakini kabla sijamaliza nitakuwa sikufanya vizuri kama sikumpungeza ndugu yetu Betty Mkwassa, kwa ushindi wake na pia ningependa nichukue nafasi hii niipongeze Timu yetu ya *Simba Sports Club*, watoto wa Msimbazi kwa ushindi mkubwa waliotuletea katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. EDWARD N. NDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili kwa mara ya kwanza nichangie katika hoja ndani ya Bunge lako Tukufu, nikianzia na hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo ilikuwa ni ya kina na naiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuititia Bunge lako nikishukuru Chama cha Mapinduzi kwa ngazi zote za uongozi,

Matawi, Mashina, Wilaya, Mkoa kwa maoni yao mazuri waliyonipatia ambayo yameifanya Kamati Kuu iweze kunitua kugombea Jimbo la Kigoma Kusini. Jimbo ambalo lilikuwa mikononi mwa Wapinzani na kwa ushirikiano mzuri tumeweza kulirudisha mikononi mwa CCM. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, nilipokanya katika viwanja vya Bunge nilisita kidogo kwa sababu nilijua tutapewa majina mbalimbali kama wanavyopewa wageni wanapoingia katika jamii mpya. Kwa mfano, katika Vyuo utaambiwa wewe ni *Form One* hata kama uko Chuo Kikuu, Jeshini utaambiwa wewe ni Kuruta na mahali popote ambapo unakuwa mgeni unapewa jina jipya. Hali hiyo ilikuwa tofauti kabisa katika eneo la Bunge na ndani ya Bunge kwa sababu Waheshimiwa Wabunge walitupokea kwa hamasa kubwa na kutupokea vizuri. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa mapokezi mazuri na utashi mwema ambaao wametupatia katika Bunge lako Tukufu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba niongelee mambo machache ambayo yapo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Moja ambalo ameliusia Mheshimiwa Waziri Mkuu ni suala la kilimo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipokuwa anawasilisha hotuba yake alisema katika hatua iliyopo ni lazima tuchukue hatua za kuinua sekta ya kilimo kwa kuandaa mpango wa kuendeleza sekta ya kilimo na mkakati wa maendeleo vijijini. Akasisitiza kwamba kinachotakiwa ni kutekeleza sera ya mkakati wa kilimo kwa kuikwamua sekta hii ambayo bado ilikuwa inaonekana ni dhaifu. Naye Mheshimiwa Waziri Mkuu akaungana na hoja hiyo akisema jitihada za pekee zielekezwe kuongeza tija katika kilimo na uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, hapa nadhani ni mahali pazuri pa kuanzia na mchango nilionao katika hili ni jinsi gani ambavyo tunapaswa kuongeza tija. Mara zote tumekuwa tukiangalia pembejeo na pembejeo ambayo tumekuwa tukisisitiza ni mbolea za viwandani.

Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aliainisha Mikoa minne (*The Big Four*) kwamba itapewa upendeleo maalum kwa ajili ya kupata ruzuku ya mbolea hii kwa sababu Mikoa hii haiwezi kuzalisha chochote bila mbolea. Wakati tukifanya hivyo hatuna budi tujiulize kwamba Mikoa hiyo ilifikia katika hali hii kutokana na nini? Hakuna ardhi ambayo haina mbolea kwa asili yake. Mikoa hiyo imefikia hali hiyo baada ya uharibifu uliotokea katika maeneo hayo ya wakulima wa tumbaku ambaao walikuwa wanatumia mbolea ya aina hiyo kwa kipindi kirefu na ardhi ikaharibika.

Mheshimiwa Spika, maeneo yale ambayo yana mbolea ya asili kwa mfano Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Morogoro haihitaji mbolea, tunachotakiwa kusema haihitaji mbolea ya viwandani hivi sasa kwa sababu bado Mikoa hiyo ina mbolea ya asili. Lakini je, ni kwa jinsi gani tutakavyowawezesha wakulima wetu waweze kuitumia hii mbolea ya asili na kuiendeleza. Mbolea ambazo tumeziweka pembeni na ambazo wakulima watapata maarifa na kuweza kuzimiliki ni mbolea zetu za asili, mbolea kama mboji. Mboji ni mbolea ambayo tumeiacha kwa kipindi kirefu na ambayo nadhani wakulima wanapaswa wasaidiwe katika kuitengeneza mbolea. Mkoani kwetu Kigoma najua kuna

aina nyingi za nyasi ambazo wataalam wakielekeza ni jinsi gani ziimarishwe zinaweza kuongeza tija katika kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, lakini mbolea nyingine ambayo nafikiri ina nafasi ya kuendelezwa ni mbolea ambayo inatokana na mifugo nayo ni samadi. Ukizingatia kwamba ipo Mikoa nchini mwetu ambayo ina mifugo mingi. Kwa wale wafugaji Waheshimiwa Wabunge wanajua kwamba ng'ombe mmoja tu samadi anayotoa kila siku siyo chini ya kilo 20, sawa na debe moja. Kwa kiasi hicho cha kilo 20 kwa siku ni sawasawa na tani 7 kwa mwaka. Kwa hiyo, Mkao ambao una ng'ombe 200,000 kwa mfano, unaweza kuzalisha tani 1,400 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nadhani kwa kutumia raslimali hii ya mifugo tunaweza tukaimarisha ushirikiano wa sekta hizi mbili, sekta ya Mifugo na sekta ya Kilimo. Kwa sababu Mikoa ile ambayo imebahatika kuwa na mifugo ina hiyo raslimali ambayo ni samadi, lakini haijatumika katika kuendeleza kilimo katika maeneo hayo na hili pia lingetusaidia kuondoa hali hiyo ya mgongano wa kijamii ambapo wafugaji wanalazimika kutembea na mifugo yao kutoka sehemu moja mpaka nyingine.

Mheshimiwa Spika, naamini wafugaji wakiona kwamba samadi yao inaweza kusababisha viwanda katika maeneo yao vya *ku-process* hiyo mbolea, ni dhahiri watathamini samadi hiyo na kwa hiyo, mifugo yao wataiweka katika maeneo ambayo ni rahisi kukusanya hiyo mbolea.

Kwa hiyo, nashauri kwa mtazamo huo tuhimize matumizi ya raslimali hiyo ambayo ni mbolea kutopteka na mifugo kwa ile Mikoa ambayo ina mifugo mingi kiasi cha kuwa na ziada kubwa ya mbolea ambayo inaweza kuuzwa Mikoa mingine kama Kigoma, Lindi, Mtwara na kwingineko ambako hakuna mifugo.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu unatufanya tuwe tayari na chanzo chetu cha mbolea nchini na kuweza kuuziana kama biashara ambayo itakuwa inakuza kilimo. Lakini pia hii itakuwa inachangia katika kuimarisha viwanda kwa sababu mbolea ya kiasi hicho ambacho nimesema kwa ng'ombe 200,000 yaani tani 1,400 kwa mwaka, basi utahitaji watumishi wengi katika kuiandaa katika vijijini.

Kwa hiyo, hapo tena tutakuwa tunazungumzia ongezeko la ajira kwa watakaokuwa wanahusika katika *ku-process* hiyo mbolea ili iweze kutumika na pia kuuzwa katika Mikoa mingine ambayo haina raslimali ya namna hiyo. Lakini wakati huo tutakuwa tunaimarisha viwanda ambavyo vitazalisha magunia kwa ajili ya kupakia hiyo mbolea na tutakuwa pia tunaongeza uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Serikali kwa hatua ilizozichukua kuimarisha ulinzi katika mwambao wa Ziwa Tanganyika. Maeneo yale ulinzi umeimariswa na Jeshi la Polisi pamoa na Jeshi la Ulinzi na niishukuru Serikali pia kwa hatua hiyo kwa sababu sasa hivi hali inaanza kuimarika. Ni imani yangu baadhi ya viongozi ambao tumewapata hivi sasa, kama Mkuu wa Mkao ambaye katika muda mfupi

ameweza kutembelea maeneo yote hayo na kwa nafasi yake kama Mwanajeshi atasaidia katika kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nadhani ni vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu akiangalie ni katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa miundo mbinu. Mkoaa wetu wa Kigoma na hususan Jimbo langu la Kigoma Kusini lina ukubwa ambao lazima miundombinu iimarishwe kwani kutoka Kigoma mpaka mpakani mwa Jimbo langu Mashariki linapopakana na Urambo ni kiasi cha kilomita 200 na Mkoaa wa Kigoma kwa hali ya hewa iliyanayo ya mvua nyingi karibu miezi minne kila mwaka maeneo yale yanakuwa hayapitiki kwa sababu ya mvua na mafuriko yanayotokea katika Bonde la Mto Malagarasi. Kwa hiyo, usimamizi unakuwa mgumu katika mazingira hayo. Mtendaji hata Mbunge kama anataka kwenda katika maeneo hayo inabidi atumie muda mrefu kupitia Kasulu, Kibondo, Kahama mpaka Tabora na baadaye Nguruka ni kiasi cha kilomita zisizopungua 900 na hii ni kwa sababu hakuna daraja katika mto Malagarasi. Kwa hiyo, hili ni ombi la dhati kabisa kwamba uimarishaji wa miundombinu hasa barabara ni muhimu sana katika ukanda huo na kwa hiyo daraja la Mto Malagarasi na barabara ya kutuunganisha maeneo hayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la miundombinu ni kuelekea kusini mwa Jimbo la Kigoma Kusini ambapo Jimbo hilo linatunganisha na majirani zetu wa Mkoaa wa Rukwa. Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, alipokuwa anachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, jana alielezea manufaa ya kiuchumi yaliyo katika eneo hilo na akataja mpunga, lakini siyo mpunga tu katika eneo hilo. Eneo hilo lina fursa ya kuzalisha mbaa kwa wingi, samaki na dagaa wanapatikana kwa wingi, pia kuna madini katika maeneo hayo. Lakini tusisahau pia kwamba kuna mbuga maarufu ya wanyama ya Mahale. Umbali wa kutoka Kigoma mpaka Mahale ni kilomita 200. Eneo hili halifikiki kwa urahisi, kwa hiyo, tunakosa fursa nzuri ya utalii katika maeneo hayo. Kwa sababu siyo watalii wote wanaweza kukodisha ndege na kwenda mpaka katika eneo hilo. Ni vigumu kwa watalii kwenda maeneo hayo kutoka Kigoma kwa kutumia boti, ambako si chini ya masaa 10 hadi 12 kufika katika maeneo hayo. Lakini kama barabara ambayo ni muhimu kuwepo itajengwa basi itakuwa ni fursa nzuri sana kuweza kuinua uchumi wa eneo hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nadhani kitu kingine ambacho kitapaswa kitazamwe katika usimamizi na utekelezaji ni eneo la maji. Maeneo hayo yana matatizo ya maji katika baadhi ya vijiji. Sasa hilo ni vizuri likaangaliwa na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. PARSEKO V. KONE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naomba kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kwenye chaguzi ndogo hasa Waheshimiwa Wabunge wa CCM nawapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niseme mapema naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usimamizi wake wa shughuli za Serikali na kwa kweli wananchi wameanza kuona utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu ya CCM. Lakini niwapongeze Askari wake wa miavuli Mheshimiwa Edward Lowassa na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa kutembelea Wilaya ya Simanjiro na kuona matunda ya Waheshimiwa Mawaziri kufika huko kwetu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la uhaba wa chakula. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alieleza kwamba kuna uhaba wa chakula nchi nzima au maeneo mengi katika nchi yetu. Wilaya ya Simanjiro ni moja kati ya maeneo yenye uhaba wa chakula. Nimetembelea kila kijiji na vijiji vyote havina chakula, kwa maana ya chakula cha nafaka. Kwa hiyo tuna upungufu wa mahindi tani 7,400. Kuna wananchi wanaoweza kununua na kuna wananchi ambao hawatakuwa na uwezo wa kununua.

Sasa naishauri Serikali kwa hawa wenye uwezo wa kununua ni vizuri pia wangepatiwa na Serikali chakula cha kununua kwa bei nafuu. Lakini kila wakati tumehimiza kilimo cha umwagiliaji nina hakika Serikali ingeyaendeleza maeneo ya umwagiliaji katika Wilaya ya Simanjiro ambayo ni maeneo ya Kambi ya Chokaa, Kiruani, Lemukuna, Ngage, Loiborsoit B, Ruvuremiti, Ngage na Gunge tungepunguza uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, afike katika maeneo hayo ili tuone namna ya kupunguza hali hii ya upungufu wa chakula. Kwa kweli kwa Wilaya ya Simanjiro asili yake na ardhi yake siyo ya kilimo ni ya ufugaji zaidi, na hasa kwa sababu pia tunategemea mvua. Kwa hiyo, maeneo hayo yakiendelezwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji tunaweza kumwagilia hekta 5,222 ambayo itasaidia sana kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, la pili, napenda kuishukuru na kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tatu, kwa kurudia historia ya Serikali ya Awamu ya Kwanza kufuta kodi ya maendeleo kwa wananchi. Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro naishukuru Serikali na naishukuru Serikali kwa kutamka kwamba itapunguza na kufuta sasa kodi zenye kero kwa wananchi, nyingine zimeishafutwa. Lakini naomba niieleze Serikali kwamba kuna kodi moja ambayo ni kero sana kwa wananchi ambayo Serikali haijatamka kuifuta nayo ni kodi ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kodi ya mifugo ni kero sana kwa wafugaji na sijui kwa nini Serikali inatoza mifugo kodi. Sioni sababu, kwa sababu kwa mfugaji ndama ni sawa na mahindi yakiwa shambani, ng'ombe aliyekomaa ni sawa na mahindi yakiwa kwenye ghal. Sasa wafugaji wanauliza, hivi Serikali ya Chama cha Mapinduzi huwa inatoza kodi mahindi yakiwa shambani? Jibu ni hapana. Kama haitozi kodi kwenye mahindi kwa nini itoze kodi kwenye ndama maana yake wanahesabiwa mpaka ndama waliozaliwa siku hiyo wanatozwa kodi. (*Makofsi*)

Wafugaji wanauliza hivi Serikali inatoza kodi mahindi yakiwa kwenye ghalia la mkulima? Jibu ni hapana. Kwa nini umtoze mfugaji kodi ya ng'ombe wakiwa kwenye zizi lake. Hayo ni maswali ambayo wafugaji wanatarajiwa wajibewe na Serikali yao.

Tuna hakika mahindi yakifishwa sokoni inatozwa *crop cess* kwa sababu limeshakuwa zao la biashara. Nao wanakubali, ng'ombe wakifika mnadani wanatozwa kodi tena wanatozwa mara mbili kwa muuzaji na mnunuzi hapo ni sawa. Lakini kwa nini watozwe wakiwa kwenye ghalia. Hapo wafugaji wanasema kwamba kuna *double standard* katika kuwashudumia wananchi wa Tanzania.

Kwa hiyo, nitaiomba Serikali ione hilo na itamke baadaye kwamba hakuna kutoza mifugo kodi ila pale wanapouzwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatu nzungumzie suala la Mikoa. Tunapitisha Bajeti ya uendeshaji wa mikoa. Lakini kabla ya kurekebisha sheria ya Serikali ya Mitaa, Mkuu wa Mkoa alikuwa muhimili wa Halmashauri zilizopo katika mkoa wake. Sasa sio. Alikuwa na Wakuu wa Idara kwa kila Idara, sasa hanao hao anaye Sektarieti. Alikuwa na vikao vyenye kutoa maamuzi kama *RDC*, sasa ana vikao vya ushauri tu *RCC* na *TANROAD*. Alikuwa anapokea fedha za maendeleo na *OC* kwa Wilaya zote na Halmashauri zilizoko kwenye eneo lake. Sasa tunasema fedha hizo zitakuwa zinakwenda moja kwa moja kwenye Halmashauri.

Kwa hiyo, nafasi ya mkoa sasa ni uratibu. Lakini nafasi hii ya uratibu ni ghali sana. Kwa kweli uzoefu inatukaza nafasi hiyo na kudai kwamba nafasi hiyo iwepo. Lakini kwa uhakika nafasi hiyo sasa hivi haina nafasi haistahili kuwepo. Kwa hiyo, japo sieleweki wala sijui nitalieleza hili vipi mimi nashauri nafasi za mkoa zifutwe. Kwa sababu tumewanyang'anya kazi za kufanya. Kwa sababu ya uzoefu tunaogopa kutamka hilo au hatuwezi kulifanya hilo, basi mikoa tuipunguze. (*Makofii*)

Kenya ina Mikoa minane lakini inaendeshwa tu vizuri. Hivi sisi kila mikoa mitatu itarudi kuwa mkoa mmoja tutakuwa na mikoa saba ya kuratibu. Halmashauri na Wilaya zilizomo humo, kuna makosa gami. Hiso fedha sasa hivi Bara tuna mikoa 21 ukifanya mikoa 7 kwa maana mikoa mitatu kuwa mkoa mmoja hiso fedha za mikoa 14 zitarudi kuendeleza wananchi huko Wilayani. Kwa hivyo kama tunaona mazoea hayaelekei kuturuhusu kufuta ngazi za mkoa lakini kwa vitendo tumefuta kwa kunyofoa majukumu yao na tukawabakiza hawana kazi basi tupunguze eneo hilo. Kwa hili Wakuu wa Mikoa wasije wakanielewa vibaya najua ni wachapa kazi wazuri, lakini basi kama ninayosema sio kweli tumewabakiza wafanye nini. La sivyo tuwarudishie madaraka waliyokuwa nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la nne ni suala la Wizara ya Ushirika na Masoko. Hii Wizara kwa hali hii ya siasa ya kiuchumi ni Wizara muhimu sana. Ni Wizara ambayo ndiyo inayoandaa masoko kuwajulisha wananchi na kuhakikisha wafanyabiashara wanafika kwenye masoko haya au kuwasiliana na masoko hayo.

Lakini sina hakika kama Wizara hiyo inafanya kazi yake vizuri. Mimi sio mtathmini lakini kwa maoni yangu naona haifanyi kazi yake ipasavyo. Nikitoa tu mifano michache wafugaji wanahangaika kutafuta masoko ya kuuzia mifugo na mazao yatokanayo na mifugo hiyo, hawajui wapate wapi. Wakulima ukiondoa mazao ya asili *traditional crops* kahawa na kadhalika tunayouza nchi za nje kwa mazao mengine hawajui wapate wapi masoko na kuna Wizara ya Masoko.

Mheshimiwa Spika, Nakumbuka kipindi kilichopita Mheshimiwa Ndaboine alikuwa anatafuta soko la asali ili vikundi vya akinamama huko Kigoma waungane pamoa wauze hiyo asali. Wizara ilishindwa kuwatafutia soko mpaka mwenyewe amejitahidi kulipata soko Afrika ya Kusini. Niliwahi kufika Uingereza, Balozi wetu ametuambia huku kuna soko kubwa la asali. Lakini Wizara ipo naishauri Wizara hiyo ianzishe jarida litakalotoka kila mwezi kuonyesha masoko yanapatikana wapi kwa kila zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sio vizuri Mbunge mzoefu kupigiwa kengele ya pili, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu asilimia mia kwa mia, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia maoni kiasi kuhusu Bajeti hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninadhani nchi hii tunaiua wenyewe. Tunaiua wenyewe kwa sababu tumeacha utekelezaji tumeja maneno matupu na Serikali haitekelezi wajibu wake. Serikali katika dunia hii ni ya pili kufuatana na nguvu za Mungu. Mungu anaua na Serikali inaua na huna mahali pa kuidai. Sasa Serikali ikianza kuwa nyoronyoro haisimamii mambo haina meno hakuna atakayeilogopa wala kuijali, ndiyo matokeo tuliyonayo hayo. Ndiyo maana miradi tunapanga mipango na fedha zinatoka zinachezewa zinaliwa hakuna wa kusema tunarudi hapa hadithi ile ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali yetu ni kwamba uchumi wetu hauwezi hata kidogo kubadilika kwa sababu hakuna anayewajibika. Wasimamizi wenyewe wa Serikali ni waoga kuwakabili watu wasiotekeleza kufanikisha shughuli tulizopanga, ni waoga. Kwa namna hii hakuna mwenye uwezo wa kusukuma chukua ngazi zote hakuna anayeweza kusukuma. Sasa wanabaki kutafuta njia namna ya kumdanganya Waziri Mkuu ili mambo ayaone ni sawa. Sasa kwa kuwa nchi hii ni kubwa hawezi kutembelea kila mahali mengine anayakubali, lakini hayako. (*Makofi*)

Leo tumeamua kuwa madawati kila shule yatengenezwe, taarifa wanasema tayari asilimia 60 au 70 yako wapi sasa madawati shulenii, hakuna. Hakuna mtekelezaji ni maneno ya kumreomba Waziri Mkuu kumbabaisha na kumweka kuwa aelewamambo yanakwenda, hakuna wenye meno kule unabaki Mkuu unatoa maana watu hawajui maana ya Serikali, sasa hata Serikali haizingatii ukweli. Hilo ni tatizo moja ambalo kwa kweli ni gumu sana.

Tumesema vidhibiti mwendo sasa leo magari ndiyo yanakwenda kuliko vidhibiti mwendo vilivyosemwa. Watu wanayaona haya hakuna wa kuchukua hatua wala wa

kushangaa sote tunatazama tu hivi hivi. Na ajali zinazidi hakuna wa kukemea wala wa kuchukua hatua. Sasa imekuwa Serikali na mtu wa kawaida ni kitu sawa sawa tu.

Serikali lazima ionyeshe makucha yake na uwezo wake iogopwe, watu waitii waisikilize ndipo watekeleze kwa woga. Serikali isiyojenga woga kwa watu wakaitambua na wakaogopa wakatekeleza ni Serikali kwa kweli bandia haitaleta maendeleo dunia hii. Haiwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii tunasema kuhamia Makao Makuu Dodoma. Dodoma yenye we ndiyo hii hakuna miundombinu wala barabara viwanja watu wanalipia porini. Watu wanaona ni sawa sawa tu. Hivi maana yake nini, Serikali iko wapi? Watu wanalipa kodi lakini hakuna cha barabara hata mifereji ya kuonyesha nyumba zimepimwa huku, hakuna lakini wanatozwa kodi. Hivi Serikali iko hapa. Leo tunaongeza *CDA*, Manispaa zote zipo hapa zinafanya kazi gani na wanapata fedha tunatenga fedha, fedha tumeamua kutoa zawadi kula tu au zilete maendeleo zionyeshe mipango inayofahamika ili na mwaka kesho tujue tunafanya nini. Hasa kama ndiyo lugha tunazunguka hivi hakuna tutakachokiona kwa kweli kitakachotokea.

Tumesema Ofisi za Wabunge leo tunaambiwa zinatekelezwa, ziko wapi. Hivi tumeamua kudanganyana hapa. Kama tunadanganyana sisi je, wasiokuweko hapa. Hivi kama fedha zinapelekwa huko hawa wanaokula fedha hizo hawatekelezi Serikali ina meno haina meno, imechukua hatua gani. Watu wanakula tu fedha. Sasa na hawa Mawaziri na mipango yao ya maendeleo hawatekelezi hivi tunawafanyia nini. Hatuna sababu ya kuogopa watu. Tuwaambie watu watende vitu vionekane na ndiyo msingi wa mabadiliko na maendeleo yetu, sio kukaa hivi tunaangaliana machoni kubabaishana tu hapana, haitusaidii kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Waziri Mkuu umeeleza, maeleo yako mimi ninakubali kabisa. Lakini sasa yanakwenda mahali yasioweza kuleta matokeo. Umeeleza juu ya matatizo ya Shule za Sekondari wananchi wanakubali wanajenga Shule za Sekondari, lakini hakuna walimu. Walimu wa Sekondari hakuna hivi tunasema wajenge, wajenge ili iwe nini. Hivi kweli Serikali inashindwa kukaa na kufikiria kama ni kuwaongeza kama tatizo la *TRA* tulikaa tukasema waongezwe kipato na limefanikiwa.

Kwa nini tusifanye walimu angalau wapate nyongeza ya kuwasukuma waweze kujiunga na walimu wa kutosha. Leo unataka mwalimu awe na kiwango cha chini aingie katika ualimu tutampata wapi mwalimu wa namna hiyo. Serikali iangalie na hili ni suala la kukaa na kufikiria kwamba sasa walimu wale wa Sekondari waingie waanzie hata shilingi 150,000/=. Hivi nalo hili ni tatizo?

Leo hii walimu hakuna shule zinajengwa. Mimi kule kwangu shule tatu zinajengwa walimu sasa hakuna hata zilizopo hazina walimu. Tunasema eti tuongeze kujenga, tutajilettea matatizo. Maana mafanikio hayapo tufanye vitu vinavyoleta matokeo na mafanikio ambayo yatakuwa ni kumbukumbu kwa maisha yetu na utendaji wetu wa kazi na hiyo ndiyo sifa ambayo tunaihitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunasemea suala la leo hii ni siku ya kumbukumbu ya waliokufa na treni hapa. Je, reli yenye hii mazungumzo baada ya habari wanaeleza je, mmeefanya mabadiliko gani, tumefanya nini ili kulinda usalama na kuleta sawa sawa. Bajeti haina hata senti ya kusaidia reli hii ipate kurekebisha. Leo tunakwenda kumbukumbu hizo tukakumbuke ili yaje yatokee mengine tuje tukumbuke tena. Serikali iangalie hii ni aibu katika dunia watu wamekufa leo tuweke kumbukumbu hatuna hata senti ya kuongeza kurekebisha hayo. Iangalie ikatoe popote pale yale mataruma pale watu wanatembea kwa bahati tu. Kwa kweli mtu kuingia kusafiri kwa reli kwa hali inayoonekana hiyo ni kujikusuru maisha yako mwenyewe. (*Makofi*)

Kwa kweli suala kama hili ni lazima tuwe macho. Turekebishe pale likitokea lingine liwe ni bahati mbaya kweli lakini kila siku bahati mbaya, bahati mbaya mpaka lini. Sasa watu kama wale wa Dar es Salaam wanaambiwa ondokeni kwenye mito hawataki wanarudi, hivi wakija kuzolewa na maji tuanze kusema maafa tena. Serikali si ya kubembeleza hivyo ikishaona hatari ni kuamua asiyetaka asombwe aswagwe aende. Hilo ndilo tunaloagiza Serikali na tulione Waziri Mkuu unalismamia kwa dhati na nguvu zote ndiyo tutaa mini hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tunazungumzia juu ya pembejeo tusipoangalia pembejeo hizi zitakuja kufika mahindi yameshaanza kutoa mbelewere. Sasa lazima watu wafanye kazi wawahi kupeleka mbolea katika vijiji vinavyotakiwa na wawe watu waaminifu zile pembejeo zilizowekwa mwaka juzi watu wamegawana kwa mbinu tu. Sasa wasipokuwa waaminifu nani awadhibiti hawa. Serikali sio kuachia mtu afanye anavyotaka. Serikali mtu yoyote anayefanya kinyume cha malengo ya Serikali huyo ni Mpinzani, huyo ndiye anayevuruga siasa na lengo la nchi linakotaka kwenda. Achukuliwe hatua za kumtosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tuna hizi Halmashauri hazitadumu zinakuja kufutwa tu maana zitafilisika. Watu wamegeuza Halmashauri ni mahali pa kugawana fedha. Taarifa hii ya ukaguzi wa Kamati ya Bunge inaonyesha wazi, sasa tunafanya nini. Makatibu Wakuu wapo, *Ma-Paymaster General* wapo, Fedha watu wanakula bila utaratibu tunatazama eti tunasema nchi hii ni nzuri, nzuri wapi. Tunajichimbia shimo wenyewe na kuombaomba kutegemea misaada ni kujifedhehesha na aibu, tusimamie tulichonacho ili kionyeshe mafanikio na kituletee heshima watu watupe kwa heshima tuliyonayo. Lazima tukubali hivi Mkuu wa Mkoa na Mkoo wa Wilaya ndio wahimili wa Halmashauri, hivi mpaka mambo yaharibike kule wako wapi? Sasa waambiwe kama hawapo tusiwaweke. Ya nini kuaweka. Na tabia hii ya kuunda vikundi vingi, Tume na Idara nyingi fedha nyingi zinatumika hakuna tunalolipata ni kufuja fedha zetu na nguvu yetu kudhoofisha maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba hili Mheshimiwa Waziri Mkuu ubadilike uwe sasa ni fimbo ya moto uchome watu wasikuchezee. Uchome kabisa watu waache uzembe Serikali itakwenda na kazi zitakwenda na mafanikio yataonekana. Lakini hivi tulivyo hakuna kitakachowezekana.

Naomba kuanzia leo kwa kweli Waziri Mkuu ubadilike na uanze kutoka na watu waelewe maana ya Waziri Mkuu kuwa ni msimamizi wa utekelezaji na hakuna mtu kukuchezza, akikukuchezza anachezea nchi. Wewe uko kwa niaba ya nchi hii anayekuchezza anadhalilisha nchi. Tusiwape watu nafasi kuchezza Serikali na kuchezza nchi. Bunge pia litakuwa na nguvu kama wewe kiongozi unasimamia kweli na sisi tutakuunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nakushukuru tena nilitaka tu niseme haya maana yananiuma sana kila ninapofikiria. Yananiuma kweli. Sasa inakuwa hata ushirika tunasema ushirika uko wapi mmeuona ushirika uliko huko. Majitu yanadhulumu watu tu, hakuna ushirika wowote ni dhuluma inaendelea nchi hii. Tuwe wakweli tuangalie tusiruhusu dhuluma, tusifikiri ushirika kwa maneno ndio unaweza kufanikisha hii tunajenga balaa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu. Naanza kusema kwamba hoja hii naiunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kuipongeza Serikali ya Rais Mkapa, Waziri Mkuu wake pamoja na Mawaziri pamoja na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na wote ambao wanafanya kazi katika Serikali ili tuweze kuwa na amani. Ni kweli mapungufu tunayo lakini mimi mara nyingi nasema kwamba Tanzania nafikiri tuna Serikali mahiri sana na hili ukitaka kulijua unalinganisha na Serikali aidha za majirani zetu sasa utaona kwa kweli pamoja na kwamba tunafumuka sana hapa lakini lazima watendaji wa Serikali mjue kwamba mnafanya kazi nzuri hasa.

Kwa hiyo, mimi ningependa nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Tanzania. Mnaelewa kabisa kwamba Serikali ya Tanzania ndiyo imeleta uhuru wa nchi zote Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kwa kutumia Serikali iliyopo hii ya Tanzania na Chama cha Mapinduzi. Ningependa niseme kwamba tuna Serikali mahiri “*We have the best government in Africa, we have the best government in the World*”. Kabisa. Tunayo mapungufu na kwa bahati nzuri tunapokuja hapa tunasemezana na tunawekeana na mikakati ya namna ya kuyatatua au namna ya *ku-iron out*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa niongelee suala la njaa. Suala la tusilifanyie mchezo. Ningependa niwatahadharishe kwamba suala la njaa tusilifanyie mchezo. Mimi katika jimbo langu sijui sehemu zingine kata zote hakuna chakula. Mimi nina kata za aina mbili, kuna kata zile *pre-urban* ambazo ni za vijijini halafu na kata za mjini.

Katika Kata ya Kizumbi hakuna chakula, watu hawakupata chakula, Kolandoto hakuna, Mwamalili hawana chakula, Chibe hakuna chakula, Ibadakuli hakuna chakula, Mwawaza hakuna chakula na sisi watu wa mjini huwa tuna vishamba vidogo vidogo katika *pre-urban area*. Kata za mjini ni Ngokolo, Ndala, Kambarage, Mjini, Chamaguha,

Kitangiri chakula hakiko. Bahati nzuri nilipotoka Shinyanga nilikwenda Moshi nikalala Arusha halafu kesho yake nikalala Moshi, halafu kesho yake nikapanda basi kuja Dar es Salaam sikuona chakula kule. (*Makofî/Kicheko*)

Mimi nafikiri kwamba badala yake tungelilia badala ya kucheka. Chakula hakipo na Serikali ina-*appreciate* kabisa kwamba chakula hakipo, lakini wamefanya nini. Mimi ningelipenda nishauri kwamba unajua njaa sio kitu cha mchezo. Ukiwa Professa ukilala na njaa siku mbili au tatu U-professa haupo.

Ukiwa Daktari ukilala na njaa siku tatu hakuna Udaktari. Nilikuwa naomba kabisa kwamba Serikali iweke mikakati kuhusu njaa. Vile vile ningependa msome kuhusu historia ya njaa. Kuna vitabu vya *encyclopaedia, The World Book, In China* mwaka 1944 walikufa watu milioni 9, India mwaka huo huo walikufa watu milioni 5. Ebu jiulize kama sisi tunafanya mchezo wakifa watu milioni 9 hapa tunakuja kufanya kazi gani. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema kabisa kwamba kama itabidi hata baadhi ya *project* ambazo tumezifanya kuziwekea hata *break kidogo* ili kusudi tupate chakula watu wetu wapone, vinginevyo kwa kweli tusifanye mchezo na suala la njaa. Mimi bahati nzuri tulikuwa tuko Mwanza nikamwambia Waziri wa Kilimo kwamba tunavyoonekana sasa hivi mvua imeshindikana, nikamshauri kwamba ile barabara ya kutoka Shinyanga, Tabora, Ipole, Inyonga, Mpanda kwa kuwa kule chakula kipo ili kusudi barabara ile itengenezwe kwa utaratibu wa kijeshi. Wamerikani nafikiri mwaka 1945 walitishiwa na Japan kwamba watashambuliwa kupitia Alaska, walijenga barabara kwa miezi 18 kilomita karibu 2,500 za lami.

Nilimwambia na bahati nzuri Mheshimiwa Keenja alimwandikia barua Waziri wa Ujenzi kwamba hiyo barabara itengenezwe. Lakini *as if this is not enough* kama hii haitoshi utakuta chakula kilichopo Rukwa sasa hivi tunawauzia watu wa Zaire, Zambia na Malawi. Eti tunapata shilingi 22,000 kwa gunia ndiyo tunaona hiyo ni hekima. Tunaona hiyo ni hekima sisi watu wetu wakifa je, kweli hivi tunaona fedha ndiyo ina thamani kuliko maisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nasema kabisa kwamba suala la njaa tusilifanyie mchezo. Niliwahi kumwambia Waziri wa Kilimo kwamba tulianza vizuri tukawa tunajenga *silos* za kuwekea mazao. Ukisoma kwenye Biblia nafikiri Farao ile ndoto ya Farao iliyotatuliwa na Joseph. Ng'ombe saba nene, ng'ombe saba nyembamba na masuke saba. Lazima tujenge utaratibu katika Taifa hili wa kujiwekea akiba.

Utaratibu tunao hata kama kuna *bumper crop* chakula tunachokiweka sasa hivi *actually* sio utaratibu mzuri kwa sababu inavyoonekana sasa hata wadudu baada ya kuja wadudu wengi hawa sasa hivi kutunza chakula ni gharama kubwa kweli. *Silos* za Iringa hazifanyi kazi, *silos* za Arusha hazifanyi kazi, sijui za Dar es Salaam zikoje. Lakini ilitakiwa zile *Big Four* kila mahali kuwe na *silos*. Nimewahi kuuliza swalii la nyongeza hapa. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alisema hakuna sababu tutakuja kuisha kabisa halafu Taifa la Tanzania litakuwa la kaburi. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu barabara yetu ya kutoka Shinyanga - *Mwanza border* - Tinde - Nzega - Isaka. Mwaka 1999 tuliambiwa Serikali imepata fedha kutoka *European Union (EU) Euro bilioni 57* na wakatangaza *tender* mwaka 2001 ama 2002 na *tender* ile ikafunguliwa na waka-*award* watu, lakini nimeshangaa sana, nimetafuta katika vitabu vyote vya Bajeti barabara hiyo haimo! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, *this is a political crime*, yaani ni dhambi ambayo sijawahi kuiona! Ni kwa nini watu wa Shinyanga tumekatwa? Yaani barabara imekuja kuanzia Nzega! Wananchi wamewahi kuniuliza kwamba: “Hivi wewe Mbunge tumekutuma huko kwenda kufanya kazi gani? Ni kwa nini hufuatilii masuala haya?” Nimemuuliza Waziri, akasema kwamba fedha zipo, zipo wapi kama hazipo kwenye vitabu vya Bajeti za Serikali? Wakati mwingine ni lazima tuwe waangalifu sana na tujue kwamba hiki kitu kinaweza kikatuletea matatizo makubwa sana hasa kisiasa, kwa sababu hii barabara imeongelewa tangu tumejitawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninajua kabisa kwamba Rais Benjamin William Mkapa, ni mtu mahiri sana, daraja la Ruffiji lilikuwa ni hadithi tangu tumejitawala, lakini sasa limejengwa na binafsi nilikuwa na uhakika kwamba barabara hiyo sasa itajengwa. Niliuliza habari hizi kwenye Vikao vya CCM nikaambiwa nitajibowi, lakini bado sijapata majibu. Namwomba Waziri Mkuu atakapokuwa ana-*windup* anijulishe kwamba hii barabara itajengwa na kwa nini fedha hazipo? Kwa kweli ni lazima tukae chonjo sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, ninaiomba Serikali, pamoja na kununua ndege ya Rais, inunue *helicopter* ile ya *engine* mbili ili kusudi Viongozi wetu Wakuu wanapokuwa wanatakiwa kwenda kwa haraka mahali ambapo magari hayaendi haraka waende kwa kutumia *helicopter* hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia, napenda niwapongeze ndugu zangu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, japo mwaka jana nilichemsha sana hapa kuhusiana na Wizara hiyo, kwa kweli kazi wanayoifanya ni nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo ni lazima tuangalie, ukisoma historia ya matatizo ambayo yanatokea Liberia, Sierra Leone, Somalia, *DRC* na kadhalika, utakuta kwamba watu walianza kama majambazi, halafu walipoji-*consolidate* ndiyo wakaanza kupambana na Serikali na mmeona sasa mambo hayo yameanza! Niliwaambia tangu siku nydingi, ikitibidi tutumie hata Wanajeshi kusudi tuondokane na hali hii kwa sababu baadaye itakuja kututokea puanii. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jana nilisoma gazeti la ...

MBUNGE FULANI: *Sunday News?*

MHE. LEONARD N. DEREFA: Siyo *Sunday News* ni lile ...

MBUNGE FULANI: *The Guardian?*

MHE. LEONARD N. DEREFA: Hapana!

MBUNGE FULANI: Alasiri?

MHE. LEONARD N. DEREFA: Hapana, ni lile lenzake na *Sunday News, Daily News.* (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimeona Halmashauri na Manispaa zote wamepewa miradi, lakini nimeshangaa kuona Shinyanga hatukupewa mradi na kwa bahati mbaya sisi ndiyo kitinda mimba katika suala la Manispaa! Kwa hiyo, nasi tunaomba tupewe miradi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kusema kwamba, kodi inayotozwa kwenye madini ni ndogo sana, ni lazima tuongezwe nao na waboreshe kodi hiyo. Halafu kitu ambacho kimeanza kujitokeza sasa hivi ni kudhalilisha Watanzania wanaofanya kazi huko migodini. Sasa hivi wanapimwa UKIMWI na majibu ni lazima yatoke Afrika Kusini.

Vile vile, wanapima *stress evaluator* eti kuwacheki kama ni wezi, halafu na majibu yanatoka Afrika ya Kusini, huu ni udhalilishaji wa hali ya juu. Ninaomba Waziri wa Kazi ajaribu kufuatilia suala hili, kwa kweli kama tutaruhusu watu kuja kuwekeza hapa na kuja kutudhalilisha siyo jambo zuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na natamka kwamba naunga mkono hoja hii, pia, mambo niliyoyasema yarekebishwe. Ahsante sana.

MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia. Pia, napenda kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wapya walioingia Bungeni katika kipindi hiki, ninawakaribisha sana na tunategemea michango yao na ushirikiano wao mkubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake wote wawili pamoja na watumishi wote wa Ofisi yake, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kutengeneza na kutayarisha Makadirio ya Bajeti ya mwaka huu wa 2003/2004 kwa kina na kwa ufahamu mkubwa ambao umetuwezesha leo hii kuwa hapa na kuchangia, kwani isingejuwa hivyo, tusingeweza kutoa michango yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa napenda kuchangia kuhusu Makao Makuu Dodoma. Napenda kutoa pongezi kwa Serikali kwani kuna maendeleo ambayo yamefanyika kuanzia jambo hili lilipoamuliwa hadi hivi sasa. Mimi binafsi ni mmoja wa watu ambao wameishi na kusoma Dodoma, kwa hali hiyo ninafahamu Dodoma ya zamani, ile ya miaka ya 1970 na Dodoma ya sasa hivi. Kuna maendeleo makubwa, tunaona majengo ambayo zamani hayakuwepo, tunaona maeneo mapya kama

ya *Area C* na *Area D* ambayo hayakuwepo. Kwa hiyo, kuna juhudi zinazoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, katika mambo yote yanayoelezwa katika kuanza kuhamia Dodoma, sijasikia chochote ambacho kinazungumziwa kuhusu nyumba na Ofisi za Balozi mbalimbali. Naona Wizara zinahama, lakini kuhusu Balozi za nchi mbali mbali sifahamu itakuwa vipi kwa sababu naona wanazidi kujizatiti Dar es Salaam tu, wanajenga maofisi makubwa na majumba makubwa (ngome). Kwa hiyo, sielewi kama wameruhusiwa kubaki huko au kama kuna mkakati wa wao kuhamia huku Dodoma. Wakibakia Dar es Salaam, wasiwasi wangu ni kwamba, itakuwa exercise ngumu sana kwa Serikali kuwa Dodoma wakati Balozi mbalimbali zikiendelea kuwa Dar es Salaam!

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, napenda kuchangia kuhusu vita dhidi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI. Ninaipongeza Serikali kwa juhudi inazofanya katika kupiga vita ugonjwa huo. Kwa kweli sasa hivi ukienda Vijiji, hata watoto wadogo wanajua UKIMWI ni kitu gani, mitaani wanajua jinsi ya kujikinga na UKIMWI, kitu kama condom ni wimbo ambao kila mtu anauimba, hii yote ni juhudi za Serikali katika kupamba na ugonjwa huo. Lakini hizo ni juhudi za upande mmoja tu, Serikali imekazania kuhusu kuzuia ambukizo la UKIMWI, lakini bado najiuliza. Sasa hivi watu wanaoumwa ni zaidi ya milioni 2 hapa nchini. Je, hawa tunawaacha waendelee kufa kwa kukazana kudhibiti tu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa watu wanaoumwa, wanahitaji kuendelea kurefusha maisha yao na njia ya kurefusha maisha yao ni kupata dawa za kuwastiri na kuwaongezea siku zao. Katika Bajeti ya safari hii, nimeona Serikali imeelezea mikakati yake, kwamba inajitayarisha kusambaza dawa za UKIMWI, lakini haikueleza kwamba; je, dawa hizi zitakuwa ni bure au zitasambazwa ili kila mtu ajinunulie? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waathirika wengi wa UKIMWI ambao wanafariki mapema, ni wale wasiojiweza na kwa sababu hawajiwezi, mambo ya kujinunulia dawa bado itakuwa ni ndoto ya mbali. Wataendelea kuishi hivyo hivyo na wengi wao watakimbilia kwa waganga wa kienyeji, huko nako wataambiwa wamerogwa na wakati huo hali itazidi kuwa mbaya na tutazidi kupoteza maisha ya Wananchi wetu wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nzuri za Serikali kwa upande wa dawa, natoa pendekezo kwamba dawa hizo zigawiwe bure kwa sababu watu wengi hawajiwezi.

Pia, katika kuwasaidia walioathirika lishe inahitajika na nitatoa mfano wa Marekani. Nchi hiyo wamegundua kwamba lishe ina mchango mkubwa katika kumuongezea mtu maisha yake, kuliko hata kukazana na dawa peke yake. Hapa Tanzania lishe ndiyo kikwazo kikubwa, kwa sababu ni watu wangapi wanaoweza kupata chakula bora cha kuwasaidia kuzidi kuongeza siku zao na wapate vile viini vyakurutubisha miili ili waweze kuendelea kuishi?

Mheshimiwa Spika, binafsi naona kwamba katika suala la lishe, nchi yetu imebarikiwa sana, kwa sababu tuna ardhi nzuri, zile lishe ambazo nchi zingine

wanahangaika kuzitafuta mfano mboga za majani sisi tunazo kwa wingi, karanga tunazo na matunda tunayo. Sasa Serikali igeuze msimamo na ianze kufundisha na kusisitiza mambo ya lishe na pia pale inaposhindikana, wasaidie kutoa lishe ili tuokoe maisha ya Wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kuzungumzia kuhusu udhibiti wa madawa ya kulevyia. Kwanza natoa pongezi kwa Serikali kwa sababu tunaona kila siku kwenye *television* na kusoma kwenye magazeti, kwamba watu wamekamatwa wamemeza vipaketi vya madawa ya kulevyia. Kwa hiyo, hizo ni juhudhi ambazo Serikali inafanya ambapo zamani hazikuwepo. Lakini pamoja na juhudhi hizo, bado hali inaonyesha kwamba madawa ya kulevyia yanaongezeka na kama bado yanaongezeka inatufanya tuamini kwamba bado hatujafikia kwenye shina au mzizi ili kujua chimbuko kubwa ni nini! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu vijana wote hawa wanaokamatwa na kuonyeshwa kwenye *television*, ni vijana wadogo kati ya umri wa miaka 18 - 25, ninajiliza vijana wadogo kama hawa, wana uwezo wa kuwa na fedha za kununua tiketi kwenda nchi za nje kuleta madawa?

Pia najiuliza, mtaji wa madawa kama haya ni mkubwa. Je, watoto wadogo kama hao ambao wengi wao wanatoka kwenye familia maskini wanatoa wapi fedha kama hizo za *ticket* ya ndege na kununulia madawa hayo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna usemi unaosema kwamba: ‘Ukitaka kukausha mti kata mizizi yake.’ Kwa hali hiyo, hawa watoto wetu wadogo tunaowakamata wamemeza madawa, wanapelekwa jela na kadhalika, ni matawi tu, lakini kuna mizizi yake! Basi kama kuna hiyo mizizi, napenda kuitahadharisha Serikali kwamba kazi hii bado ni kubwa sana. Hawa watoto watakamatwa, lakini hiyo mizizi ina uwezo, *wata-recruit* vijana wengine, watawapeleka kufanya hiyo biashara, vijana hawana ajira wanachukulia ile kama ni ajira halali. Anakwenda kule analeta mzigo analipwa kazi imekwisha, yeze kajipatia chochote!

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri muda mwangi ninakuwa Dar es salaam, katika kupita pita mitaani, ukiwaona hawa vijana ambao wanatumia hayo madawa ya kulevyia wanasisitisha na baadhi yao wanatisha! Sisi Akinamama huwezi ukapita usiku mitaani peke yako kwa sababu watakukuba wakupokonye chochote ulichonacho ili mradi wakanunue madawa ya kulevyia siku hiyo! Akinamama majumbani nao wanaishi maisha ya wasiwasi, kwa sababu hawa watoto wamefikia hatua hata ya kupora vitu majumbani ili wauze na wapate pesa za kwenda kununua hayo madawa, ikishindikana hata kijiko ndani ya nyumba anakibeba, anakwenda kuuza ili apate pesa ya kununulia dawa za kulevyia siku hiyo!

Mheshimiwa Spika, binafsi naona kwamba, haya madawa ya kulevyia zaidi ya kupoteza nguvukazi ya baadaye, pia yanaleta umaskini mpaka katika familia. Baadhi ya Wananchi wengi wakiongea inaelekea kwamba wana *information* wanazozifahamu, kwa sababu utakuta wanajua kwamba yule ni teja, anachukua dawa mahali fulani. Sasa kama

hali ndiyo iko hivyo, ina maana Wananchi wanajua *information* ambazo zingeweza kuisaidia Serikali, lakini je, usalama wa maisha yao baada ya kuongea mambo hayo utakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwa Serikali katika mikakati wanayoifanya, japo hatujui, lakini waweke matangazo ya kuwaelimisha Wananchi na kuwahakikishia usalama wao, huenda watapata *information* ambazo zinaweza kusaidia katika kupiga hatua zaidi katika kupambana na vita hii dhidi ya madawa ya kulevyta.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabla kengele ya pili haijagonga, napenda kuongelea kuhusu mchango wa Asasi zisizo za Kiserikali - *NGOs*. Kwanza, naishukuru Serikali mpaka hivi sasa wameweza kuweka mambo bayana, Sera ya *NGOs* imetayarishwa na ni nzuri, Sheria yake pia imeshatoka, ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Serikali kwamba, *NGOs* ni Mshirika Mkuu wa Serikali katika kuleta maendeleo na kwa sababu mambo yote yako bayana, basi Serikali isisite kutumia *NGOs* kila mahali inapotakiwa, kwa sababu hali ya hivi sasa ni kinyume na ilivyokuwa.

NGOs wanahangaika wenyewe kutafuta ni kazi gani wazifanye wakati Serikali ina mambo mengi ya kupiga vita, kama UKIMWI, madawa ya kulevyta na kadhalika. *NGOs* ziko karibu sana na Wananchi wangetumiwa kwa kazi kama hizi wangeweza kusaidia kwa hatua kubwa sana. (*Makofi*)

Kwa hali hiyo, ninaiomba Serikali itumie *NGOs* na pale inaposhindikana wakijua kazi hizi zipo wazitangaze ili waweze kuzifanyia kazi na kuisaidia Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, napenda kuunga hoja hii kwa asilimia mia moja na ninashukuru kwa kunipa muda wa kuongea. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. HADIJA K. KUSAGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa vile leo ni mara ya kwanza kuchangia katika Bunge hili la Bajeti kwa mwaka huu, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa hivi karibuni na tunawakaribisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia, kwa vile sikuweza kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza sana hotuba hiyo na kwa kweli Wananchi wangu wa Temeke wamefurahishwa sana na mambo ambayo yamo kwenye hotuba hiyo, hususan kuondoa kabisa kodi ya maendeleo ambayo ilikuwa ni kero kwa Wananchi wa Temeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze katika kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza ninampongeza sana, hotuba yake ni nzuri na imegusa kila eneo. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana dada yangu Mama Rose Lugembe, ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Watendaji wote kwenye Ofisi hii ya Waziri Mkku, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuchangia ukurasa wa 29 katika kitabu hiki kidogo cha Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze na kifungu namba 34 katika ukurasa huo wa 29 ambacho kinalezea Sekta za Huduma za Kiuchumi. Nimesoma kifungu hiki kwa makini sana na kwa kweli ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuweza kugusa maeneo mengi, lakini nitaanza kuzungumzia suala zima la barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Manispaa yangu ya Temeke hupokea fedha kutoka Mfuko wa barabara kupidia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kila robo ya mwaka. Mwaka jana Manispaa yangu ilipokea zaidi ya Shilingi 164 milioni, fedha hizi zilitengwa kwa ajili ya kuleta maendeleo katika Manispaa hiyo. Kwa bahati nzuri sana kwa kuongezea na fedha ambazo sisi wenyewe tunajitafutia kwenye Manispaa yetu, tumeweza kuzitumia kikamilifu na kuweza kutengeneza barabara ambazo zilikuwa zinatutatiza kilomita zipatazo 91 na kwa kweli tumepunguza kero kwa kiasi kikubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuzitaja barabara ambazo zimepata bahati ya kutengenezwa. Mojawapo ni barabara ya Buyuni ambayo imetengenezwa kwa kilomita 20, barabara ya Mjimwema - Tungi, imetengenewa kwa kilomita sita, barabara ya Yombo Vituka imetengenezwa kwa kilomita 14, barabara ya Mbagala Kuu nayo imetengenezwa kwa kilomita 10, barabara ya Vumilia Ukooni imetengenezwa kwa kilomita 11 na barabara ya Chekeni Mwasonga imetengenezwa kwa kilomita 20. Jumla ni kilomita 94. Tumetengeneza kwa kutumia fedha ambazo tunapewa kwenye Mfuko wa Barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa kutuwezesha kufanya mambo hayo. Lakini si hayo tu, pia, barabara ya kutoka *Davis Corner* iliyoko Tandika kuelekea Makangarawe, ilikuwa ni tatizo kubwa kwenye Jimbo langu la Temeke, lakini sasa hivi inatengenezwa kwa kilomita zipatazo 6 kutokana na fedha hizo tulizoletewa. Lakini tutaitengeneza kwa kiwango cha changarawe. Ninaipongeza sana Serikali kwa sababu imetusaidia katika kuondoa kero hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni kubwa zaidi ni kwamba, fedha hizi tumezitumia kuweza kutengeneza madaraja mbalimbali ambayo yalikuwa yakitusumbua hususan daraja la Kilakala.

Daraja la Kilakala kwa upande wa Jimbo langu la Temeke lilikuwa ni tatizo na hasa kwa Akinamama kwa sababu lilikuwa linatenganisha Mjini na Vijiji, yaani wakazi walioko Yombo Vituka walikuwa wanatenganishwa kufika Mjini kutokana na kikwazo cha daraja hili, sasa hivi limeishatengenezwa na magari yamenza kupita.

Kwa hiyo, akinamama waliokuwa wanajifungulia watoto njiani, sasa hivi wanakimbizwa hospitalini haraka, iwe ni Temeke ama Muhimbili, kwa kweli, tunaishukuru sana Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nijielekeze kwenye barabara ya Kilwa. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Sophia Simba, kwani ameweza kuzungumzia suala hili. Binafsi pamoja na Mheshimiwa Magoba, tumepata tatizo kubwa sana hapa. Tumesemwa sana kuhusu barabara hiyo hasa pale Serikali ilipoanza kuitengeneza. Wananchi wamebomolewa majumba yao na wengine wamefariki kwa kupata mshtuko!

Mheshimiwa Spika, jambo hili ninalizingumza kwa masikitiko makubwa sana. Wananchi wamebomolewa majumba yao na bado Serikali haikuweza kuwawezesha angalau kwa kiasi fulani ili kuondoa makali ya kubomoa nyumba hizo, wameachwa tu, sana sana tumetupiwa Manispaa yetu ya Temeke ili tuweze kusaidia matatizo hayo. Lakini tutayaweza? Hivi ni kweli Serikali mmeagizwa mwende mkafanye fujo halafu muwaachie Manispaa warekebishe? Jambo hili ni la kushangaza sana! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali, tuliambiwa kwamba barabara ile inakwenda kupanuliwa, lakini toka Wananchi hao wamebomolewa ni jambo la kusikitisha sana, yapata mwaka sasa hakuna kinachoendelea, kinachofanyika hapo ni kukarabati mifereji tu. Sasa, ni kweli Wananchi wale walibomolewa nyumba zile ili wakarabati mifereji? Ama walibomolewa nyumba zile ili barabara ile iweze kupanuliwa?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninazungumza kwa masikitiko makubwa sana. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ana jeuri kubwa sana, unapomfuata kumweleza suala lolote. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ni mkali na anasema: ‘Sisi hatuna fedha za kuwalipa.’ Hana ile *polite language*, hana! Ninasikitika sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Waziri Mkuu amwulize nini hatma ya wakazi wa Barabara ya Kilwa? Sisi tuko hatiani sana na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Magoba ameandika barua kupeleka kwa Mheshimiwa Rais na ninayo *copy yake* hapa ameniletea na ye ye analalamikia suala hili hili. Wananchi wetu wametupwa, mpaka wanajiuliza hivi kuna Serikali hapa? Kwa kweli hawatuelew! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba niongelee kuhusu suala zima la *TASAF*. Napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea Mfuko huu wa *TASAF*. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, katika Wilaya ya Temeke, tulibahatika kuwemo katika mpango huu wa *TASAF* na kwa kweli tumefaidika sana.

Kuna miradi mingi ambayo tumeifanya kupitia Wananchi kwa kuchagua wenyewe kwamba hapa tuna tatizo gani tufanye na kwa kweli imekwenda vizuri. Sasa hivi tunavyo visima vyta kutosha na tumeweza kuongeza idadi ya madarasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini si hilo tu, pia tumeweza kutengeneza mifereji katika barabara nzuri ambazo zimejengwa. Wananchi walihofia wakasema: "Kama hatukuweka mifereji, basi barabara hizi hatutaweza kudumu nazo." Kwa hiyo, Wananchi waliweza kupata ajira, ungebahatika kufika ukakuta Akinamama, Wazee kwa Vijana wanavunja mawe kwa ajili ya kutengeneza mifereji, usingeamini. Tumenufaika sana na Mfuko huu wa *TASAF*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, apeleke salaam zetu za pongezi, kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea Mfuko huu. Umeboresha na umeondoa umaskini kwa Wananchi wangu wa Temeke. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu kuondoa umaskini. Nadhani sote tunafahamu kwamba mwananchi huwezi kupata maendeleo bila kukopa. Hata Serikali inakopa na ndiyo maana tunasema tuna madeni na tunadaiwa.

Mheshimiwa Spika, binafsi nilikuwa napitia hotuba hii ya Waziri Mkuu, kwa bahati mbaya inawezekana nime-*overlook*, hakuna sehemu ambayo imeeleza nini mikakati ya makusudi inayofanywa na Serikali kuhusu mikopo kwa upande wa akinamama pamoja na vijana, sikuona! (*Makofî*)

Ninatarajia Mheshimiwa Waziri Mkuu, ataliangalia suala hili, ili kuona ni kwa kiasi gani tunawawezesha akinamama pamoja na vijana kuhusu kuwapa mikopo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sisi wananchi Mkoa wa Dar es Salaam tumeanzisha Benki yetu ya Wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam. Benki hii bado ni changa lakini imeanza kutoa mikopo kwa kiasi kidogo sana, elfu hamsini, hamsini.

Mheshimiwa Spika, sasa tatizo letu kile kiasi cha shilingi elfu hamsini unafanya biashara gani ya kuweza wewe kurejesha mkopo uliokopa? Kwa sababu ni hela kidogo sana. Kwa hiyo, wananchi wanapochukua zile fedha wanafanya biashara ndogo ndogo ambazo zinalingana na wateja ni wale wale tunanyang'anyana kwa hiyo wanashindwa kurejesha ile mikopo. Vile vile bado kuna taasisi mbalimbali za watu binafsi kama vile *pride, thinker* na *kadhalika*. Hawa tunamshukuru sana, Mheshimiwa Basil Mramba, ametuelekezea waweze kutupatia mikopo na kwa kweli wanatoa. Lakini masharti yao ni magumu. Wananchi wetu wanashindwa kumudu kurudisha riba kwa sababu ni kubwa sana ndugu zangu. Ni kweli tunapata mikopo tunashukuru, lakini unapewa elfu hamsini ni biashara ya kununua unga wa ngano hakuna zaidi ya hapo. Leo huyu anatengeneza maandazi mwingine chapati, wanunuvi ni wale wale wanashindwa kupata faida ya kutosha. (*Makofî*)

Sasa kutokana na kutopata faida wamekuwa wanashindwa kurejesha ile mikopo. Kinachotokea hapo ndugu zangu ni kitu cha kusikitisha sana. Watu wa *thinker*

na *pride* wanakuja kuchukua vitanda na magodoro. Kwa hiyo, mwananchi huyu unakuwa umemwezesha au umekwenda kumwongezea umaskini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu mjaribu kutuwezesha kwa njia nyingine katika kupata mikopo. Benki yetu ya wananchi wa Dar es Salaam inaendelea, lakini bado uwezo wake ni mdogo haijaweza kuweka mitandao kuenea mpaka vijijini.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu ambao ni wa mwisho ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ajaribu kuongea na hawa wenzetu hususan Wizara ya Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, wajaribu kutenga fedha ambazo zitatolewa kama mikopo kwa vikundi mbalimbali vitapunguza makali ya kutegemea hizo *NGOs* ambazo zinatoza riba kubwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, mwaka juzi sisi Wilaya ya Temeke tulipata fedha kiasi cha shilingi milioni mbili.

WABUNGE FULANI: Ni kidogo sana.

MHE. HADIJA K. KUSAGA: Ndiyo ni kidogo lakini ziliweza kugawia vikundi 8 na walipata faida kuanzia laki moja na nusu, laki mbili. Sasa kama tutafanya hivyo kutoka Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, basi tutaweza kujikwamua kwa kiasi fulani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nisisahau Wananchi wa Temeke wamenitura nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, apeleke salamu za pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kuweza kukamilisha ujenzi wa Daraja la Mto Rufiji. Kwa kweli tunampongeza sana na wameniomba daraja hilo ili kuweka kumbukumba basi, liitwe Benjamin Mkapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kutoa shukrani zangu zingine za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kukubali Uwanja wa Kisasa uoteshwe pale Wilayani Temeke, kwa kweli tunamshukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, asilimia mia kwa mia. Nakushukuru sana. (*Makofî*)

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri walio chini yake kwa kazi nzuri ya kuleta hotuba ambayo ina mwelekeo na ina hekima nyingi. Kwa kweli inaridhisha kwa hiyo mimi ninaiunga mkono moja kwa moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sikupata nafasi ya kuzungumza napenda nipongeze hotuba ya Bajeti iliyopita kwa kweli imetupa matumaini. Kwa hilo, napenda nimpongeza Rais wetu kwa hekima na busara anazozitumia kwa kuwatumia Mawaziri wake na viongozi kuweza kuangalia hali za wananchi. Naishukuru Serikali ya CCM kwa

kuondoa ada ya shule za msingi na watoto wetu kuweza kusoma, kuondoa ada katika vyuo vya ualimu na walimu wengi kujunga na ualimu, kuahidi kuajiri watendaji wa vijiji ambao walikuwa wanasota kwa muda mrefu na ni watendaji wakubwa nawashukuru kwa hilo.

Vile vile kuondoa kodi ya maendeleo. Kwa kweli ilikuwa inanyanya wananchi na wengi walikuwa wanahangaika. Nadhani tukubaliane na akina mama kwamba walikuwa wanateseka, walikuwa wanakosa mambo mengi kwa sababu ya wazee wao kujificha. (*Makofi*)

Vile vile naipongeza Serikali kwa kujenga nyumba za walimu pamoja na madarasa. Kwa kweli ni wazo la busara. Labda tu kuna malumbano kidogo tu kwamba sijui ni sisi tumeanzisha hiyo kauli, napenda niseme tu kwamba wananchi wetu si kwamba hawana akili, wanaelewa Serikali ni ya nani. Sasa tunapotaka kuchukua Serikali hewa utakuwa na matatizo lakini wananchi wanaelewa kwamba nani ameleta hiki. (*Makofi*)

Kama unataka labda subiri kwenye mwaka 3000 labda utaondoa nauli za mabasi na ndege lakini sasa hivi ni CCM imefanya hivyo na ni Serikali yake. Kwa hilo mimi naipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda ningependa nizungumzie kuhusu suala la elimu ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu, amelizungumza pamoja na kujenga madarasa, nyumba za walimu, nafikiri sasa inabidi tuangalie watendaji, walimu na wenyewe tuangalie maslahi yao kwa sababu tutakuwa tunapoteza muda. Tutakuwa na vyumba, madarasa lakini watendaji tusipowaangalia maslahi yao kwa kweli hakuna kazi itakayofanyika. Kwa hiyo, ni vema tuangalie watumishi. Walimu sasa wanakwenda likizo hawapewi haki zao, anakwenda hospitali hapewi haki yake, anapewa *transfer* wanadai fedha nyingi hawalipwi.

Sasa kwa mazingira yale usitarajie kwamba atafanya kazi katika hali ya raha. Hata madaraka yao, ukienda kufanya *analysis* ya mshahara wa mwalimu mkuu wakati mwingine anazidiwa na mwalimu wa darasa. Afisa taaluma hana hata *allowance, headmaster* mwenye shule yenye wanafunzi 1000 analingana na mwenye wanafunzi 300. Kwa hiyo, vyeo vimekaa ovyo ovyo, hebu boresheni hapo muone mambo yatakavyokwenda. Kwa kweli nilikuwa naiomba Serikali ijaribu kuliangalia hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeondoa kodi ya maendeleo, nashukuru sana. Lakini mimi naomba kwenye fedha za ruzuku ijaribu kuangalia kwa makini itumie vigezo vitakavyoweza kusaidia wananchi ili zisije fedha zikawa zinaenda uelekeo mmoja au kwa sababu kuna wajanja eneo lile basi zitaelekezwa huko. Ikiwezekana itumie sana sensa ya idadi ya watu itaweza kusaidia. Vinginevyo tutakuja kugombana hapa. Kwa sababu zinatoka mkondo mmoja naomba angalieni idadi ya watu katika kugawa fedha hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja hii kwa nguvu zote ukurasa wa 31 na 32 Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameeleza vizuri jinsi madini yanavyosaidia maendeleo ya nchi hii na yanavyochangia kodi. Kwa kweli ni kitu kizuri sana na nafikiri neema imeletwa na Mungu, katika nchi na kwenye maeneo mbalimbali. Lakini mwaka 2001 kwenye maeneo ya madini kulitokea hoja ya watu kuomba mrahaba, labda tulitumia lugha mbaya. Mimi nilivyoolewa tulikuwa tunaomba msaada wa kuweza kuimarisha maeneo yale fedha kwa ajili ya kuweza kuendeleza maeneo hayo yaendelezwe. Karibu maeneo yote yanayotoa dhahabu wananchi waliopo pale kwa kweli wanatisha, ni maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa Wilaya ya Geita, ina watu laki saba na kumi na mbili, inakaribia Mkoa wa Lindi na inakaribia kidogo Zanzibar. Lakini kuna mgodi mkubwa wa machimbo. Ule mgodi umekuwa ni kero sana kwa wananchi. Kwanza ardhi imechukuliwa, umewekwa pale njia zimepindishwa watu wanasaafari umbali mrefu kwenda mjini Geita, ushirikiano hawana, magonjwa yameongezeka, idadi ya watu ni kubwa, bei imepanda, hakuna miundombinu, hakuna huduma za jamii, imekuwa ni shida tu. (*Makofi*)

Sasa tunaiomba Serikali iangalie ichukue kitengo hicho, Mheshimiwa Waziri Mkuu chukua kitengo kile kama sehemu ya maafa ya sehemu yako. Kama ni UKIMWI unapatikana kwa wingi sana maeneo hayo. Ni kweli kwamba kuna siku mgodi unachangia fedha kwenye Serikali, lakini hata kama ni *cake* ya taifa lakini kuwe na *direct impact* ya watu wa pale wapate na *spice over*, yale maji yanapomwagika angalau wapate pate manyunu. Sisi tunaambiwa matajiri lakini tunalalia ngozi, bararabara, hakuna. (*Makofi*)

Siku moja Waziri alizungumza akasema kwamba wanatengeneza barabara, barabara gani wanatengeneza? Wametengeneza barabara yao ya kutoka Ilogo kwenda Kahama ya kwenda kuchukua bidhaa zao sehemu za Kahama na imepita porini walivyo washenzi. Haikupita kwenye miji ya Kata kusaidia wananchi, barabara ambayo wanetusaidia ya kutoka Usagala kwenda Geita mjini. Wanaleta mafuta yanaingia kule nafikiri kwa msamaha, yanapita yanaingia Mjini Geita, lakini yanaharibu barabara. Fedha yote ya Mkoa inaishia pale na bado barabara ile mbovu. (*Makofi*)

Ukisafiri kutoka Geita kwenda Mwanza ni masaa manane ni shida kwa nini walikuwa wameandika barua walitudanganyadanganya eti wataweka lami, wala hakuna lami wala hakuna chochote walichoweka. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakuomba uwaambie kwa sababu wamefikia hatua ya kumwita Waziri bwana njoo, anakuja hajawasiliana na Mkuu wa Mkoa, hajawasiliana na Mkuu Wilaya sasa huyo tutamwambia kweli atatusaidia? Kama anakuja mbio namna hiyo, tunaidhalilisha Serikali. Wewe Serikali unaitwa njoo, unamwuliza Mkuu wa Mkoa, wewe vipi nije kuna nini? Mkuu wa Mkoa hana habari.

Kwanza inatakiwa Mkuu wa Mkoa afahamu kwanza anaingia maeneo hayo lakini siyo kuingia bila taarifa jamani! Mimi nashindwa kuelewa sijui mambo haya yanakwenda namna gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine nafikiri tuangalie na hii Mikataba ya asilimia 3, jamani yaani mimi nina dhahabu unanipa asilimia 3, yaani, kwa nini tusielewane? *Okay running cost* tunazitoa, kilichobaki tugawane kwa sababu na mimi nina mali pale, kama wewe ni tajiri tunagawana *parts*. Basi unizidi angalau kidogo lakini tugawane. (*Makofi*)

Mimi nina wasiwasi kwamba sisi tulio kwenye uongozi hasa Wabunge rafiki zangu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya tukizikwa eneo la Geita uzeeni wajukuu wetu tutakapokufa watakuwa wanapiga makaburi yetu na kusema shenzi ulikuwa Mbunge, mali yote ikaenda kwa wageni, watakuwa wanapiga makaburi yetu kwa nguvu sana. Kwa sababu hakuna kitakachobaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nieleweke kwamba dhahabu zinakwisha siyo kama pamba *is not renewable* sasa ikiisha tutabaki na nini sisi? Kwa kweli inatusikitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni fidia. Kinachosikitisha sana tarehe 26/5/2003 wakati nakuja Bungeni wananchi walikuwa wamemzingira *DC* wanataka kumkong'ota, Wabunge tukajikusanya tukaenda kubembeleza wananchi, wamehamishwa, wananchi wazee wa miaka mingi sasa hawajapewa fidia. Sasa sijui wanaidai Serikali? Lakini walituambia tunaomba ruhusu tumwondoe huyu aliyeingia kwenye eneo letu, sisi tuanze kuendelea na kazi zetu za kulima. Waliondolewa pale. Rais alikuja akaahidi kwamba taratibu zitafuatwa watalipwa sasa jamani ahadi za Rais aliye kule juu nafikiri kwa nchi hii ye ye anamuata Mungu ndiye ametamka hatuwezi kutekeleza ahadi zake? Wametuambia turudi na jibu kwa kweli msipotupa jibu la fidia haturudi Mheshimiwa James Musalika, wewe Mheshimiwa Ernest Mabina utakwenda sijui watakuweka wapi? Sisi hatuwezi kurudi Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakwenda kwa Rais. Wananchi wanataka fidia. Mimi kila siku kuna wazee wanakuja kuzunguka nyumba yangu wanakuja wanauliza fidia, wanasema tunakuja kula kwako mmeshatuondoa tuambie Serikali yenu hii itatulipa lini? Sasa tufanye nini ndugu zangu? Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini tulisikitika alipoondoka bila kuzungumza na wananchi, angalau akatuuliza ndiyo hayo Mheshimiwa Waziri tunakuomba utusaidie, njoo, ulikuja kule, tunaomba uje tena.

La mwisho napenda niombe hizi *NGOs*, *TASAF*, kwa nini kwetu Geita haziji? Tunaona magari yanapita ya kwenda Bihamulo, sasa mpaka tuweke mawe barabarani ndiyo mjue kwamba tumekasirika, wanatuharibia tu barabara sisi! (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mna dhahabu,

KABUZI F. RWILOMBA: Tuna dhahabu! Tunafaidika na dhahabu hiyo? Kwa kweli naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na sisi hizi *NGOs* zije kwetu ili tuweze kufaidika au kwa sababu shule yenye watu ni wengi tunaongoza katika nchi nzima idadi ya wananchi, lakini chuo kikuu hata mmoja hayupo? Ndiyo maana labda hatupatiwi hivyo vitu. Lakini tunaomba vije basi hata kama hatukusoma tusaidiwe baadaye tutasoma na sisi tutapata wawakilishi, tutapata Mawaziri nakadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifikirie posho ya Madiwani kwa kweli wanateseka. Wanafanya kazi kubwa sana, wafikirieni.

Ninaomba vile vile hiki kidogo wanachopata Wabunge kinachopelekwa kwa Ma-DC kipelekeni kwenye Ofisi ya Spika, mnatugombanisha na Ma -DC yaani ni kero kwa nini kisipitie kwenye Ofisi ya Spika. Kwa mfano kama zinakuja kidogo mfano shilingi elfu hamsini tunagombana na wahasibu. Zipitie kwenye mfuko wa Spika. Vile vile anasema anakwenda kututengenezea Ofisi, Ofisi zenyewe ziko wapi?.

Mwisho naomba umeme vijijini. Kama kweli tunasema dhahabu ni kitu kizuri na tunakihitaji basi tuwasaidie hata wachimbaji wadogo wadogo nao wanufaike, tuisaidie tu hawa wawekezaji, ndiyo tunawawekea sheria laini. Naunga mkono hoja kwa nguvu zangu zote. (*Makofi*)

MHE. STEPHEN M. KAHUMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ambayo pengine itakuwa ya mwisho mchana huu, lakini nashukuru zaidi kwa kuniita baada ya Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba ambaye amenipa msingi wa kufanya kazi kwa sababu anatoka kwenye madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitangaze kwamba naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kwa sababu ni nzuri sina matatizo nayo. Niliyotaka kuzungumza leo nitazungumza kidogo kwa sababu tarehe 5 nilifanyiwa *operation*. Kwa hiyo, sikuweza kusoma kitabu, ili kuweza kupata takwimu nzuri za kunisaidia kuboresha hotuba hii. Hata hivyo ninapenda tu kwanza niwapongeze ndugu zangu Wabunge wapya kwa kuchaguliwa kwoao na pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa niaba ya Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kwa kukubali kutupatia fedha za kujenga jengo la Halmashauri badala ya lile letu lililochukuliwa na Mahakama. Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua kwa sababu tuliiingia pamoja hapa Bungeni, kilio hiki nimekuwa nikikisema mara kwa mara mpaka Mahakama ilighadhhabika ikasema basi tunahame twende Kigoma. Tukasema Mahakama Kuu tunaitaka, lakini tunaomba Serikali itusaidia kutupatia uwezo wa kujenga jengo lenye hadhi ya Manispaa ya Tabora. Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Tabora amenitura nishukuru kauli ya Waziri ya kwamba tutapatiwa fedha ya kujenga jengo jipy. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda nishukuru Serikali kwa kufuta kodi zenyeye kero na vile vile kwa kuongeza kiwango cha pensheni ya wastaifu wenzangu. Lakini nilizungumza na Katibu wa Wastaifu wa Mkoa wa Dodoma alisema wamefurahi sana, lakini wangependa zaidi kama malipo hayo wangekuwa wakipewe mwezi kwa mwezi kwa sababu miezi sita ni muda mrefu na wao wengine wanadaiwa kodi za pango, wenye nyumba hawawezi kungoja miezi sita ndiyo wadai kodi za mapango yao. Kwa hiyo, nilipenda niseme kwa sababu wameniomba nifikishe ujumbe. Pia kwa wastaifu ambao kutokana na udogo udogo wa pensheni walichukua mkupuo na bado wako hai, wanaomba wafikiriwe kwa sababu bado wanaishi, lakini wanaishi kwa dhiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie ambalo nilitaka kuzungumza mwaka jana. Mwaka jana kulikuwa na sakata kubwa la uanzishaji wa Mkao wa Manyara na sakata hili lilimkabili sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi nikasema hapa Bungeni kwamba kwa kuwa nina ugomvi na mke wangu, tumekwenda kwa baba mkwe tukakuta naye anagombana na mke tutakunja matatizo yetu tukarudi. Sasa kwa kuwa mambo ya Arusha yamekwisha, nafikiri na mimi niseme kwa uwazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Serikali iliongeza Mkao wa Manyara kwa kuugawa Mkao wa Arusha ambaa ulikuwa ni Mkao mkubwa sana. Mkao huu ulikuwa ukifatiwa kwa ukubwa na Mkao wa Tabora, lakini Mkao wa Tabora ukaongezwa Wilaya. Wakati ule mimi sikujua kwamba Wilaya maana yake ni *DC*, mimi nilidhani wilaya maana ni Halmashauri, lakini baadaye nimejifunza kwamba kumbe *DC* ndiyo Wilaya kwa sababu kule Tabora tulipewa *DC* wa Mjini. Zamani *DC* mmoja alikuwa anashika Tabora Vijijini na Mjini. Sasa wakaweka *DC* wa Mjini na *DC* wa Vijijini. Sasa ikasemwa tumepata Wilaya mpya na ile Wilayaya Tabora Vijiji nadhani tuliipa jina la Uyui, ingawa Waheshimiwa Wabunge, bado wanaitwa Wabunge wa Tabora na mwingine wa Igalula.

Kweli kupatikana kwa *DC* mpya wa Tabora tunafurahia lazima tupokee. Tunampongeza na kumshukuru Rais kwa kutapatia huyu *DC*. Lakini tunapenda kupata Halmashauri nyingine kwa sababu hapa tunapogawa fedha, tunagawa kwenye Halmashauri, Halmashauri zikiwa chache Mkao huo unaathirika kwa kupata hela kidogo. Hata hivyo tumefuta kodi tunasema Serikali itatoa *grand*, haitatoa kwa Ma-*DC*, itatoa kwa Halmashauri. (*Makofî*)

Kwa hiyo, Tabora itaendelea kupata fedha hizo kwa Halmashauri zile zile ambazo tulikuwa nazo. Kitu hicho hatuna matatizo nacho kwa sababu waswahili wanasesma yaliyopitwa si ndwele tugange yajayo. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipata kutembelea Jimbo la Bukene kwa masikio yake mwenyewe alisikia watu wa Bukene wakimwambia kwamba wanataka kuwa na Wilaya kwa sababu Bukene ina sifa zote za kuwa Wilaya na mara nyingi nimeuliza maswali hapa Bungeni nikajibowi kwamba vigezo vyote vya kuweza kuifanya Bukene kuwa sehemu Wilaya vinapatikana. Lakini hali ngumu ya nchi. Hali ngumu ya uchumi.

Mheshimiwa Rais vile vile alifika Bukene na juzi alikuja kuweka jiwe la msingi kule Nzega nikamwambia, mimi kama Mbunge wakanituma nikazungumza naye nikamwambia kwamba hoja kwamba fedha ndiyo tatizo sisi watu Bukene kuichukua kama upopo unapeperusha mvua sasa tukamuuliza Mheshimiwa Rais kwamba ni lini mvua ya mvua ya wima itanyesha Bukene? Kwa sababu kila inapotaka kunyesha upopo unakuja unapeperusha. Mheshimiwa Rais akasema mvua hiyo itanyesha leo. Mimi nikapata imani kwamba sasa amekubali tutapata mvua ya wima kwa maana kwamba tutapata Wilaya. Sasa hotuba ya Waziri Mkuu sikuona mahali popote na simlaumu.

Lakini nina imani kwamba Mheshimiwa Rais alivyosema itanyesha mvua ya wima ilikuwa ni ahadi na haikuwa mzaha kwa sababu Mheshimiwa Rais tangu amenijua

mimi hajanitania hata siku moja. Angekuwa ni Kitwana Kondo ningesema huo utani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, amkumbushe Mheshimiwa Rais kwamba ile mvua bado tunaingoja na aseme kama yeye mwenyewe alivyoambiwa asiaa akaanza na neno eti kwa sababu mtu ukishaanza eti anasema hivi, umekwisha *dilute*.

Mimi nilipokuwa *headmaster* wa shule mwalimu akija kuniambia eti watoto wanalamika uje hauna sukari, namwambia toka hapa kwa sababu hajafanya kazi afadhali uje uniambie nimeona uje kweli hauna sukari, tuongeze kilo mbili umefanya kazi, sasa unataka mimi ndiyo nikaanze kuonja uje. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, kamwambie tu kwamba Watu wa Bukene wanataka Wilaya na uliwaahidi mvua itanyesha. Hilo nilitaka nizungumze hivyo. Lakini nilitaka nizungumze tangu mwaka jana karatasi maalum Mheshimiwa Waziri Mkuu wamempa Wabunge wa Mpanda, Rukwa, Tabora, Kigoma mikoa mitano ambayo tunaathirika na utaratibu wa rolling plan.

Waziri wa Fedha juzi alipokuwa aki-*wind up* amesema atateua Tume ya kuchunguza njia bora ya kugawa fedha. Mimi nikashangaa kwa sababu wanatoa sealing ya kwamba Tabora mpange mpaka hapa ni Wizara ya Fedha na Mipango sasa wanataka wafanye nini zaidi? Wakati ndiyo waliota *sealing*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mikoa hiyo ni Rukwa, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Singida. Nimechukua mikoa mitano, mingine inayopata fedha nyingi sana ni Arusha, ikiwa pamoja na Manyara, Iringa, Tanga, Kagera na Mara. Hii mitano inapata fedha nyingi. Miaka yote inapata fedha nyingi sana. Mimi tumeingia katika Bunge hili na Waziri Mkuu, miaka yote nimekuwa nikiliona hili jambo, nikiuliza hapa napata majibu. Nakumbuka mwaka juzi Waziri Mkuu alijibu kwamba Arusha nadhani mmeendelea, kuna wasonjo wanatembea uchi, hilo ndiyo jibu la kutufanya sisi tupate hela ndogo? (*Makofi/Kicheko*)

Kabla ya hapo aliniambia kwamba mikoa inayopata fedha ina wahisani. Sasa kama ina wahisani sisi tusiokuwa na wahisani kwani tumewakataa? Kama wao wametukataa mhisani wetu sisi ni Serikali ya CCM. Sasa kama walivyosema Wabunge waliotangulia ninaona ni ajabu kwamba unaona Mkoa una wahisani, unapewa fedha nyingi halafu na Serikali yetu nayo inawaongezea kitita zaidi ya Mkoa usiokuwa na wahisani.

Sasa hapa tunashangaa kwa kweli. Sasa hapo ndiyo tunapokuja kusema kama alivyosema ndugu yangu, basi ingawa tuna madini tupeni basi *royalty* na lenyewe kosa. Tukisema hilo nalo kosa sasa tufanye nini? Ukitisema wanasesma hivi ameng'ang'anisa *royalty* utasemaje? Huwa tunasema hivyo hivyo, ukweli unapokuwepo unasesma ule ule, huwezi ukaenda msikitini ukaanza kusali vingine utasafiri Bismilah Rahman Rahim. (*Makofi/Kicheko*)

Ukienda Kanisani utasema kwa Jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu. Wala huwezi kugeuza ukasema leo tutaanza Ibada kwa jina la la shangazi na la mjomba, huwezi. Sisi tutazidi kuomba kwa sababu inatia huzuni sana. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, atakayeanza mchana atakuwa ni Mheshimiwa Mohamed Missanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Halimenshi Mayonga.

(*Saa 7.00 Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia*)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, naomba radhi sauti yangu leo sio nzuri. Lakini pili nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia ili na mimi nichangie kwa shabaha ya kujazia nyama katika hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ndio mara ya kwanza kuzungumza, nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wabunge wenzetu wote waliojiunga na sisi katika kipindi hiki hasa wale wa Chama cha Mapinduzi na wenzetu Wazanzibar kwa sababu wametuhakikishia kwamba hapa Maruhani hakuna. Lakini tahadhari yangu ni kwamba, inawezekana Marohani hakuna lakini Subiani wapo. Kwa hiyo kama Subiani wapo, basi mambo ni yale yale. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya kina, yenyé maelezo mazuri ya utekelezaji na mwelekeo wa huko tunakokwenda. Nampongeza ye ye pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wawili walioko katika Ofisi yake na Katibu Mkuu wake na wote wale ambao kwa kweli wanamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Ofisi yake kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa masikitiko. Kwa ruhusa yako naomba nitumie nafasi hii kutoa rambirambi kwa wapigakura wangu wawili wa Tarafa ya Sepuka kwenye Kijiji kinachoitwa Ighombwe. Kwa mujibu wa gazeti la Mwananchi la jana linaleza kwamba wananchi wawili wameuawa na tembo kule Ighombwe Singida. Kwa hiyo kwa ruhusa yako naomba nitumie nafasi hii kutoa rambirambi zangu kwao na kuwaomba wafanye subira na inshallah Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu Peponi.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile niseme, katika eneo hili la Ighombwe ambalo ni Kata ya Mwaru na Tarafa ya Sifuka na Tarafa nyingine kule Ikungi Kata ya Isuna tembo wako wengi sana na mara kwa mara wamekuwa wakitishia usalama na maisha ya wananchi wa Singida. Sasa hapa niombe Serikali iwe inachukua hatua za haraka pale

wanapoambiwa kwamba pana wanyama waharibifu kama hao tembo ili kunusuru wananchi.

WABUNGE FULANI: Ndovu.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Ndovu eeh! Nashukuru sana. Hata huyu mwandishi naye kama mimi kaandika tembo badala ya kuandika ndovu. Naomba Serikali iwe inachukua hatua za haraka pale wanapopata taarifa kwamba kuna wanyama waharibifu kama ndovu ili kuokoa maisha ya watu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ni mara nyindi taarifa zimekuja lakini hatua za haraka hazikuchukuliwa. Pia jambo lingine pale kwenye Wilaya yangu, upo upungufu mkubwa wa Askari wa Wanyamapiro. Kwa kumbukumbu nilizonazo mimi wapo wawili tu ambao kwa kweli hawatoshi. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu isaidie kulifatilia hili kutoka kwa Ofisi zinazohusika ili angalau Askari hawa waweze kuongezwa kwa ajili ya kunusuru maisha ya watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ukurasa wa 63 kifungu Na.71 anazungumzia habari ya upungufu wa chakula. Ni kweli kabisa nchi yetu imepata matatizo ya upungufu wa mvua na kwa hali hiyo upungufu wa chakula, na sisi watu wa Singida ni mionganoni mwa hao ambao tumepungukiwa chakula. Kwa mujibu wa takwimu za mwanzo mwanzo, zinaweza zikasahihishwa baadaye wakati naondoka, sisi tunahitaji tani zisizopungua 38,000 ili zitusaidie. Nasema ni takwimu za mwanzo mwanzo zinaweza zikarekebishwa baadaye, lakini wakati naondoka mahitaji ya upungufu ni tani 38,000.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hapo kwamba kimsingi Mkoa wa Singida na Wilaya ya Singida ni Wilaya na Mkoa ambao unajilisha wenyewe, labda tupate matatizo kama vile *El-Nino* na haya ya mwaka huu. Lakini kama hali ni nzuri sisi tunajilisha. Mwaka huu hali imekuwa mbaya zaidi kwa sababu ya tatizo la ndege waharibifu. Wamekula chakula kingi sana na hili tatizo sasa linakuwa sugu. Mwishoni mwa mwezi Desemba nimekwenda Ofisini kwa Mheshimiwa Keenja nikawaeleza tatizo hili, Januari mwanzoni nimekwenda tena akanipeleka kwa wataalam wake nikamweleza tatizo hili wakasema wanlishughulikia. Lakini hawakulishughulikia, ndege wameendelea kuharibu chakula mpaka mwezi Mei ndio ndege ilipelekwa kushambulia kweleakwelea. Sasa jiulize toka Januari, Februari, Machi, Aprili, hakuna hatua zilizochukuliwa mpaka mwezi Mei, hivi kweli unategemea wananchi watasema nini? Wananchi hawaelewii! Kwa hiyo, hili linanisikitisha sana na mimi namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli angalau tupate majibu mazuri, vinginevyo kule iko chuki kubwa sana kati ya wananchi na Serikali yao kwa sababu ya kushindwa kupeleka ndege za kuangamiza ndege waharibifu katika wakati unaostahili. (*Makofi*)

Sasa la pili, wako ndege wengine wanaitwa kasuku. Sisi kule nyumbani tunawaita silingu kwa lugha ya kwetu. Hao ndio wameangamiza zaidi chakula. Kwa sababu mpaka naondoka Singida, hajjatolewa idhini kwa sababu inasemekana hawa ni raslimali na kwamba hawawezi wakauwawa mpaka Wizara ya Maliasili na Utalii itoe kibali.

Mpaka naondoka Singida kibali hakijatolewa. Sasa wananchi wanauliza raslimali ndege na raslimali watu ipi bora watu wasifike mahali waamini kwamba Serikali inajali sana raslimali ndege kulikoni raslimali watu? Hilo ni jambo la kusikitisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wanasesma mnatuhimiza kulima, tunalima mazao ya biashara na mazao ya chakula, tunawaambieni ndege wapo hamji, sasa sisi hatulimi na wala msije kutuambia habari ya kulima. Sasa hivi ukienda kwenye ziara wanakwambia umekuja kusemajie? Umetuletea ndege au umekuja kwa dhununi la ndege? Hawataki kusikia habari nyingine! Wanataka kusikia habari ya ndege kuja kuangamiza ndege waharibifu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anahitimisha hoja yake basi alitolee maelezo kwani ni jambo la kusikitisha kwamba taarifa nimetoa toka mwezi Desemba, lakini mpaka mwezi Mei ndio ndege inaua kweleakwelea. Mpaka naondoka Jimboni hakuna kibali kilichotolewa kwa ajili ya kuua hawa kasuku. Sasa tuambiwe, kama raslimali ndege ni bora, basi wananchi wa Singida na hata tarafa hiyo ya Sipuka wajue kwamba raslimali ndege ni bora kulikoni raslimali watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo, nataka niseme tu kwamba kufuatia matatizo ya kazi kwa ajira ya vijana na kwa sababu Sekondari ndio hizo chache, wanafunzi wa Darasa la Saba hawaendi kwa kutosheleza, tegemeo letu ni *VETA*. Singida hatuna *VETA*. Mikoa mingine kadha wa kadha wana *VETA* nzuri tu, majengo mazuri na Ufundii mzuri, vijana wanasonmeshwa. Hivi Singida tuna matatizo gani sisi? Tatizo la ajira lipo kama Mikoa mingine. Kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aelekeze kwa wale wanaohusika ili angalau na sisi tupate *VETA* kama sehemu nyingine ili vijana wa Singida wanaomaliza Darasa la Saba na vijana wengine wanamaliza hata *Form Four* nao wapate kujiendeleza kwa sababu ya kukidhi tatizo hili la ajira.

Lingine ni kwamba kuna kitu kinaitwa Kanda. Makao Makuu ya Kanda, hivi sisi Singida mbona hatuna hata Makao Makuu moja ya Kanda? Sisi mara tumewekwa Arusha, mara tumewekwa Dodoma, mara tumewekwa Tanga, hivi Singida sisi tuna matatizo gani hata Kanda moja hatuna? Hivi kweli inakujia akilini Singida iwekwe katika Kanda ambayo Makao Makuu yake iwe Tanga kwa Wagosi wa Kaya hiyo Sawasawa? (*Kicheko/Makofi*)

Haiwezekani! Sasa nasema hili kwa kweli linatusononesha kana kwamba sisi Singida si chochote! Maadam sasa kuna Mkoa wa Manyara, mimi nilitegemea kwamba walau Manyara, Dodoma, Singida itakuwa Kanda na Makao Makuu itakuwa Mkoa wa Singida. Eeh, mambo namna hiyo angalau yatakuja kuja tu! Lakini kila siku mara Arusha, mara sijui Dodoma, mara Tanga, mara wapi hali hiyo inatia kichefuchefu. Ningeara sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie suala hilo. (*Makofi*)

Niishukuru Serikali na hapa namshukuru sana Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa kututengea Shilingi milioni 100 kwa ajili ya uwanja wa ndege wa Singida. Naomba sana, sisi wenzenu hatuna Uwanja kiasi kwamba hata Waziri Mkuu

ukija kule utembee na gari, huchoki? Wewe mwenyewe huoni hiyo? Tunakuonea huruma sisi! Hivi tunamtegemea Mheshimiwa Rais aje atutembelee, mtamtembeza na gari wee, mpaka achoke. Hivi jamani na sisi tusaidieni tupate uwanja wa ndege angalau Rais aone hamu ya kuja kwani, hajaja Singida toka mwaka 2000. Moja ya sababu ni kwamba hakuna uwanja wa ndege ndio maana hajaja. Ingawa magari yapo lakini nadhani kama ndege ingekuwepo angefanya ucharaka kuja. Kwa hiyo, nashukuru kwa kiasi kilichotolewa, lakini naomba mwakani tupate kingi zaidi ili kusudi tupate uwanja wa ndege.

Kwa niaba ya wapigakura wangu, nashukuru kodi ya maendeleo imeondolewa, lakini swalı langu ni kwamba lile pengo linajazwaje? Ni busara kuondoa baadhi ya shughuli ili zifanywe na Serikali Kuu? Kwa mfano barabara za Vijijini kwa mujibu wa utaratibu zinatengenezwa na Halmashauri ya Wilaya. Sasa hivi hali zao za fedha ni dhoofulhal. Je, si vizuri sasa Serikali Kuu au Tanroad wakachukua jukumu la kutengeneza barabara za Vijijini na kadhalika? Naomba hilo nalo lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka jana Mheshimiwa Mramba alisema amepunguza asilimia 50 ya heavy furnace oil (12.8) kutoka Sh.26.50 mpaka Sh.13,050 ili kupunguza *production costs* kwa ajili ya viwanda. Je, imefanyika hivyo? Lakini Singida mwaka jana tulikuwa tunanunua cement Sh.7,500/=, hivi sasa tunanunua Sh.8,000=/. Pale *Wazo Hill* ukienda *cement* ilikuwa Sh.7,280/= mwaka 2001, Sh.5,808/= mwaka 2002, hivi sasa ni Sh.6,540=/. Swalı langu, huu msamaha uliotolewa umewasaidia vipi wananchi? Au ni kiini macho ambapo tunapigwapiwa hapa tu kwamba tunafanya hivi, tunafanya hivi! Ningependa maelezo ya kusema msaada huu umewasaidia namna gani wananchi katika suala hili la umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la wastaifu kwamba kima cha chini ni Sh. 20,000/= lakini hazitoshi. Nasema alhamdulillah tumepata, lakini lengo liwe kutoa pensheni inayolingana na kima cha chini, ndio wenzetu wanavyofanya. Sasa ni ombi langu kwamba huko mbele tunakokwenda au siku za usoni tunakokwenda, basi ni vema pensheni ilingane na kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Spika, lingine ni lile ambalo wenzangu wamelizungumza wale waliochukua mkupuo na bado wapo hai. Naomba sana hawa watu tusiwaue kabla ya siku zao, hebu na wao tuwaingize katika utaratibu wa kulipwa pensheni. Maadamu sasa utaratibu wa mkupuo umekwisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho kinasikitisha zaidi ni kwamba katika *PPF* watu waliostaifu au kuwa retrenched, wame-*qualify* kwa mujibu wa taratibu na sheria wakaanza kulipwa pensheni, halafu marekebisho ya juzi ya sheria ya *PPF* yamekuja kuwafanya watu hawa pensheni yao isitishwe. Hiyo ni kuwanyima haki. Mimi nimesha-*qualify* nikapata haki yangu, leo unababilisha sheria inaanza kule nyuma. Sheria inaanza with *immediate effect*. Mimi sioni kwa nini hawa watu walikuwa wanapata pensheni yao, halafu leo uwanyime pensheni yao eti kwa sababu ya sheria hii wakati walisha-*qualify*, walikwishaitumikia na wakafika mahali kwamba wanastahili. Hii ni utovu wa haki za kibinaadamu kwa sababu haki za wafanyakazi ni haki za kibinadamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko makubwa sana kwa wastaaafu na viongozi wastaaafu. Ndugu zangu, viongozi wetu wale wa zamani kwa mujibu wa Azimio la Arusha wamestaafu hawana kitu. Dhoofulhal taaban unamkuta Mheshimiwa aliyekuwa Waziri, sijui alikuwa Jaji, anatembea na kandambili. Hivi hii hali nzuri? Sasa lalamiko lao ni kwamba wametupwa, wamesahauliwa, wala hatuwajali, wala hatuwafikirii chochote!

Mheshimiwa Spika, hii inasikitisha sana. Na sisi tutastaafu na nyinyi huko mbele mtastaafu, hivi mtataka kesho tuwaone mnatembea na kandambili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningekuomba sana kwa kweli, ni vizuri kuwa na Benki ya wastaaafu ambayo tunawaangalia lakini vile vile wanaweza wakasaidia kukidhi mahitaji pale penye upungufu, utaalamu wa Madaktari, Walimu na wengine wengine kama Majaji au Mahakimu na kadhalika. Sasa kwa kweli suala la kuwalea wenzetu ambao tumeefanya nao kazi vizuri, wameitoa nchi hii huko inakotoka mpaka hapa, sisi tumeikuta iko hapa kwa sababu imetengenezwa. Kama sio kazi nzuri waliofanya wale sisi tusingeikuta katika hali hii. Naomba sana hili Serikali iliangularie tuwalee viongozi wetu waliofanya kazi nzuri na wameacha kazi vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ilikuwa kengele ya pili. Nitamwita Mheshimiwa Mayonga lakini baada yake atafuata Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na wajiandae Mheshimiwa Karim Said Othman na Mheshimiwa Salim Omar Ali. Mheshimiwa Halimenshi Mayonga.

MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuongeza machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabla sijaenda mbali naunga mkono hotuba yake nzuri na yenye kupendeza.

Mheshimiwa Spika, ninayo mambo mawili. Mengine yatakuwepo tu, lakini makubwa ni mawili yale ambayo wameongea Waheshimiwa Wabunge. Kwanza niwapongeze wale Wabunge ambao wamechaguliwa kwenye Majimbo yao, nawakaribisha sana. Huu ndio Ukumbi wetu wa kutafuta maendeleo kwenye Majimbo yetu. Wote tu mlionchaguliwa bila kubagua Chama, wote tu ni halali na mimi ni rafiki yenu mzuri tu. Kwa hiyo nawatakia maisha marefu muendelee kushinda. Vurugu ndio zipungue tu, vurugu ziendelee kupungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba tu kusema tangu mwaka 1991 mpaka 1995 nimeongea hayo hayo, Bunge lile la Dar es Salaam, mwaka 2000 haya haya, hiki kipindi cha tatu naongea hayo hayo, mpaka lini? Leo tunamalizia haya mambo namna gani?

Naomba suala hili la umeme Mkoani Kigoma lipate sasa suluhi. Yaani mimi siji kuomba kura tena nije kipindi cha nne! Kuomba tena Ubunge kipindi cha nne hakuna umeme Mkoani Kigoma, haiwezekani! Hii ni burudani isiyoelewka! (*Kicheko*)

Maswali mengi ya Waheshimiwa Wabunge humu yanapojobiwa unakuta kabisa yanakwenda mpaka kwenye Vitongoji, hivi Serikali inapata wazo sahihi la namna gani unapopeleka umeme wa kudumu kwenye kitongoji wakati Mkoa mwingine bado wanawasha ma-chimney? (*Makofi*)

Juzi Waziri Mkuu alikuja ndio ilibidi yaletwe yale ya pu-pu-pu-pu, yaani tumekaa tumeweka ma-watchman ili isizime Waziri Mkuu asilale gizani. Alipoondoka giza sasa limerudi kutawala. Namshukuru kwamba alitusikiliza Wabunge wa Mkoa wa Kigoma bila kujali Vyama. Alituita wote tuliokuwepo. Lakini sisi tulisema hivi, tumwambie hoja moja.

Pamoja na matatizo mengine yaliyopo, tumwambie agenda moja tu ya umeme wa kudumu. Sasa mbona mnaturepeleka Burundi? Sisi sio Warundi bwana! Mbona mnaturepeleka Kongo? Sisi sio Wakongo, ni Watanzania, tupeni umeme sasa wa kudumu. Kama Serikali haiwezekani kuupata tuambieni tu yaani jibu liwe zuri kwamba bwana Kigoma kaeni tu umeme haupo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikwenda Karatu nikakuta umeme wametandika mpaka porini kule. Mradi wa maji umekwenda mpaka Vijijini, mpaka porini kabisa. Sasa leo kama Dr. Slaa alikuwa hajawa Mbunge umeme umekwenda na maji yamekwenda, upinzani wa kumwondo huyo Mbunge unaanza wapi? Huyo huyo! Tena nilipokwenda ndio akatupeleka na kwenye hoteli nzuri, mimi Mbunge wa CCM ananiambia unanikwepea wapi? Mayonga umeme huu hapa na maji haya hapa. (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Anakutambia!

MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA: Ananitambia. (*Kicheko*)

Sasa jibu kwa Mkoa wa Kigoma ambao ni Mkoa mionganoni mwa Mikoa ya kwanza ambayo ilitambuliwa na Wakoloni na Mkoa wa Kigoma umo. Sasa unatambuliwa na Mjerumani tu, wala hata Muingereza hakuutambua.

Sasa Serikali yetu hii miaka 40, kigezo ni nini? Mimi naomba hilo tu. Yaani nikisema nieleze mambo mengi, mengine tume faulu. Sekondari tumejenga zinatosha, nzuri tu na tunamshukuru Waziri wa Elimu, nyingine ametufungulia na juhudhi nyingine ameturuhusu, hiyo hatua tunakubaliana ni nzuri.

Sasa huu umeme alikuwepo Waziri sio Majogo, Waziri wa Mambo ya Nje Jakaya Kikwete. Tumeongea naye na Warundi na Wakalimani akina Ntagazwa; ukalimani Kirundi kupeleka kwenye Kiswahili hapa hapa Dodoma. (*Kicheko*)

Amekuja Majogo hapa hapa Dodoma, amekuja Yona hapa hapa Dodoma, sasa hivi tunatumia ukalimani wa namna gani kupata umeme Mkoa wa Kigoma? (*Kicheko/Makofi*)

Tunaomba sasa hivi hii agenda kweli ni *critical issue* ambayo ni *unsolved*, sasa ni *much better we solved* tutapendeza. Sisi pia ni sehemu na wala haiwezekani kwamba wapinzani sasa hivi waje waseme unaona miaka yote ile 40 hamna umeme? Shughuli pale haziendelei kwa sababu ya umeme.

Jamani, naomba hili tulitazame kwa macho mawili kwamba ni muhimu na inahitajika haraka iwezekanavyo kabla ya uchaguzi wa mwaka kesho kutwa. Yaani mwaka kesho kutwa 2005 tunamwelezaje Rais? Maana Rais wa Kwanza sawa, tulikuwa tunatafuta uhuru.

Rais wa pili, ilikuwa ni kwa ajili ya maendeleo nayo ndio hayo na yeye mwenyewe amekuja ndio risala tumeelezea. Rais wa awamu ya tatu. Sasa anakuja Rais wa awamu ya nne, sasa anakujaje kuomba kura za namna hiyo? Kwa kuanzia namna gani? Hata ziara za viongozi wakubwa Kitaifa akija Kigoma itakuwa siasa yetu, agenda ni ipi? Mkuu wa Mkoa atakuwa anajiumauma tuanze namna gani, sijui pale ataanza kuelezea mpango, anamwelezea kitu gani sasa hapa? Hebu elezeni!

Kama umeme unaweza kwenda kwenye Vitongoji na mimi najua umeme umefika kwenye Vitongoji fulani fulani katika nchi hii sitaki kuvitaja, najua na Ushahidi ninao. Tena unakwenda kwa mabilioni basi. Nani anakataa hiyo?

MBUNGE FULANI: Mimi sikatai.

MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA: Sasa unataka kusema kwamba Kigoma sisi tukipata umeme wa kudumu hatuwezi kuzalisha kwa kutumia umeme? Sasa huo Mkoa unabaki ni masikini. Ni makusudi mazima ya Serikali kudhamiria kwamba basi ninyi bakini masikini. Humo humo ndio tumepata zawadi sisi Kitaifa tunatangazwa sasa kwamba Mkoa wa Kigoma ndio unaongoza kwa watu kuzaliana. Ongezeko! Yaani sisi ndio zawadi tumepewa. Sasa, mimi nasikitika sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo kwanza utazame kwamba idadi ya wakimbizi wapatao karibu milioni moja na kuwaweka pamoja, wale watoto wanakuwa ni wengi. Mimi nafikiri wakimbizi watakapokuwa wamerudi kwao inawezekana na sisi tukarudi mahesabu ya kuwa wa kwanza, tukawa wa mwisho.

Sasa hiyo sijui mtalielezaje! Huku tunaonekana ni watu wa kwanza, lakini sababu ya wakimbizi kuwepo pale na kututoa meno kila siku na silaha zao nzito nzito, tunalala kwa hofu. Ndizo shughuli wanazozifanya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, wote walioko pale. Huyo Mkuu wa Mkoa ambaye amekuja Kigoma, kwa sehemu robo tatu anashughulikia maendeleo ya watu wa Kigoma yuko wapi?

Yaani *introduction* ya kwanza ni kukamata bunduki zinazoingia kwenye Ziwa Tanganyika na kutoka Burundi na Rwanda. Zote zinawaangukia watu wa Kigoma, zinawaatamia, wanalala roho kichwani hata mimi nikiwemo. Leo kukicha nasema la, leo Mungu amenisaidia kweli! Kila Waziri anapokuja salamu ya kwanza ni kumpeleka kuangalia zile silaha zilizolundikwa kama mihogo. Jamani hilo nalo sio tatizo? Sasa tunalimaliza namna gani? (*Makofi*)

Mimi naiomba Serikali katika hili la wakimbizi, tushinikize Serikali zao za Burundi na Kongo ziweze kufikia hatua sasa na zilitambue kwamba ugomvi wa kisiasa ufikie mwisho. Wale wanaokimbia hawana hatia kwa sababu wanakimbia na watoto. Hawana hatia na kwamba kwa kuendelea kufanya hivyo, basi ni mauti yetu sisi Kigoma. Watu wetu wengi wamepoteza maisha kwa sababu ya wakimbizi. Sisi hapa ni wakimbizi? Naomba hili Serikali ilitazame. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili nataka kumjulisha Mheshimiwa Waziri Mkuu ajue hili, kwamba tunapata abiria mara mbili kwa wiki kwa treni na idadi ya abiria hao ni wale wanaolingana na mabasi mawili kwa wiki nzima. Katika nchi hii, hivi wewe unataka kusema kwamba watu wanaotoka Mkoa wa Mbeya, Arusha, Mwanza pale barabara inaweza ikapita ni basi mbili tu? Haya maendeleo yanaweza kupatikana wapi kwa watu hao?

Sasa kigezo kikubwa kinachosababisha, tunategemea treni tu na treni ina behewa moja la *third class* na baada ya ajali hii ilivyokuwa baada ya Mkurugenzi aliyekuwepo kupunguza iwe kiasi, lakini ajali ya haya mabehewa yaliyoharibika hayana *replacement*.

Uwezo wa Shirika kununua mengine unahitaji nguvu ya Serikali pengine kwa kuokoa hilo jahazi. Tuna watoto wengi wa Shule za Msingi wanaosomea Mikoani. Ni mlundikano mpaka hapa. Yaani kila siku nakwenda kugombana na *Station Master* hapa, ndio maana huwa nakuja nimechelewa. Naamkia stesheni! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, alishawahidi kupata na barua kwa nini nachelewa. Naamkia stesheni kila siku. Hivi hata kesho asubuhi nasafirisha watoto nakwenda kugombana na *Station Master* ndio napunguza abiria ili watoto hawa waliofunga shule wapewe kwanza kipaumbele. *Station Master* hiyo anaijua na nampongeza sana kwamba hilo huwa anatekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Naomba dakika kumi kwa idhini yako (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hiyo ni basi mbili tu. Sasa tunaomba barabara. Barabara ya mkato itakayotoka hapa Dodoma - Singida - Tabora - Urambo - Kigoma itakuwa imemaliza biashara ya lami. Hapo tutakuwa tumekuelewa na tunaomba kabisa ianze sasa hivi wala isichukue muda mrefu. Mwambie Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, mpango huo uwe wa haraka kuanzia dakika hii na shughuli ianze mara moja wala sio kuchukua muda mrefu, wa kazi gani?

Sasa haya mambo ya kuchukua upembuzi yakinifu unachukua miaka mitano, miaka mitano utachukua lini? Kama kuna pesa za ndani ipewe kipaumbele kwanza huko, yaani iwe ni makusudi mazima. Sasa upembuzi yakinifu, sijui bado, wataalamu, usanifu unachukua miaka 20 ndio agenda za kujibu hapo.

Mimi nimeacha kutunga maswali kwa sababu nitajibiwa upembuzi yakinifu, kuna upembuzi, inachukua muda mrefu. Afadhalii hoja hii hapo. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ile reli ilijengwa na Wajerumani. Wajerumani walioikamilisha Vita Kuu ya Kwanza, haiwezekani kwamba sasa hivi katika Karne ya 21 bado tuendelee kutegemea kitu cha namna hiyo. Watanzania wanaotoka Mkoo wa Kigoma, Tabora, Singida wapate wepesi wa kuweza kusafiri katika mazingira mepesi.

Kwanza umbali ule ni mfupi, kutoka Kigoma ni 1,200 mpaka Dar es Salaam bus likitoka Asubuhi. Lakini ukipanda treni ni siku tatu mpaka Dar es Salaam. Huo usafiri unakwenda wapi? Marekani! Yaani msafiri ametoka Kigoma kwenda Dar es Salaam ni safari ya kwenda Marekani kwenda na kurudi! Wewe uliona wapi na hamna chombo kinacho sema basi, kuna uongozi fulani unaofikiria. Tunakwenda tu, tunafika wapi? (*Kicheko*)

Sasa naomba mwone kwamba haya ndio mambo ambayo ni ya kuyafahamu na hatusemi kabisa kwamba tuache wenzetu. Wafanyakazi wengi wanaogopa kwenda huko kwa sababu ni mazingira ambayo ni magumu, hayapitiki. Sasa hiyo barabara itengenezwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, amekosha moyo wangu. Kile kipande cha barabara ya Mwandiga - Manyovu nimekiimba miaka yote, sasa juzi alinipeleka Ofisini kwake akafungua mjadala ule nikaona akaweka na sahihi kwamba itakuwa imekamilika katika miezi minane.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi sitaki kumgusa ndio maana nimepitia kwa Waziri Mkuu, ili asisitize sasa hilo. (*Kicheko/Makofii*)

Pamoja na kumshukuru kwa sababu Waziri Mkuu tuliacha kumpeleka kule, haiwezekani upeleke viongizi sasa hivi mahali ambapo ni pagumu kama ndio adhabu ya kumwonyesha. Hapana. Ndio tulibana na Magufuli.

Sasa Mheshimiwa Waziri Magufuli amejibu zile salamu ni njema na tukuombee maisha marefu uendelee na kazi. Naunga mkono asilimia mia moja kwa mia moja. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofii*)

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya mchana au jioni ya leo ili niweze kuchangia machache ambayo yanatokana na hotuba ya Waziri Mkuu. Kabla ya kuchangia kwanza nimshukuru Waziri Mkuu, kwa hotuba yake pamoja na Mawaziri wake wote wawili na wataalam wake

waliompa ushauri wa kuweka hotuba hii na kuwasilisha Bungeni kama ilivyowasilishwa jana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili, nami napenda kuwapongeza wale Wabunge wa CCM waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni na vile vile nawapongeza Wabunge wa *CUF* waliochaguliwa. Naomba tushirikiane. Kazi ya Ubunge inafanana na CCM na *CUF*. Kwa hiyo, tushirikiane katika kuijenga nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza tu mchango wangu utaelekea moja kwa moja katika ukurasa wa tano katika hotuba ya Waziri Mkuu iliyosema: “Kuondosha au kushirikiana katika hali halisi ya kuondosha kero za Muungano”.

Mheshimiwa Spika, suala hili kwa kweli sasa linawekwa au limewekwa katika sura nzuri ya kuhakikisha kuwa Muungano wetu unaanza kuimarika kwa vipengele ambavyo hivi sasa Serikali zetu mbili zinachukua hatua muafaka na kuhakikisha kuwa baadhi ya kero zinaondoka. Hapo nyuma tulikuwa tunafanya kosa kubwa sana, wananchi wetu walikuwa hawaelezwi mafanikio ambayo yanapatikana baina ya Muungano wetu tulionao. Hili lilikuwa ni kero kwa ambao hawaelewii kinachozungumzwa au kinachofanyika katika Serikali ya Muungano na kushushwa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, walikuwa hawana taarifa yoyote ya mapato au ya matumizi ya pesa ambazo zinatokana na ruzuku au zinatokana na Benki Kuu ya Tanzania. (*Makofî*)

Vile vile ni kama tungewaelimisha mapema nafikiri baadhi ya matatizo yangeliondoka kabla hata baadhi ya mambo hayajatokea au Wapinzani wetu au wale ambao hawatutakii mema kulizungumza katika sura nyingine ambayo kwa kweli inaleta bughudha kwa baadhi ya viongozi wetu. Hili lilikuwa ni suala ambalo lilikuwa lifanywe hapo mwanzo na hivi sasa ndiyo linaendelea.

Lakini hata hivyo, kuna baadhi ya matatizo madogo madogo ambayo yanaweza yakaletwa, yakarekebishiwa kwa kushirikiana kama alivyosema Waziri Mkuu. Kwa mfano, matatizo ya bandari zetu, ukweli bandari zetu zina matatizo madogo madogo ya urasimu. Lakini ni matatizo ambayo yanaweza yakasawazishwa kwa sababu ni vitu ambavyo tunaweza tukashirikiana baina ya Serikali mbili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hili likawa likatatuliwa na suala lingine ambalo kwa kweli hivi sasa haliko katika sura nzuri ni la uvuvi wa Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing*).

Hili kwa kweli lina mgogoro au halikupata maelezo mazuri lilipoanzia. Kwa hiyo kama tutalianza halafu tutarudi na kuangalia tulipolianzia, basi nafiri matatizo madogo madogo yanaweza yakaondoka. Niendelee kusema kwamba, baadhi ya matatizo ambayo yakipata ufumbuzi hivi sasa kwa kweli ushirikiano wetu utakuwa ni mzuri sana na Mungu ajalie uendelee hivi hivi. Lakini kuna baadhi ya mambo lazima tuwe *serious* kuyatekeleza.

Kwa mfano, hivi sasa kwa kweli ukiangalia Zanzibar tangu Muungano wetu ulipoanza mpaka leo kuwa hakuna majengo ya Serikali ya Muungano Zanzibar ni tatizo. Mawaziri wetu wanakuja, wanaishia Serena, Bwawani, humo ndiyo kwenye vikao. Lakini hawana Ofisi ambayo kwa kweli wanaweza wakayazungumzia au kuyajadili matatizo au masuala ya maendeleo kuhusiana na nchi zetu mbili. Kwa hiyo, ilikuwa niseme tu kuwa katika jambo hili, lazima tuwe *serious* kuhakikisha kuwa kuna viwanja ambavyo vimetolewa lakini utaratibu wa kuvijenga viwanja vile haujawekwa hasa na Wizara ambazo zinahusika.

Naishukuru sana Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, wameonyesha moyo ambapo hivi sasa wameshaanza kulipa fidia kwa wenye mazao, ambapo sasa tayari wameshalipa kiasi cha shilingi milioni 20 na baadaye watamalizia shilingi milioni 38, ili kuhakikisha kuwa viwanja vile vinajengwa.

Mheshimiwa Spika, lakini na Bunge vile vile niseme kuwa nalo limo katika utaratibu huu wa kwenda sambamba katika ujenzi wetu. Tushughulikie katika kuhakikisha kuwa Muungano wetu unadumu si kimaneno tu hata kivitendo. Halafu suala lingine hapo hapo kuwa wafanyakazi wa Sekta za Muungano Zanzibar kwa kweli ni wachache na ajira zao zinakuwa ni za matatizo, zinasumbua, zinachukua muda mrefu na hili tumelipigia kelele sana, kwa mfano, suala la uhaniaji. Kwa kweli hili ni suala ambalo inabidi lifanyiwe utaratibu waajiriwe Maafisa Uhaniaji.

Hivi sasa wamefanya *interview* wapo lakini bado hawatoshelezi. Kwa mfano, Mkoa wa Kaskazini kuna Kituo cha Uhaniaji au Ofisi, lakini wafanyakazi waliopo hivi sasa ni wachache. Kati ya wafanyakazi 10 wameongezwa wafanyakazi watatu. Bado halijachukuliwa suala hili kama ni suala ambalo linaweza likaleta ufanisi katika shughuli zetu katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kwa kweli nashukuru sana na naweza kushukuru kwa kuniweka katika Kamati ya Huduma za Jamii. Tumetembelea sehemu nyingi sana kuona hali halisi ya fedha za Serikali zinavyotumika, ambazo zimekuja kwa msaada kwa ajili ya MMEM. Fedha hizi kwa kweli zinasaidia sana na kwa kweli ukiangalia wananchi nafikiri wengine wameelewa lakini wengine bado hawaajaelewa ipasavyo. Kuna matatizo madogo madogo katika pesa au matumizi ya pesa hizi. Kwa mfano, Kamati za Shule bado hazijaelezwa ni nini hasa utaratibu wa pesa hizi. Tulipoangalia sana ukiwaliza maswali kwa kweli yanakuwa hayajibiwi ipasavyo, isipokuwa anayehusika sana ni Katibu wa Kamati, ambaye ni Mwalimu Mkuu wa shule. Kwa hiyo, hili ni tatizo, inaonyesha Mjumbe wa Kamati hajui kinachoendelea katika fedha zile. Fikiria mwananchi ataaelewa nini katika fedha hizo? Niseme kuwa tuhakikishe kuwa fedha hizi zinakwenda lakini bado maelekezo au elimu ya fedha hizi itolewe zaidi kwa wananchi ili kuhakikisha kuwa zinatumika ipasavyo na kuimarisha elimu ya msingi.

Suala lingine ni kuhusu agizo la Waziri Mkuu. Agizo la Waziri Mkuu, anapopita sehemu nyingi sana anaagizia madawati. Lengo la madawati limeeleweka, hadi kufikia 2004 madawati milioni mbili yawe yameshaenea Tanzania nzima. Lakini hivi sasa hata

nusu ya madawati kama hayo bado hayajapatikana. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo kwa kweli lazima livaliwe njuga. Waziri Mkuu anatoa kauli lakini bado utekelezaji wake unakuwa mzito kwa watendaji au wale wanaohusika. Hili pia tumeliona, uchache wa walimu katika shule zetu za msingi bado ni tatizo sugu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine katika hotuba ya Waziri Mkuu, alilolitaja ni kuhusu suala la afya. Utaratibu hivi sasa ambao Wizara ya Afya imeweka ni mzuri sana, wa kufanya mabadiliko ya Sekta ya Afya katika kuimarisha au kuboresha zaidi huduma zake. Imeweka Hospitali za Rufaa, Hospitali za Mikoa, Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Hivi sasa zimebekwa katika mfumo ambao unaweza ukaboresha huduma hizo. Kwa mfano, Hospitali za Rufaa ziachiwe zenyewe, ambapo katika Sheria hii au mabadiliko haya ni kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni na *management* zinaachiwa Hospitali za Rufaa zenyewe.

Lakini tatizo lipo kwani baadhi ya Hospitali za Rufaa zinabeba mzigo mzito kutokana na Hospitali za Mikoa na jambo hili haliwezi kufanikiwa kama hawatashirikiana na Wizara kama TAMISEMI na hili kama watashirikiana ipasavyo, basi tutaziondolea mizigo Hospitali zetu za Rufaa ambazo hivi sasa zinabeba mzigo mzito kutokana na wananchi wengi kukimbilia kwenye Hospitali za Rufaa kuliko kutumia Hospitali za Mikoa au Wilaya au Vituo vya Afya.

Hili tuliliona na kwa maana hiyo, ipo haja TAMISEMI na Wizara ya Afya kulivalia njuga na kuhakikisha hili linafanikiwa. Halafu vile vile suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu Bima ya Afya. Bima ya Afya kwa kweli hivi sasa inaanza kueleweka vizuri na wananchi wengine ambao bado walikuwa na wasiwasi, nafikiri wasi wasi umeondoka kwa kauli ya Rais aliyoitoa katika hotuba yake ya Mei Mosi. Lakini hata hivyo, baadhi ya kauli za Waganga au Madaktari zinawavunja moyo wananchi na suala hili limeachiwa Halmashauri zenyewe kuhakikisha kuwa wale ambao wanatoa kauli chafu wanachukuliwa hatua. Lakini hata hivyo, Wizara ya Afya ichukue bidii na juhudhi kuhakikisha kuwa wale ambao wanaenda kinyume na kauli za Mheshimiwa Rais, basi wanachukuliwa hatua kali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia liko katika ukurasa wa 43, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumzia kuwa kuzifanyia ukarabati Shule za Ufundı kwa mfano, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam. Vyuo hivi kwa kweli zinahitaji ukarabati wa hali ya juu. Kwa mfano, tulitembelea Dar es Salaam Chuo cha Ufundı kile kwa kweli kina hali ngumu. Majengo ya 57 mpaka leo bado hajafanyiwa ukarabati hata mara moja. Fedha ambayo inahitajika ni fedha ya ufadhili kutoka nje ndiyo ifanye ukarabati pale. Hili ni tatizo sugu ambalo tuliliona na kama hautafanywa ukarabati Chuo kile kinavuja na maendeleo yake kwa kweli hivi sasa ni duni sana, kama hakuna ufuutiliaji wa aina yoyote kinaweza Chuo kile kikawa hakina maendeleo mazuri katika utoaji wa taaluma.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kipindi kilichopita kuhusu Chuo cha Waandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma, kiliwekwa katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam. Lakini Chuo hiki kwa kwa

kweli kinatoa taaluma nzuri na kinaleta ufanisi kwa Waandishi lakini kina upungufu wa miundombinu. Mfano, Chuo kile hivi sasa hakina mabweni, hakina usafiri, hakina vifaa vya kutosha. Kwa hiyo, naomba liangaliwe suala hili na kisha kile Chuo kifanyiwe marekebisho au kipatiwe huduma kama hizi ili kitoe Waandishi ambao watakuwa na taaluma ya uandishi kuliko hivi sasa ambavyo wanafanyakazi kwa kubahatisha tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu, mia kwa mia. Namaliza kwa kukushukuru nasema ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. KARIM SAID OTHMAN: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, nakupongeza kwa kunipa nafasi, la pili ni uungwana na ni ustaarabu kupongezana. Mimi binafsi kwa niaba ya wenzangu, nawapongeza Wabunge wa CCM walioingia katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashangaa sana kusikia kiongozi mwanasiasa mahiri anasema kwamba, hawezi kutupongeza sisi. Ni jambo la kushangaza sana, kwa sababu sisi tumekuja hapa kwa mlango mwingine ambao mmeufungua ninyi. (*Makofi*)

Watoto wenu, hamuwezi kutupongeza! Kwa hiyo, hapa naona kuna kasoro ya uungwana kidogo. Halafu la pili, ni kwamba, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuleta jedwali katika kitabu chake hiki ukurasa wa 82 linaloonyesha matokeo ya chaguzi ndogo za Wabunge. Napenda kuanzia namba tano mpaka 19. Muone jinsi namna tulivyoingia humu. Hii ni alama ya kwamba, sisi tayari tumemaliza kazi nyumbani huko. (*Makofi*)

CCM wamekosa hata *deposit* zao. Sasa kwa sababu nyumbani hatuna kazi, Mheshimiwa Mbunge wa Sikonge, itabidi sasa kazi tuifanye huko, tutaanza Hanang na tutafika Sikonge. (*Makofi*)

Usiwe na wasi wasi, sisi tunakuja tumemaliza kwetu. Sasa ni lazima tukipande chama chetu Bara na tutaanzia huko. (*Makofi*)

La pili, Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri Mkuu kwa hatua yake. Katika suala la Muungano, Waziri Mkuu ameona kwamba, kweli Muungano una kasoro na una kero ambazo zinawakera wananchi na sasa hivi Watanzania wameanza kutambua haki zao. Sio wajinga tena. Yote ambayo mnayafanya sasa hivi, ni kupaka mafuta kwa mgongo wa chupa. (*Makofi*)

Suluhisho la matatizo ya Muungano, ni kuwa na Serikali tatu, hakuna lingine. Tembeeni kushoto na kulia, Kaskazini na Magharibi lakini tatizo la kero za Muungano ni kuwa na Serikali tatu pekee. Serikali ya Zanzibar, Serikali ya Muungano, Serikali ya Tanganyika. Hilo pekee ndiyo tatizo la Muungano litamalizika. Wanaosema kwamba ni kuvunja, siyo kuvunja. Muungano una maana na una umuhimu. Leo ukija huku kuna nchi ndogo, inataka kuimeza nchi ndogo. Wazanzibari wanatuonea, sijui Zanzibar

wanatutegemea. Malalamiko haya yataondoka, kwa kuunda Tume ya pamoja ya fedha, si suluhisho la kero ya Muungano. (*Makofi*)

La pili, Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri Mkuu, kwa kuona tena sana kwamba, kuna umuhimu sasa Chama Cha Mapinduzi kuanza kufahamu demokrasia, ndiyo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, yuko tayari kuanzisha Daftari la Wapiga Kura na yuko tayari, Serikali kupoteza shilingi bilioni 3 kwa Daftari la Wapiga Kura! Mimi nampongeza ni hatua nzuri sana. Lakini kwa nini kitu au suala ambalo halihitaji hata shilingi moja lisitumiwe, kwa mfano, kuunda Tume Huru ya Uchaguzi, ambayo itakuwa na Wajumbe wa Upinzani na Chama kinachotawala, kuna shida gani hata hii Tume isiundwe? Shilingi bilioni 3 zitatumika kwa kutayarisha Daftari la Wapiga Kura ili kujitayarisha katika uchaguzi ulio na haki. Lakini Tume Huru ya Uchaguzi kwa nini isiundwe?

Vyama 15 vinavyoingia katika uchaguzi, Watanzania wawe tayari kuamuliwa matokeo ya uchaguzi, Tume ya Uchaguzi ya chama kimoja, hii ni haki? Mimi naiomba Serikali na namwomba Mheshimiwa Rais, Rais wetu ni mzuri, ni msikivu, ni mahiri, mwambieni hili kwamba, sisi tunamwomba aunde Tume ya Uchaguzi mara moja. Hii haihitaji hata shilingi moja. Abadilishe Tume hii. (*Makofi*)

Baadaye lifuatane pamoja na Daftari la Wapiga Kura, ili Watanzania wawe na haki ya kuchagua viongozi wao wanaowapenda wenyewe. Masuala yote ya uchaguzi ya nchi hii yawe chini ya Tume ya Uchaguzi. Kusiwe na mfano labda *DEDS*, sijui nani hawa, Maafisa Tawala wa Mikoa na Wilaya, ambapo hutakuwa wewe Afisa Tawala wa Mikoa au Wilaya, kama hujawa mkereketwa wa CCM na ye ye huyu ndiye *Returning Officer* wa chaguzi zetu, mnatupeleka wapi? Kwa hiyo, hili tunalisema kwa upana. (*Makofi*)

Narudia tena kwamba, Watanzania hili hawatalikubali. Watakachokifanya wataingia wapi? Barabarani! Wakiingia barabarani mtakayoyafanya mwayajua. Nawahakikishia kwamba, Shimoni safari hii hatuendi peke yetu. Kama ni kwenda Shimoni tutakwenda sote. Lakini Watanzania wataingia barabarani kwa hili. Kwa hiyo, si tabia nzuri hata kidogo. Namwomba Waziri Mkuu, kupitia kwako Mheshimiwa Spika, amwambie Mtukufu Rais kwamba, ajitahidi Tume ya Uchaguzi iende sambamba na Daftari la Wapiga Kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la habari. Vyombo vya habari jamani naomba viwe huru. Viwe na uwezo wa kutangaza yale ambayo wanayo. Gazeti sasa hivi, kama halizungumzii vizuri CCM linaambiwa hilo si gazeti. Serikali inatafuta vigezo kuwaambia Mhariri wake huyu si raia, mara sijui vipi, kwa sababu gazeti lake linatoa mambo ya kweli ya kuipinga CCM. (*Makofi*)

Juzi juzi hapa, kuna gazeti la Dira liliambiwa Mhariri wake kwamba yeye si raia. Mtu aliyewahi mpaka kuwa Katibu wa Kiongozi Mkubwa Serikalini, hamkujuu tu kwamba si raia? Uraia akose kwa sababu anazungumza ukweli ndani ya gazeti wa kuigonga CCM! Ni aibu. (*Makofî*)

Yaliyompata Jenerali Ulimwengu wa Gazeti la Mtanzania maskini sijui imefikia wapi kwamba yeye si raia? Halafu la pili, Serikali bwana isifanye hivyo, kama sasa hivi hawana uwezo wa kutoa matangazo ya Redio na Televisheni mpaka tupate ufadhili na msaada, basi tuwaruhusu wenyewe uwezo. Sera ya asilimia 25 hii tuiondoe kwa muda. Tuwaachie vyombo hivi vya binafsi kama *Radio One*, *ITV*, mkimruhusu Mengi atatangaza Tanzania nzima kwa siku chache tu. TTV haionekani hapa Dodoma, itaonekana wapi? Kwa hiyo, tunaomba sana kupitia kwako Waziri Mkuu kwamba, Serikali haijakuwa tayari, haijakuwa na uwezo, si vibaya kutokuwa na uwezo, lakini wale ambao wana uwezo ambapo Serikali haitatumia hata senti moja, waruhusiwe, kitu gani mnachokio gopa jamani?

Kama hii sera nilimsikia Waziri mmoja juzi alisema kwamba, sera hii ya vyombo hivi vya matangazo visipewe mtandao wa nchi nzima, ni kwa sababu mmeiga hii kutoka Uingereza. Si mambo yote ya kuiga bwana, kama kuna jambo moja baya ambalo tumeliiga ni hili. (*Makofî*)

Watanzania wana haja ya kujua nchi yao kweli. Hivi leo kuna baadhi ya sehemu hawajui kwamba, Mwalimu Nyerere hatunaye tena duniani, nina hakika na hili. Haya matangazo ambayo Wabunge mnayafanya humu na kuzungumza wapiga kura wenu wasikie, hawasikii. Kwa sababu Redio Tanzania haina uwezo wa kufika huko. Lakini tukubali jamani hili, tukubali kwamba asilimia 25 sasa hivi tuiondoe kwa muda mpaka Serikali itakapokuwa na uwezo.

Kwa hayo machache Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. SALIM OMAR ALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia machache katika Bunge lako hili. Lakini kabla sijasema lolote, kwa heshima kubwa ningependa kutoa pongezi zangu kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Tumbe, kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao wa Jimbo la Tumbe. Haikuwa kazi rahisi kunichagua tu, bali walipima uwezo wangu wa mwaka 1995 hadi 2000. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ningependa kusema kwamba, naipongeza sana hotuba ya Waziri Kivuli katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Hotuba ambayo ilikuwa ni nzuri na ambayo imevutia Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niingie katika sehemu ambayo ilinifanya nisimame mbele yako. Kwanza naomba nizungumzie suala zima la Ugonjwa wa UKIMWI. Sasa hivi Watanzania wengi tuko katika foleni ya kutafuta ajira. Lakini kwa sababu ya uwingi wetu, ajira zimekuwa chache, raia tumekuwa wengi. Lakini tukifumbia

macho suala hili la Ugonjwa wa UKIMWI ambao dawa yake ni kaburi, basi ni dhahiri kwamba, Watanzania tutakodi watu kuja kufanya kazi Tanzania ambapo sasa hivi hatuna ajira.

Kwa hiyo basi, Mheshimiwa Spika, tuchukue tahadhari. La kwanza ni kuziba mianya ambayo ndiyo chanzo cha kusababisha UKIMWI na kwa kweli vyanzo hivi ni kudhibiti mwendo wa akina mama kutembea nusu uchi. Kwa kweli jambo hili linakuwa ni hatari na linakuwa ni sugu, badala yake wanasema wanabakwa, hali ya kuwa wanatamanisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli UKIMWI ni hatari na tayari tumeshaambiwa kwamba, UKIMWI hauna kinga, hauna dawa, wala tiba. Lakini tunaanza kulifumbia macho suala hili, tutaathirika. Sasa mimi napendekeza ya kwamba, kwa sababu Bunge lina uwezo wa kutunga Sheria, tujitungie Sheria sisi Waheshimiwa Wabunge, ukianza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, pamoja na wafanyakazi wetu, twende tukapime UKIMWI, pia badala yake sauti yetu itafika kwa wananchi watatuelewa kwamba, viongozi wetu kweli wako imara wameshapima Ugonjwa huu wa UKIMWI. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la UKIMWI kila mmoja analielewa, mimi nataka niishie hapa, kwa sababu ya wakati. Sasa naomba nizungumzie uchaguzi mdogo, ambao ndiyo ulionifikisha mimi hapa.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi mdogo Rais Mkapa aliusifia. Waziri Mkuu katika hotuba yake pia amesifia. Uchaguzi ulikuwa na waangalizi wa ndani na wa nje, pia wakausifia. Lakini napata matatizo kumsikia Mheshimiwa Mbunge ye yote anasema kwamba, uchaguzi Zanzibar ulikuwa na matatizo hasa Pemba. Sasa ni nani anayeongea ukweli kati ya Rais, Waziri Mkuu na huyu anayesema kwamba, uchaguzi ulikuwa mbaya Zanzibar?

WABUNGE FULANI: Nani Mtikila?

MHE. SALIM OMAR ALI: Mtikila ana nini? Maneno yanatoka Bungeni unasema Mtikila, Mtikila, Mtikila siyo Mbunge? (*Kicheko*)

WABUNGE FULANI: Aseme ni nani? (*Kicheko*)

MHE. SALIM OMAR ALI: Mheshimiwa Spika, juzi tarehe 21 Juni, 2003, tulikuwa na michezo ya Waheshimiwa Wabunge, timu tatu zilicheza kwa wakati mmoja, wewe ukauliza hivi mshindi ni nani, ukaambiwa wote ni washindi, zawadi zikatoka. Tulikuwa na mama hapo nje ya Ukumbi wa Bunge au Viwanja vya Bunge, yule mama alikuwa ni mtangazaji. Alisema kwamba, naomba nimnukuu: “Ukimwona mtu ni mrefu ujue ana kasoro, ukimwona mtu ni mweupe ujue ana kasoro na pia ukimwona mtu anasema sana kutafuta cheo ujue ana kasoro.” (*Kicheko*)

Sasa huyu mtu anayesema uchaguzi Pemba ulikuwa na kasoro basi labda naye tumwelekeze huko. Lakini maneno ya yule mama yeye aliyanukuu kwa mtaalam wa

magonjwa ya akili, ndiko alikoyatoa huko, je na sisi tuelekee huko Waheshimiwa Wabunge?

Mheshimiwa Spika, uchaguzi umekwisha, wapiga kura wetu wanatusikiliza nini tunawatetea katika chombo hiki cha kutunga Sheria, uchaguzi haukuwa na kasoro Pemba, wala haukuwa na mizengwe yoyote. Vyombo nya dola vilifanya shughuli zao baada ya Serikali iliyoundwa na Chama cha Mapinduzi kusema sasa tunataka kufuata Utawala Bora. Sidhani kama walikuwa wanapima, lakini inawezekana ikawa ni mwelekeo wa safari tunayokwenda. Sasa Tumbe waliamua kunichagua mimi, mimi nilipata kura 5,049 kitabu kikaandikwa.

WABUNGE FULANI: Maruhani hayo.

MHE. SALIM OMAR ALI: CCM kura 530 kitabu kikaandikwa na *TLP* ilipata kura 40 kitabu kikaandikwa, sasa uchaguzi ulikuwa mbaya kwa vipi, ultaka kura zangu upewe wewe, aah haiwezekani! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kutokana na wakati mdogo, naomba nizungumzie kuhusu Utawala Bora, ili niunganishe na hili suala la chaguzi ndogo. Utawala Bora ni haki ya nchi na ni haki kwa wananchi wake, kwa hiyo tusiilazimishe demokrasi ifanye nini au tusiwalazimishe wananchi wafanye nini, wakati wa uchaguzi ukifika tuwaacie wananchi waamue wafanye nini, hapo tutakuwa na Utawala Bora na siasa safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano uchaguzi wa mwaka 2000. Mwaka 2000 kwa Zanzibar hakukuwa na uchaguzi, pamoja na kwamba mimi nilitangazwa kuwa Mbunge, lakini hakukuwa na lolote wala chochote. Sisi baada ya hapo tuliamua wenyewe kugomea matokeo, baada ya kuona uchaguzi ulikuwa ni wa mizengwe, uhuni kuzidi na kura zilibiwa zikapelekwa zilikopelekwa, siku mne, tano, hatujui wapi zilipo na wala hatujui wapi zinakohesabiwa. Bunduki zikawa zinalia, sasa sisi tukasema huu si uchaguzi, tukaomba Serikali irudie uchaguzi, Serikali ikasema aah uchaguzi umekwishamalizika. Kwa kufuata utaratibu wa Kikatiba tukaingia barabarani, kilichotokea hapo ni maafa makubwa na majeruhi mengi, hili sote tunalijua. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tulifanya maandamano ya amani na hatukufanya lolote zaidi ya maandamano, lakini hapa kwa kutumia Katiba haikuwezekana. Sasa CCM wakapora viti Mkanyageni akapewa Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na wengine ndiyo wamo humu. Lakini ushahidi mzuri ni huu mwaka 2003, sasa hivi Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, mwakilishi wake anatoka katika Kambi ya Upinzani. Sasa mlilazimisha lazima Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein awe mwakilishi, akashindwa kulilea Jimbo lake ambapo ikatokea bahati mbaya Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein akatakiwa akikalie Kiti cha Umakamu wa Rais. Sasa Watanzania tuijulize, kama Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, alishindwa kulihifadhi Jimbo lake lenye wapiga kura 6,000, hivi atawea kweli kuiongoza Tanzania yenyе jumla ya watu milioni 34? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

SPIKA: Kuhusu utaratibu, kaa chini Mheshimiwa Salim.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anayechangia sasa hivi kwa kweli ametumia majina kwa kejeli, majina anayoyataja Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein huyu ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hakushiriki katika uchaguzi huu anaousema, ni kweli ye ye kashinda lakini hakumshinda Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. Kwa hiyo, ningependa azingatie nidhamu ya nchi hii, amwite Mheshimiwa Makamu wa Rais. Ibara ya 50 inazuia kutumia majina ya viongozi vibaya. (*Makofî*)

SPIKA: Kwa kuzingatia hayo endelea.

MHE. SALIM OMAR ALI: Mheshimiwa Spika, mimi nadhani aliyesema kuhusu utaratibu ni haki yake kusema, lakini nikizungumza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, *Doctor* ni cheo, ingelikuwa labda nimetamka ...

SPIKA: Usifanye ubishi Kiti kinakwambia, sikiliza ushauri uliopewa. Endelea.

MHE. SALIM OMAR ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Sasa naomba nizungumzie kuhusu simu za mkononi. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Spika, simu za mkononi kwa upande wa Zanzibar zinaanza kusikika lakini kwa Pemba bado kuna matatizo makubwa ya simu za mkononi. Kuna hii simu ya mkononi ambayo inaitwa *ZANTEL*, bado haijapata utanuzi wa kujenga minara katika nchi hii ya Tanzania Bara. Sasa tungetaka kujua ni sababu zipi za msingi zinazofanya *ZANTEL* isipate kibali cha kujenga minara yake Tanzania Bara, ambapo Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano? Jambo hili ningeomba Mheshimiwa Waziri, atakapotoa majumuisho ya Waheshimiwa Wabunge anipatie taarifa rasmi kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie hali ya chakula. Hali ya chakula Waheshimiwa Wabunge wengi wamekwishaizungumzia kwamba, kutokana na ukame au kutokana na mvua kutokunyesha kwa wakati, Tanzania inaweza kupata janga la njaa. Lakini mimi nasema kutokana na kiasi cha chakula cha akiba ambacho Serikali imojiandaa kuweka, mimi nasema ni kidogo sana kutokana na ukubwa wa wingi wa watu wenywewe ulivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependekeza Serikali iweke chakula cha ziada angalau kwa asilimia 90 kwa sababu uchumi wetu ndiyo unapanda, basi si tatizo kuweka chakula cha ziada cha namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka nizungumzie chombo hiki cha *TRA*. *TRA* ni chombo muhimu kuwepo kwa sababu kinakusanya mapato, lakini kwa Zanzibar *TRA*

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MHE. SALIM OMAR ALI: Mheshimiwa Spika, naambiwa niunge mkono hoja, lakini kutokana na kutorudia maneno yale yaliyokwisha zungumzwa siwezi. (*Makofi*)

MHE. MARTHA M. WEJJA: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia machache niliyonayo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Ofisi yake, kwa kadri alivyoleta hotuba hii. (*Makofi*)

+

Mheshimiwa Spika, pia naomba nisimsahau Mkuu wangu wa Mkoa, Mzee Makamba, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Mkoa wa Dar es Salaam. Nitashukuru kama na wenzake katika Mikoa mingine wataiga nyayo zake, nafikiri tutakuwa tumepiga hatua kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kuzungumzia kuhusu Idara ya Maelezo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Idara ya Maelezo mimi sikuiona vizuri, katika ukurasa wa 55 amezungumzia habari ya vyombo vyahabari lakini Idara ya Maelezo hakuzungumzia. Ninavyoilewa mimi Idara ya Maelezo ni sawa na chombo muhimu kwa Ofisi yake Mheshimiwa Waziri Mkuu, Idara hii ni mdomo wa Serikali lakini hakuzungumzia. Sasa wakati atakapokuwa ana *wind-up* anieleze Idara hii ameiweka wapi kwa sababu Idara hii hata Mikoani watumishi wake hawana hata vyombo vyahabari ya kufanya kazi, wapo wapo tu, sasa ina maana imefutwa au haitambuliki? Basi tuelezwe kwa sababu hata katika Bajeti mimi sikuiona kama imewekewa Bajeti yake, haina nyenzo kabisa hata katika Mikoa watumishi wapo lakini hawana nyenzo utakuta wanahangaika tu. Sasa mimi nilikuwa nafikiri umefika wakati Ofisi ya Waziri Mkuu waitambue hii Idara ya Maelezo ili tuweze kujua kwa sababu kuna watumishi ndani yake, maslahi yao na jinsi ya utendaji kazi wake. Kwa kweli nitashukuru sana kama atanieleza kwa sababu iko Mikoani lakini haina vitendea kazi, sasa itakuwa ni jina tu la Idara ya Maelezo.

Napenda pia kuzungumzia habari ya Redio Tanzania. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema kwamba, sasa hivi kuna mwelekeo wa kushirikisha hivi vyombo vyahabari. Mimi ninaomba kusema kitu kimoja kwamba, Redio Tanzania kuna mama mmoja, ambaye sasa hivi anakaimu, huyu mama amekaimu kwa muda mrefu sana na kazi yake tumeionta, anaitwa Mama Sanga kama sikosei. Huyu mama amekaimu na bahati nzuri mpaka sasa hivi kazi yake tunaisikia vizuri sana, asubuhi ukitaka kuhakikisha pale Kituo cha Ubungo, msafiri ye yeyote anaweza kutaja kama leo anaondoka, atafika saa ngapi, yote hayo ni matunda ya kazi yake na vipindi vingi tu ambavyo amefanya kama mwanamke na ujasiri wake ameuonyesha.

Sasa mimi ninakuwa na wasiwasi kwamba, huu uunganishaji wa vyombo vya habari, isije ikafika huyu mama akaachwa solemba kwa sababu mtakapounganisha mtaanza kusema ooh huyu mama sijui vipi. Mimi ninaomba kwamba, kama mama huyu amefanya kazi ya ukaimu kwa muda mrefu, apewe haki yake, akumbukwe na mtakapoweka uunganishaji wenu na yeYe asiachwe pembeni, kwa sababu nina hakika kabisa kila mmoja ana hakika naye, mmekwishayaona matunda yake na anafanya kazi vizuri na nina hakika kabisa ya kwamba, amefanya kazi zaidi hata ya wanaume ambao wamekaa katika ulingo wa kazi za Redio Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, naomba pia maslahi ya wafanyakazi wa Redio Tanzania yaangaliwe. Wafanyakazi hao wanafanya kazi katika mazingira magumu lakini taarifa wanazitoa vizuri, sidhani kama kuna tatizo, kila mmoja anayeinuka hapa anaisifia Redio Tanzania, taarifa zake zinavyotoka vizuri. Labda tuombe tu kwamba, waongeze mbinu za kufikisha Mikoani lakini tayari kila Mkoa una mtumishi wa Redio Tanzania anayetupa taarifa zote katika kila Mkoa, sasa tunachotaka zaidi ni kitu gani, nafikiri mtu mzuri ni lazima asifiwe na kizuri husifiwa kwao, sasa tufanye nini? Sisi ndio wenye hicho chombo, sasa ninaomba tafadhali katika sifa hizo, basi na wenyewe tuwakumbuke, Ofisi ya Waziri Mkuu, iwakumbuke ili nao wajisikie na kazi yao waweze kuitenda na kuiendeleza vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuingia katika upande wa kilimo. Katika upande wa kilimo pamoja na Serikali kuonyesha nia yake ya kutia msukumo katika suala la kilimo, kila mwaka inasema kilimo ni uti wa mgongo, mwaka huu imeonyesha vizuri kwamba, kila Mkoa utakuwa na mazao ya kulima ambayo yatakuwa ya biashara. Lakini mimi ningeshauri kwamba, basi kila Wilaya na kila Kijiji pawepo na Mbwana Shamba. Hili suala nilikwishalizungumza hata mara ya kwanza kwamba, Mbwana Shamba hawaonekani katika Vijiji lakini enzi za zamani za uhuru kabla hatujafikia CCM, palikuwepo na Mbwana Shamba na Mbwana Shamba ndiyo wanaoonyesha mifano, wananchi wanaona mashamba ya Mbwana Shamba jinsi wanavyoweka mbolea na jinsi wanavyofanya kila kitu. Sasa leo unahimiza mimi nikalime na ninalima kwa mkono na mbolea yenye inakuja kwa manati, ikisemwa kwamba kuna mbolea mpaka nikiipata mvua zinakuwa zimepita, unategemea nini? Mimi nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, kila sehemu pawepo na Mbwana Shamba ambao wamesomea kazi ya Ubwana Shamba, waweze kuonyesha mfano katika kila Kanda inayohusika na si Kanda tu ila kila maeneo ya Wilaya na ikiwezekana katika Kata.

Mheshimiwa Spika, pia tukumbuke kuwapa nyenzo za kufanya hiyo kazi yao kwa sababu tunaweza kuwa na Bwana Shamba lakini hana nyenzo za kuwatemblea wakulima, basi tutakuwa hatujafanya chochote. Mimi nilikuwa naomba tafadhali tuwape nyenzo za kufanya kazi hao Mbwana Shamba na Bwana Shamba yeyote atakayeonekana kwamba hakutimiza wajibu wake aondolewe na si kuondolewa kwamba ahamishwe labda kutoka Bunda apelekwe sijui Tarime, hapana, kama hafai ni hafai aondolewe na kazi iendelee kwa watu wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo pia ningeomba mbegu ziwe nzuri. Kuna tatizo moja, kuna hasa hizi mbegu za mahindi zinawahi kweli lakini ni ajabu kwamba unapotoa mahindi shambani tayari yana wadudu, dudumizi, sasa sielewi hizi mbegu inakuwaje zinakuwa na wadudu. Mimi ningeomba Wizara inayohusika basi iwe na uchunguzi mzuri wa kuangalia mbegu zinazofaa tuwapelekee wananchi wanapolima ili wasiweze kuwa na matatizo ya chakula wanachokilima, wasipate madhara mapema.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuzungumzia habari ya rushwa. Rushwa imekuwa ikizungumzwa sana, naona karibu kila mmoja anaisifia *TRA* inafanya kazi nzuri. Lakini katika Kitengo hiki cha *TRA* bado mimi naona kwamba, huo mkondo wa rushwa upo kidogo. Sasa mimi nilikuwa naomba pia Serikali ifanye kazi ya kuchunguza, pamoja na kwamba, mimi nimeona mmoja amehamishwa kupelekwa kule sielewi kama amehamishwa kwa sababu ya rushwa au kahamishwa kwa sababu ya kikazi. Lakini kuna chombo kingine ambacho niliwahi kikitaja hata mahali fulani kwamba, kuna mkono tena wa mtu mkubwa, matokeo yake akahamishwa mahali hapo akapelekwa mahali pengine. Sasa kama Mheshimiwa Waziri Mkuu, atahitaji kumjua huyo mtu mimi nitamweleza, sitaki kumtaja hapa halafu niambiwe njieenze. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama atahitaji nitamweleza, nimsaidie ili aweze kufanya hiyo kazi. Maana yake rushwa ni msaada, msaada ni sisi tuwasaidie na ninyi mtusaidie, siyo nimtaje halafu kesho anabaki pale pale, utakuwa haujafanya kitu chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, napenda kuzungumzia habari ya television. Tumejitahidi sana Waheshimiwa Wabunge, kupinga muundo huu wa ndugu zetu wanaotuletea utamaduni wa nje, mavazi mafupi na pia michezo isiyofaa. Mimi naona bado hawajafikia mahali pa kuelewa, maana yake vitendo ninavyoviona ni tofauti kabisa na maadili ya nchi yetu, ninaomba mkazo uendelee. Hata huu uvaaji wa nguo fupi si kwamba ni kwenye mabaa tu, hata kwenye mahoteli, naweza kusema hata mifano. Ni kwamba, juzi nilikuwa kwenye ziara, nilikwenda katika hoteli fulani, nilimkuta msichana mzuri na mrembo lakini alivaa nguo ya ajabu na ni mchana, nikamwambia binti umependeza sana lakini nasikitika nguo uliyovaa usirudi kunihudumia. Mimi sikuridhika nikaenda kumwambia tajiri wake, nikamwuliza hivi unaona kweli huyu nguo aliyovaa ni ya maana sana; je, asipoivaa hii watalii hawataingia hapa? Akasema mama nimekuelewa. Naomba hilo pia tulipige vita kwa ukali na kwa kusaidiana ili nchi iweze kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia habari ya Utawala Bora. Wabunge wenzangu wa upande wa pili, Wabunge wa Upinzani wamezungumza sana, mimi nimesikitishwa sana kuona Mbunge ana Jimbo anaondoka kwenda kwenye Jimbo la mwenzake eti kwa sababu ni la Upinzani, anakwenda kutoa maloloso eti huyu hafai, hapa hamna dhahabu, hamna elimu, hamna sijui nini, hivi kweli wakimfuatilia kwake ni mangapi aliyoyafanya na hata miaka mitano hajamaliza au ni kuharibu jina la mtu, huyo Mheshimiwa Mbunge mwenzie anayemkandia ye ye ana pesa zake mfukoni? Hivi ninyi Wapinzani hamjui ya kwamba, pesa zinatoka kwa utaratibu katika Serikali? Waheshimiwa Wabunge wana pesa? Waheshimiwa Wabunge ndio wanaofanya maajabu? Maana yake ni lazima ujiulize unapokwenda kumkandia Mbunge mwenzako eti kwa sababu ni wa CCM, wewe unayetoka Upinzani umefanya nini? Kama umefanya

maajabu basi una pesa zako za nje ya Bunge hili, ndiyo umefanya lakini si za Serikali. Kwa hiyo, ningewaomba tafadhali sana, bora ukakandie huko kwako lakini siyo kwenye Jimbo la mwenzako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado kuna Mbunge mwingine wa Upinzani akainuka kabisa akasema, CCM inabagua wananchi. CCM sera yake haina ubaguzi wa wananchi, napenda kuwaambia hivyo. Wafanyabiashara wengine wananyanyaswa kwa sababu si wa CCM, ninaomba basi atuthibitishie kwa uhakika kama ni Mbunge kamili na sio Mbunge wa kurashia rashia na kujitia sifa hapa kusema wewe ni Mbunge wa Upinzani, sema ni mfanyabiashara gani aliyeonewa kwa sababu yeye siyo mwana-CCM, tafadhali msiiponde CCM ndiyo imewafikisha hapo ndugu zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia habari ya mikopo. Kuhusu mikopo naishukuru sana Serikali imekumbuka mikopo lakini chombo maalum ambacho kinapaswa kuondoa umaskini katika nchi hii ni vijana pamoja na akina mama. Lakini linalosikitisha ni kwamba, Serikali pamoja na kuweka utaratibu wote wa kupata mikopo, inasahau kuomba au kuzungumza na wahusika wanaotoa mikopo kuhusu kupunguza riba. Riba ni kubwa mno kiasi kwamba, mwananchi anapochukua hii mikopo haimsaidii, hata kama ukichukua milioni nzima unakuta riba yake karibu laki mbili au laki mbili na kitu, wewe sasa unabakia na nini? Mimi nilikuwa naiomba Serikali leo hasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali tafadhali uzungumze na vyombo vinavyohusika ili wapunguze riba. Kama utakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu, humu humu Bungeni nimejaribu kuzungumza habari ya riba na mpaka kuna *NGO* moja ikanikasilikia mpaka kesho kutwa, mpaka taarifa zikanifuata nyumbani ya kwamba, anatuzonga sisi tupunguze riba, mimi sikuizonga *NGO* moja, ninazungumzia *NGOs* zote, hata vyombo vyaya Serikali kama Benki na vyombo vingine ambavyo vinatoa mikopo. Ninaomba mtusaidie riba ipungue, kama mna nia kweli ya kuondoa umaskini, mama zetu wana matatizo, mama zetu wanahitaji mikopo na pia mama zetu wana nguvu, bila wanawake ninyi wote mlioko hapa msingefika hapa jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningeomba kuzungumzia kidogo kuhusu habari ya UKIMWI au nizungumzie habari ya afya. Katika taarifa au katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumzia na ametuonyesha kwamba, kutakuwepo na msaada ambao unatarajiwa hapo baadaye na rutubisho ya waathirika wa UKIMWI kwamba itakuwepo. Mimi naomba basi na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu mmoja amezungumza kwamba, kweli itakuwepo lakini kwa sababu ni vita tunayopigana nayo, basi Serikali iweze kuliangalia upya, virutubisho hivyo vije na kama ni kuuzwa visiuze aghali sana na ikiwezekana basi vitoke kwa bei nafuu au vitolewe bure kwa sababu UKIMWI hauchagui tajiri, maskini, mfupi wala mrefu. Sasa kama utasema uuze labda kopo moja na rutubisho si kwa siku moja, ni kwa maisha ya muathirika. Kwa hiyo, ninaomba basi Serikali iliangalie kwa makini sana ili wahusika waweze kuipata kwa urahisi na waweze kufaidika katika maisha kutokana na matatizo yaliyowakabili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote, nichukue nafasi hii kuwakumbusha ndugu zangu wa Vyama vya Upinzani kwamba, tunapozungumzia Tume Huru ya Uchaguzi, Tume Huru ya Uchaguzi haitoi Wajumbe kadhaa kutoka Chama hiki cha Siasa na Wajumbe kadhaa kutoka chama kingine cha Siasa. Tume Huru ya Uchaguzi wanateuliwa watu ambao kwa kweli wako huru, wanajitegemea, ni *independent* na kwa mujibu wa Sheria zetu anawachagua Mheshimiwa Rais wa nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba niwashauri sana ndugu zangu wa Upinzani kwamba, wajifunze kitu kimoja muhimu sana kutoka Chama cha Mapinduzi kwamba, ukiwa na Chama kichanga, ninyi ni wachache, mnafukuzana fukuzana huko, Wabunge walioko hapa ndani mmewafukuza. Ule muda wa kulumbana unawapotezea Mahakama muda mrefu sana, kila siku ni kesi za Vyama vya Upinzani katika Mahakama zetu na kazi ambazo walitakiwa wazifanye wale Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na wananchi haziendi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii ya dhati kabisa, kuzungumzia habari ya mtoto wa Tanzania na habari ya kijana wa Tanzania. Siku ya Mei Mosi ya 2003 nilikuwa mgeni rasmi katika sherehe za Mei Mosi Wilayani kwangu Singida. Katika ile sherehe niliwatazama vijana mamia kwa mamia wakiwa wanaimba wimbo maarufu ambao kila mtu anaufahamu unaosema, "Tanzania, Tanzania ninakupenda kwa moyo wote na hawa watoto wakiwa wamejaa tabasamu wakasema, tunapokwenda safarini kutazama maajabu ya nchi ya Tanzania, milima na mabonde, biashara na makazi, wakamalizia wakisema Tanzania jina lako ni tamu sana". (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jina la nchi ya Tanzania ni jina tamu sana na sisi kwa pamoja kama Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutalienzi hili jina la Tanzania kwa kuangalia kwa undani na umakini watoto na vijana wa Tanzania. Kwanza, tunatambua wanayo haki ya kupewa elimu, jambo la pili, wanayo haki ya kupatiwa usalama wao wa sasa hivi na haki ya kuwa *guaranteed* usalama wao kwa miaka ijayo na jambo la tatu, hao watoto na vijana wana haki ya kujisikia uzalendo wa nchi yao ya Tanzania. Tangu mwaka 1967 baada ya nchi yetu kuamua kumiliki njia zote kuu za uchumi, matumaini ya kijana Mtanzania yameendelea kuwepo mikononi mwake na mikononi mwa Watanzania wenyewe. Kuna watu ambao dunia itawakumbuka kwa mchango wao kwa vijana, mchango miwili ambayo nitaitoa haikuwa mizuri na mchango mmoja ulikuwa mzuri. Mtu wa kwanza anaitwa Bwana Adolph Hitler. Katika Ujerumanî ya wakati wa vita, Hitler alipoingia madarakani jambo la kwanza alilofanya ni kwamba, alikwenda katika Miji ya Munich, Hamburg, Berlin na katika Mji wa Bonn, akahakikisha ya kwamba vijana wa Ujerumanî ya wakati ule wamehamasika na wamekuwa na uzalendo na matumaini, vijana wote wakamuunga mkono Hitler.

Kwa sababu Hitler aliwathamini sana vijana, pamoja na kwamba nia yake ilikuwa ni ya uovu, alifanikiwa kuua watu milioni sitini katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Kama Hitler angekuwa na nia ya kujenga angweza kujenga maisha ya watu milioni mia moja na ishirini mara mbili ya wale aliowauwa.

Mheshimiwa Spika, miaka ya hivi karibuni, mtu mmoja maarufu sana anaitwa Osama Bin Laden, alianza kutengeneza nyumba katika nchi ya Pakistan. Alichokifanya yeze alienda kwa wale vijana Wamachinga, ambao hawana matumaini kabisa, kwa sababu mtu akikosa matumaini *number one they have nothing to lose*, unaweza kumwambia beba fimbo akabeba lakini akawapenda hawa vijana wa Pakistan baada ya muda kwa mara ya kwanza katika historia ya dunia akafanikiwa. Ni mtu ambaye ameweza kutengeneza watu ambao kwanza yeze aliwapenda akawapa matumaini pili, akawafundisha kuchukia watu wengine duniani, wakachukia kwa machukio makuu halafu wakawa tayari kufa ili watu wengine waweze kufa. Kama Bwana Osama Bin Laden angefanya mambo hayo ya kuwapenda vijana kwa ajili ya matumaini, dunia ingebadilika kwa kiasi kikubwa lakini yote yalikuwa ni vijana. Mtu wa tatu hawamsemi sana lakini wanamwita *Mother Theresa*. Katika maisha yake alisema neno moja ambalo litakumbukwa na dunia nzima, aliwaambia hatuwezi kufanya makubwa sana katika maisha yetu kama wanadamu lakini tunaweza kufanya mambo madogo kwa upendo mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa tulilonalo nchi hii ni vijana wengi ambao tusipoangalia namna ya kuwasaidia watakuwa *time bomb* hata kama tungefumba macho. Vijana wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walio barabarani wengi hawana matumaini ya kazi. Sisi kwa pamoja ni lazima tuangalie ni kitu gani tutakifanya kuweka matumaini ndani ya maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, takwimu za hivi karibuni zinasema asilimia 32 ya wanafunzi wanaomaliza Shule za Msingi katika Jamhuri ya Kenya walikwenda Sekondari, asilimia 24 ya wale waliomaliza Uganda walikwenda Sekondari, asilimia 18 ya wale waliomaliza Malawi walikwenda Sekondari na asilimia 7 - 9 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio ambao wamekwenda Elimu ya Sekondari kutokea Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, kadri ambavyo tutakumbuka dunia nzima hakuna mtu ambaye amekosea *ku-invest* katika elimu kwa sababu matunda yake ni dhahiri tutayapata. Nchi ya kibebari kama Amerika wameamua Elimu ya Sekondari ni lazima itolewe bure. Taifa la Canada na Sweden wameamua Elimu ya Sekondari ni lazima itolewe bure kama haki ya msingi ya mtoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niliambie Bunge lako Tukufu, takribani tokea miaka ya 1964, Zanzibar wameamua na naomba niwapongeze sana wananchi wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua watoto wote wa Zanzibar wanaomaliza Shule za Msingi ni lazima wasome Elimu ya Sekondari bure. Katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakuna sababu yoyote ambayo inatufanya tukiamua leo watoto wa Tanzania wasome Elimu ya Sekondari bure ishindikane. Wito wangu ni kwamba, Elimu ya Sekondari kwa wanafunzi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuitoe bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika uwiano wa Vyuo Vikuu, zaidi ya wanafunzi 50,000 Serikali ya Kenya inawasomesha katika Vyuo Vikuu vyake kwa wakati mmoja, Serikali

ya Uganda ni zaidi ya wanafunzi 40,000 na Serikali ya Tanzania ni katika wastani wa wanafunzi 15,000, tutashindwaje sisi katika ulimwengu wa *competition* kama hii iliyopo sasa hivi? Ninaomba na natoa wito Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza idadi ya wanafunzi tunaowasomesha katika Vyuo Vikuu vyetu vya Tanzania, tushindane na ninaomba mikopo ambayo tunawapa wanafunzi wanaosoma katika Vyuo Vikuu vya Serikali, *the same amount* iwe extended kwa wanafunzi wanaosoma Vyuo Vikuu vya Binafsi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii niwalaani wanafunzi wanaopenda kugoma bila sababu na wale ambao wanatumia na wanasiisa kugoma wakati Taifa letu linatumia pesa nyingi kuwasomesha. Naomba nichukue nafasi hii kuwaambia Walimu na wale wote wanaohusika, wajitahidi kutatua migomo hii pasipo kulazimisha Vyuo vifungwe mwaka mzima. (*Makofsi*)

Kwa mwanafunzi anayesoma sheria, *arts* na vitu vingine, *University of Dar es Salaam*, tunalipa takribani shilingi milioni moja na nusu kwa mwaka, mwanafunzi anayesoma Uadtari Muhimbili tunalipa si chini ya shilingi milioni sita kwa mwaka, wakigoma Chuo kikafungwa mwaka mmoja tunapoteza shilingi ngapi? Ninawapa ushauri wale wanaofanya maamuzi, wasifanye maamuzi kwa jazba, ni lazima wanafunzi hawa wapatiwe kila namna ya wao kuendelea na masomo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninaomba suala la kijana wa kijijini ambaye amekata tamaa, anahitaji elimu, lizingatiwe. Tunaweza kutumia pesa za UKIMWI kuwafanyia *training* vijana hawa wapate ajira. Tunaweza tukatumia pesa za ujenzi wa barabara za vijijini badala ya kumpa *contractor* tuwape pesa, tuwaajiri vijana wa vijijini wafanye kazi. *The spirit of enterprise* katika nchi hii ni lazima ijengwe. Ni lazima tunyanyue na tuwape matumaini, utampaje matumaini mtu ambaye hajui aanzie wapi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, naomba barabara ya Singida - Tabora - Kigoma na Singida - Arusha, zijengwe kwa lami ijengwe. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ninaomba nirudie wito wangu, Elimu ya Sekondari iwe ya bure na naunga mkono hoja. (*Makofsi*)

MHE. HASHIM A.Z. SAGGAF: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie. Moja kwa moja, napenda kusema naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, haina hitilafu wala sisiti kuunga mkono. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, pili, nataka kuzungumzia machache kuhusiana na Utaifa wetu na umoja tuliokuwa nao. Moja katika mema ambayo Mheshimiwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ametuletea ni uraia ambao ametuhakikishia na ambao umekuwa *enshrined* katika Katiba ya nchi yetu. Uhuru, utulivu na amani havikuja bure ila vimetengenezwa. Lakini la kusikitisha ni kuona kuwa kuna baadhi ya watu nao ni wachache hata mkononi hawajai, wakichukulia kwamba, Uhuru, Utaifa na usalama wa nchi yetu, kama vile ni kitu chepesi na cha kawaida ili kutekeleza azma yao ya

kujilimbikizia mali zaidi kuliko walizonazo, kuongeza makampuni zaidi chini ya himaya zao kuliko yale waliyokuwa nayo, kutafuta umaarufu kwa njia nyepesi, kutafuta uongozi wa Taifa au ndani ya wigo wa siasa na tunajua chaguzi ziko karibu, watu hawa wako tayari kuliweka Taifa letu pembezoni mwa janga wakivuruga uraia, utulivu, Utaifa na usalama wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukubwa wa nchi hii, tukikumbwa na balaa nchi hii ni ndogo sana kwa sababu balaa lile litamfika kila mwananchi. Silaha kubwa ambayo watu hawa wanatumia ni ubunifu wa maneno, wenyе fikra finyu, potofu na za kijinga na sera na dhana yao ambayo inapingana na Katiba ya nchi hii ni uzawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la kusikitisha ni kuona kuwa Serikali imenyamaza kimya kabisa hatujui je, kimya chao juu ya uzawa ni kwa sababu wanawaogopa hawa wazawa ambao ni wachache tu au wanakubaliana nao au hawakubaliani nao? Lakini ni vema Serikali ikatoa tamko rasmi sisi wananchi tukaweza kujua kila mmoja wetu mapema kabisa nini nafasi ya kila Mtanzania katika Taifa hili. Huo ni wajibu wa Serikali kutufanya, tujue kabisa kama uraia wa nchi hii umeshapitwa na wakati au kama uraia alioushughulikia Mwalimu Nyerere una matatizo au kasoro, tuelezwе mapema kabisa na je tunaanzisha mtindo wa ukoloni katika nchi hii kuleta uraia namba moja, uraia namba mbili ndani ya Taifa moja, tuelezwе na kama hizi ni njia za mwanzo za kuwawezesha hawa wazawa waweze kutimiza azma zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tulioko ndani ya Bunge hili tunaelewa mambo na tunaishukuru sana Ofisi ya Spika, kwa kuweza kutupatia *materials* mbalimbali. Lakini ni vema tukawaelewesha wananchi ya kuwa hizi sera za uzawa zinatupeleka pabaya katika Taifa hili na tuwatahadharishe wananchi hawa wasije kufikiri kuwa eti watu hawa wachache wakishahodhi makampuni yote haya na biashara zote hizi, basi wao maisha yao yatakuwa nafuu na kuwa nchi hii eti itapata utajiri mkubwa. Hiyo sio kweli, hiyo ni *ghilba* kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa biashara kubwa za viwanda una utaratibu wake, awe Mtanzania mzawa au mwekezaji wa nje wote zinamilikiwa na *supply and demand*. Soko likihitaji mwenye kiwanda atazalisha zaidi kwa kuweka mashine zaidi na kuajiri watu zaidi ili aweze kuzalisha bidhaa zaidi na kupeleka kwenye soko. Soko likianguka mashine nyingine zitafungwa lakini hatakubali kuwalipa watu mishahara bure atawaachisha kazi awe mzawa, awe nani, hivyo ndivyo atakavyofanya. Wala wasitudanganye, hao hao wazawa na biashara zao wanashirikiana na wakubwa wa nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na msimamo wa Serikali ni sahihi kabisa viwanda vitauzwa kwa wale ambao watavimudu kuviendeleza na ambao watavilipia kulingana na thamani yake na vile vile kuviwekeza sio kukaa kulalamika, waviwekeze kwa uwezo wao wenye na kufuata masharti yote ya Serikali watakayopewa na kulipa kodi zao. Kwa wazawa kusema lazima wapewe upendeleo maalum na halafu wawezeshwe, sio njia ya kuboresha uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, azma ya uzawa iko wazi, lengo lao kubwa ni kutaka zoezi zima la uwekezaji kwa watu wa nje lisitishwe, wawekezaji wa ndani ambao wana asili ya Kiasia wanyimwe fursa au wanyang'anywe. Wanataka jasho la wananchi litumike kuwawezesha wao na sio mtu yejote mwingine, hawa watu wa ajabu sana. Kwa sababu kilichotupelekea sisi kuanzisha Sera ya Ubinafsishaji ni kwa sababu ya Mashirika ya Umma kufa na yalikufa zaidi ya 400 na waliyaua hao hao wenye sura za uzawa, tuseme kweli, tunaposema kweli ndio tutakwenda vizuri. Sasa leo tutumie fedha za hao wananchi kuwawezesha wafanye mambo yao kwa uhuru zaidi. Hapana, sikubaliani na hilo na wananchi wa Jimbo langu hawalikubali na wanilikataa. Kama kuna kuwawezesha tuwawezeshe wafanyakazi, wakulima ili wawe na maisha bora, waishi vizuri, walee watoto wao vizuri, wawasomeshe vizuri katika hali ya usalamu, furaha na *self confidence* na watoto wao hawa ndio kesho watakuja kumiliki viwanda hivi, uchumi wa nchi hii na utawala wa nchi hii na sio vinginevyo. Ni njia pekee ya kueneza utajiri na kuwathamini wananchi wa nchi hii. Mimi sijaona wazawa wakapanga programu za kuwawezesha wananchi zaidi ya kuwakusanya watoto wa mitaani na kuwapa mlo mmoja kwa kutafuta umaarufu rahisi bila ya kujua hawa watoto baadaye wanakwenda kulala kwenye maboksi na vichochoroni. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wanapotoa madai yao wanakuwa sio wakweli. Wanatoa picha kama vile hakuna Watanzania asili ambao wamefaulu katika biashara. Lakini ukienda Kariakoo, ambayo ni sehemu mojawapo ya Jimbo la Mheshimiwa Iddi Simba, utakuta asilimia 60 ya watu wanaofanya biashara pale wanatoka Mikoa mbalimbali, maghorofa yanayojengwa pale zaidi ya asilimia 50 ni ya watu hao hao. Leo Wakinga wamekuwa wafanyakabiashara maarufu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna Mtanzania mmoja ambaye anamiliki Kampuni ya Usafiri wa Ndege ya *Precision Air*, kuna mwingine yuko Arusha anamiliki *Impala Hotel*, *the first class hotel*, ukiweka under any standards. Hao ni wachache tu ambao nawataja. Lakini hawa wanafanya mambo yao kimya kimya, wanatumia ujuzi wao na uwezo wao bila ya kelele, sio hawa wazawa kila wanapobanwa kidogo kibiashara hao wanakimbilia Serikalini, wanataka Serikali iwajibike eti kwa maslahi yao? Wanakuwa kama watoto wadogo ambao wakipigwa na wenzao wanakimbilia nyuma ya mama zao kujificha, hapana! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumiliki viwanda ni kazi ngumu na wanaoweza kumiliki wamefanya kazi nzito kweli, wengine wamechezea shilingi chooni, wamecheza kamari, wengine wameweka rehani, mustakabali wa watoto wao wengine wamefuzu na wengine wamefeli lakini hivi ndivyo biashara inavyokwenda ama unaelea au unazama. Kuna mengi ambayo sina nafasi ya kusema.

MBUNGE FULANI: Pasua.

MHE. HASHIM A.Z. SAGGAF: Lakini uamuji wa ubinafsishaji ni sera na tumeikubali, tukaileta hapa Bungeni na tukaipitisha. Kama kuna tatizo katika utekelezaji hayo mambo yanazungumzika hayana shaka, lakini kimsingi hiyo ni sera ya Chama na

asiyependezewa na sera hiyo basi aondoke kwenye Chama aingie kwenye Chama chochote kingine au aunde Chama chake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama hao wazawa wamejiteua kama Manabii kutimiza kilichoandikwa katika Kitabu Kitakatifu cha Biblia Mathayo 29, ambacho kinasema: "Kwa maana kila mwenye kitu atapewa na kuongezewa tele lakini asiye na kitu hata kile alichonacho atanyang'anya". Nataka Serikali iwaambie wazi kabisa kuwa Unabii wao uchwara haukulbaliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha azma ya kujilimbikizia utajiri kwa hao wachache, basi lazima tubaguane kirangi kinyume na Katiba ya nchi hii. Leo, karne hii ya 21 tunataka kutumia rangi kama ndio *component* ya *development*? Hao si Makaburu tu kama alivyowaita Mwalimu Nyerere. Makaburu tu hawa wala tusiowaonee haya. Uta-*define* vipi rangi, nani mweupe, nani mweusi, eeh?

MBUNGE FULANI: Mkorogo.

MHE. HASHIM A.Z. SAGGAF: Au tuanze kupimana pua na nywele? Tutapata shida maana mkorogo na kunyoosha nywele ndio mtindo wa leo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Chenge hayupo hapa lakini mara ya kwanza kutambulishwa kwa Mheshimiwa Chenge, nikauliza huyu ni Chotara wa Kigiriki? Nikaambiwa hapana huyu ni Msukuma halisi kabisa. Leo kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu utamwita mweusi. Kwa lugha ya Kiswahili yule anaitwa maji ya kunde. Sasa tunaanza wapi tunamalizia wapi? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, dhana hii ya *globalization* nia ni kutufanya wote tuwe familia moja duniani na sisi tumeanzisha *Africa Union*, nia yetu tuwe kitu kimoja lakini ndani ya Afrika kuna rangi chungu nzima kuna *chocolate*, kahawia, manjano, nyeusi, nyeupe, leo vipi tunaanza kujinasibu sisi kwa rangi? Mimi hii nashindwa kuielewa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo la wazawa ni kuwa hao wazawa hawasomi historia na kama wangesoma wangejua kuwa uzawa sio kitu kipy, ni kitu ambacho tayari kimeshajaribiwa huko nyuma. Hitler alikuwa mzawa na kama alivyosema Mheshimiwa Nyallandu, Warusi milioni 20 waliwaua kwa sababu ya uzawa, Wapoli 4,000, Wayahudi 6,000 walichomwa kwenye tanuri za moto, bado sijataja mamilioni ya watu waliokufa dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, kuna mtu mmoja anaitwa Iddi, lazima nimtaje, huyu Iddi aliipindua Serikali Uganda.

MBUNGE FULANI: Iddi?

MHE. HASHIM A.Z. SAGGAF: Ehh, Iddi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aliipindua Serikali Uganda, akaleta uzawa, akawahamisha Waganda wenyewe asili ya Kiasia 30,000...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

MHE. HASHIM A.Z. SAGGAF: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijajenga hoja yangu, naomba niungane na wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioshinda katika uchaguzi mdogo na kujiunga nasi katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwapongeza, naomba niwakumbushe Wabunge wenzangu kwamba, kilichotuleta ndani ya Ukumbi wa Bunge katika jengo hili Tukufu, ni kuwawakilisha wananchi wetu na kutetea maslahi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiingia ndani ya Bunge na kuleta malumbano ya kisiasa ni hatari. Tunaweza kusahau kilichotuleta maana hatukuja ndani ya Bunge kuchochea wananchi kwamba, eti Watanzania wataenda barabarani kuandamana. Maana yake nini Mheshimiwa Spika? (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Au wote tutaenda shimonii.

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Mheshimiwa Spika, ninaomba tusome Kanuni za Bunge ambazo ndio zinatawala jengo hili Tukufu Ibara ya 50(8)(d) inasema kabisa malumbano ya kisiasa hayaruhusiwi ndani ya Bunge. Malumbano yetu ya kisiasa ni wakati tunagombea kwenye viwanja pale mbele ya wananchi, pale ndio tunauza sera zetu. Ninaomba niwahakikishie kwamba, Watanzania wana akili timamu, wanajua kuchuja kati ya pumba na chuya na kuona mchele mzuri uko wapi ndio maana mwaka 2000 CCM ilishinda kwa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, CCM imejenga demokrasia sahihi ndani ya nchi hii na ndio maana tumeleta Mfumo wa Vyama Vingi bila kushinikizwa na mtu yeoyote. Kama CCM isingeamua hivyo leo Vyama vya Upinzani visingekuwepo Bungeni. Kwa hiyo, naomba tuingie Bungeni tutetee maendeleo na maslahi ya wapiga kura wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Mbunge mmoja aliyezungumzia suala la Tume Huru ya Uchaguzi. Tume Huru ya Uchaguzi maana yake nini? Wawakilishi au Wajumbe wote wa Tume wanatakiwa wasiwe *affiliated* na Chama chochote. Leo mkiwa

na Wajumbe wa Tume ambao wana *affiliation* na Chama, hiyo itakuwa Tume Huru au Tume ya Vyama?

MBUNGE FULANI: Sio kweli!

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Kwa hiyo, ninaomba tuzingatie taratibu zetu za nchi na tumekuwa tukiendelea katika nchi hii kwa uchaguzi wetu ambao uko wazi kabisa, ni *transparency* ya hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa hoja hizo, ninaomba nichukue fursa hii kuipongeza Serikali yetu ya Tanzania, Serikali ya CCM, kwa kazi nzuri ambayo inafanya. Serikali ya CCM sio Serikali nyoronyoro ni Serikali imara, ilijojengwa kwa misingi ya Chama imara, Chama cha CCM kwa sera zake madhubuti ambazo zinalenga wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuwa Waziri Mkuu au kiranja mkuu sio kazi ndogo. Nakumbuka Marehemu Kinyondo, Mungu amlaze mahali pema peponi, alikuwa anasema Serikali ina macho kama chandarua na nataka kusema Serikali ina shughuli nyingi kama matundu yalivyo ndani ya chandarua na zaidi. Sasa ukisema Waziri Mkuu au Serikali haifanyi kazi, kwa kweli ni kumwonea, hebu tujilinganishe miaka ya 1970, 1980 na leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue mfano wa kwetu tu, leo tukitaka kwenda kwetu Kusini kuna daraja Mto Rufiji huna haja ya kusubiri kivuko, unavuka kwenye daraja na unakwenda. Sasa hivi barabara ile wanaosema kwamba sio lami lakini sisi tunaona ni lami kwa sababu tunawenza kupita karibu mwaka mzima, hongera Serikali ya CCM. Nafikiri lile ndio daraja refu kuliko yote katika Afrika. Kwa hiyo, Serikali imefanya kazi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kufanya kazi hiyo, haiwezi kukosa mapungufu kwa sababu wanaofanya kazi ni binadamu na binadamu hawajatimia. Ndio maana wengine wakisimama Mheshimiwa Spika, unawaambia mbona hujasimama, kwa sababu ni wafupi na wengine si ajabu kwa urefu wao unatamani kuwaambia mbona umesimama juu ya kitu, kumbe kwa sababu ni warefu. Hatulingani na watendaji ndani ya Serikali ni hivyo hivyo. Kuna wengine ni wabunifu zaidi na wengine sio wabunifu wanahitaji kusukumwa kila wakati. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sisi Wabunge kuisukuma Serikali na kuwakumbusha wajibu wao kila wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa wa Lindi na wanawake wa Tanzania, kwa kuondoa Kodi ya Maendeleo. Kwa kweli imetupunguzia kero kubwa na imetujengea heshima Serikali ya CCM kwamba, kweli ni Serikali inayojali watu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ilijengwa hapa kwamba Waziri Mkuu, aombe radhi kwa sababu ya kuitisha Kodi ya Maendeleo wakati ule. Kuna usemi wa Mzee wetu Mwinyi ambapo anasema: "Kila zama na kitabu chake". Sasa zama ya kitabu hiki cha

sasa ni kufuta Kodi ya Maendeleo. Wakati ule tumeanzisha Kodi ya Maendeleo, Serikali ilikuwa inakusanya shilingi bilioni 25 kwa mwezi, leo Serikali inakusanya zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa mwezi, kwa hiyo, ina uwezo. Sasa ukilinganisha wakati ule kipato cha Serikali kilikuwa kidogo ni haki kuwa na Kodi ya Maendeleo. Kwa hiyo, Serikali haina sababu hata kidogo kuomba msamaha kwa sababu ilikuwa inafanya kazi sahihi maana hata vitabu Vitakatifu vinasema: “Mpe Kaisari yaliyo ya Kaisari na mpe Mungu yaliyo ya Mungu”. Wakati ule tulitakiwa tuchangie katika maendeleo yetu kwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa wengine wakisema kwamba eti tunajiandaa kwa uchaguzi wa mwaka 2005, leo 2003 jamani mbona bado tuna muda na hata kama tunajiandaa kwani kuna ubaya si tunatekeleza sera zetu za CCM? (*Makofit*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono sana hoja hiyo na nasema wala Serikali isitetereke ikaona kwamba imechupia hoja ya watu, lakini kuna watu wana uzoefu wa kupenda kuchupia hoja za CCM. Tukizijenga na zikaonekana ni hoja za msingi basi watu wanachupia wanasema hizi za kwetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nigusie suala la kuanzisha Benki ya Wakulima. Nakubaliana lakini nasema kama Serikali ina mtaji na ina uwezo wa kifedha basi iimarishe *NMB* ambayo ina mitandao nchi nzima badala ya kutaka kuibinafsisha *NMB* halafu tuanzishe benki mpya. Kuanzisha benki ni gharama, unahitaji majengo, kompyuta na kila kitu. Sasa tusije tukafika mahali tukaimarisha benki halafu tukataka kubinafsisha tena. Tuanzishe suala la kuwasaidia wakulima lakini tupitishie *NMB*.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ninapongeza Sera ya CCM ya ubinafsishaji lakini si vibaya CCM ikarejea na kuititia utaratibu wake ili tuone wapi tuna mapungufu. Kwa mfano, *ATC* imebinafsishwa, lakini huyu aliyenunua hisa 49 katoa Nembo ya Taifa, twiga hayupo. Jamani asilimia 49 na Serikali tuna asilimia 51 kwa nini twiga ametolewa? Halafu pale wakaweka Nembo ile ya Ndege ya Afrika ya Kusini. Naomba Serikali iliangularie hilo maana tusije tukarudia yale ya *TTCL*, mtu ametoa hisa asilimia kumi na saba na nusu anapewa mamlaka ya kuendesha Kampuni nzima ya Simu.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 34 Mheshimiwa Waziri Mkuu, amegusia suala la mitandao ya simu na mitambo itakayojengwa. Nasikitika kuona kwamba, Mkoa wa Lindi haujaguswa hasa ukichukulia historia kwamba Lindi ilikuwa Makao Makuu ya *Southern Province* enzi zile za ukoloni na ndiyo imezaa Mkoa wa Ruvuma na Mtwara. Kuna Wilaya ya Ruangwa ambayo imefanya kazi nzuri sana, ni Wilaya changa wana simu za kukoroga. Wilaya ya Liwale, Wilaya kongwe ambapo alitoka *PM* wa kwanza, lakini hawana simu mpaka leo, mawasiliano kule ni ya *radio call*. Naomba Serikali iliangularie hili. Wakati tunapeleka simu Tarafani, Wilaya zingine hazina simu kwa kweli naomba tusiwe *magnetic South* wa kusahauliwa sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, suala la nne, katika ukurasa wa 37 na 38 katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu amegusia juu ya Songosongo gesi ambayo itakuwa *pumped* kutoka Kilwa kwenda Dar es Salaam ili kuzalisha umeme uingie kwenye *grid* ya Taifa.

Ninazungumza kwa uchungu mkubwa kwamba sisi Lindi na Mtwara tunaambiwa tutafaidika na gesi ya kupikia hivi gesi hiyo tutaipikiaje? Majiko ya gesi ni ghali. Sisi shida yetu ni Lindi na Mtwara hakuna umeme. Wawekezaji hawataki kuja katika Mikoa hii kwa sababu hakuna umeme wa uhakika. Sasa pamoja na kazi nzuri ya kutujengea barabara, tupeni umeme. Ile gesi ya Songosongo ndiyo umeme wa uhakika na ukombozi wa Kusini katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ili kule nako tuendele. Maana historia sisi imetubana kwa sababu ya kushiriki kwetu katika vita vya ukombozi wa Kusini mwa Afrika. Sasa tusikandamizwe, ninaomba sana gesi ya Songosongo ikitoka pale ikifika Somanga wajenge mtambo wa kuzalisha umeme ambao uta-supply Lindi na Mtwara ambako hatuna umeme wa uhakika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nataka kuchangia ni katika ukurasa wa 39. Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia juu ya ardhi ambayo kila Mkoa wanatakiwa wabainishe ipimwe ili wakaribishwe wawekezaji. Napenda sana waje wawekezaji lakini natoa tahadhari tusije tukageuzea Zimbabwe namba mbili. Naomba tuhakikishe kwamba sisi wenyewe Tanzania tunawezeshwa ili tuweze kulima. *Exim Bank* imepewa fedha za pembejeo lakini ipo Dar es Salaam. Hebu niambie yule mkulima aliyeko Sumbawanga atafika Dar es Salaam? Yule Mmachinga aliye Lindi ataweza? Lakini sisi kule Mkoa wa Lindi tuna ardhi nzuri sana, *virgin land* na mimi najua kwetu kumebainisha hivyo, lakini hatuna matrekta. Je, Mfuko wa pembejeo sasa utaoa mikopo ya matrekta? Mkopo huu nao una masharti magumu. Unachukua mkopo ule na unatakiwa uurejeshe katika mwaka mmoja. Sasa wewe ukununue *sulfur*, ukapulizie, uvune, uuze na wakati mwingine usiwe na uhakika wa bei, unaweza ukafika mahali ukanyang'anywa raslimali yako kwa vile tu umepewa muda wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ: Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu. Naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri wake wa Nchi, kwa kazi nzuri ya kuandaa hotuba hii tunayojadili hivi leo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile niwapongeze Wabunge wapya kutoka CCM na wale wa Upinzani. CCM ilipoamua tuwe na Vyama Vingi vya Siasa, ni mategemo kwamba, tutakuwa na *challenge* kubwa kutoka Vyama vya Upinzani, lakini kidogo nina wasiwasi kama hilo litakuwa. Nadhani CCM tungeendelea tu kujikosoa wenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ningeomba nzungumzie kwanza hali ya uhalifu nchini, hasa maeneo mawili ya ujambazi na madawa ya kulevy. Vikosi vya madawa ya kulevy na Polisi kwa umoja wao, kwa kipindi kirefu wamekuwa wanafanya kazi nzuri ya kudhibiti uhalifu na madawa ya kulevy. Lakini vile vile kwa uchache wao hawawezi kudhibiti kila kitu kwa sababu nchi yetu ni kubwa sana. Kwa hiyo, natoa wito kwa viongozi na wananchi wote kwamba, lazima tuwasaidie Polisi ili kuweza kudhibiti wimbi la matukio haya ambayo kwa kweli kila muda unavyokwenda mbele yanazidi kuongezeka sana na

hivi sasa lipo wimbi la wahalifu kutoka nje ya nchi. Kwa hiyo, napenda kutoa rai kwamba, Serikali iandae *operation* maalum ya kuwasaka wahamiaji haramu ndani ya nchi yetu ili kutunza hali ya usalama katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, asubuhi wakati niko pale nje nilisikia mchango wa Mbunge mwenzangu mmoja, sikumjua ni nani, alikuwa anatoa hoja kwamba, Mikoa ikiwezekana iunganishwe ili Mikoa mitatu iwe na Mkuu wa Mkoaa mmoja. Mimi kwa upande wangu naona siungi mkono ushauri ule kwa sababu katika baadhi ya Mikoa, Wakuu wa Mikoa wana maeneo makubwa sana na wala hawafikii Mikoa yao vizuri kama wenyewe wanavyopenda. Lakini wakati huo huo ni juzi tu Mheshimiwa Rais, aliugawa Mkoaa wa Arusha na watu wengi tukashangilia hapa kwamba, lengo ni kupeleka huduma karibu na wananchi. Sasa leo tukidai Wakuu wa Mikoa sasa tuwaunganishie Mikoa mitatu, kwa kweli nadhani itakuwa ni kazi ngumu mno na ni yale yale ya Umajimbo ndiyo yataanza tena. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba utaratibu uliopo sasa ubakie na ikiwezekana ile Mikoa mikubwa igawanywe ili iwe miwili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nizungumzie suala la umeme. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumzia kwamba, Mikoa ya Lindi na Mtwara itafaidika na Mradi wa Songsongo kwa kupata gesi ya kupikia. Sijui Mheshimiwa Waziri Mkuu anazungumzia gesi ipi ya kupikia? Maana Mradi ule ni kuchukua gesi kutoka Songsongo mpaka Dar es Salaam ndipo inakosafirishwa, hakuna bomba la kwenda Lindi. Kwa hiyo gesi yote itakwenda Dar es Salaam na kila mnunuzi atanunua Dar es Salaam aidha wa kutoka Tabora, Iringa, Lindi au Shinyanga, soko ni Dar es Salaam ndio kwenye kiwanda. Lakini watu wa Lindi sasa shida yao siyo gesi ya kupikia, shida yao ni umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, maelezo ya karibu karibu ni kwamba, umeme wenu uko *Mnazi Bay*. Leo ni miaka ishirini na kitu toka gesi ya Songsongo ilipogunduliwa, lakini inachimbwa sasa. *Mnazi Bay* ndiyo kwanza leo tunaangalia kiwango cha gesi kilichopo, baada ya hapo tutafute mwekezaji aandike mchanganuo wa mradi, kisha tutafute fedha tuanzishe mradi, ndiyo tupate umeme. Mpango huo sijui utakuwa ni wa miaka kumi, kwa kweli wananchi wa Lindi na Mtwara hatuwezi kusubiri kwa muda mrefu wote huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, raslimali ya gesi ipo Mkoani Lindi. Gesi imetoka Lindi kuja Dar es Salaam kuzalisha umeme, lakini Lindi hakuna umeme. Hivi jamani kuna chanzo cha umeme na kwenyewe kukawa hakuna umeme, kama wapi? Kwa mfano tu kama wapi, Nyumba ya Mungu, Kidatu, Hale au Kihansi? Jawabu ni kwamba, kila mahali penye umeme na penyewe kuna umeme, lakini Lindi peke yake gesi yao inakuja Dar es Salaam umeme uende Tabora, Shinyanga na Malampaka na Lindi kwenyewe kuwe hakuna umeme! Mheshimiwa Waziri Mkuu hii kweli? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na rai moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, zipo fedha hapa zimetengwa shilingi milioni elfu moja kwa ajili ya usambazaji umeme. Mpango uliopo wa kuapatia umeme Mji wa Kilwa. Naomba Mheshimiwa Waziri, mtambo uwe mkubwa ili upeleke umeme mpaka Lindi, Ruangwa, Liwale,

Nachingwea, Mtwara, Newala, Tandahimba mpaka Tunduru kutokea gesi ya Songsongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baadaye *Mnazi Bay* ikiwa tayari, chukueni gesi muunganishe na mtandao wa gesi ya Songsongo ije Dar es Salaam, sisi tupo radhi. Lakini ninaomba sana Serikali na ni vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko pale, wananchi wa Lindi na Mtwara matumaini yetu ni kwamba, umeme wa kweli ni umeme wa gesi ya Songsongo na si *Mnazi Bay*. Kwa hiyo tunaomba mpango wa kweli uwe kutupatia umeme kutoka Songsongo na si *Mnazi Bay*, huo hatuuamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile niishukuru Serikali, baada ya kusikia kilio chetu kwa kazi nzuri ya ujenzi wa daraja la Mto Rufiji. Kwa sehemu kubwa limekamilika na kwa kweli kwa kiongozi au mwananchi ye yeyote wa Mikoa ya Kusini, hawezu kukaa kimya bila kushukuru kwa hicho ambacho kimefanyika japokuwa barabara bado. Mkataba umesainiwa huu ni mwezi wa sita sasa, hatujaona zile vuguvugu za barabara. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, yupo hapa ananisikia mtusaidie. Wale watu waanze kazi mara moja kwa sababu sasa tumepata wasiwasi, tumesikia Mkataba umeshatiwa saini, wamepewa malipo ya awali lakini mpaka leo ni darubini tu ndiyo tunazona kule. Sasa watu wanataka makatapira siyo darubini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningeomba kumalizia kwa kuomba Serikali iangalie namna ya kuwasaidia wafanyabiashara wadogo, kuwapunguzia kero ya kulipa ushuru na kodi mbalimbali ili waweze kupata nguvu ya kujijengea uwezo wao kwa kujitegemea wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa uamuza wake wa kufuta kodi ya maendeleo, ambao kwa kweli Wapinzani tumewaacha hoi, wakitegemea kwamba ndiyo *agenda* yao nzuri ya 2005, lakini hii ni mipango ya CCM na bado huo ni mwanzo tu. Naamini mwaka 2004 mtafanya mengine zaidi kuliko ya mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ABDILAH O. NAMKULALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii. Naomba nianze kwa kuipongeza Simba kwa ushindi. *RAS* wetu kule Mtwara Alhaj na *DC* wetu Dololo ukisema Simba tu basi meno yote thelathini na mbili lazima uyaone. Sasa nadhani waliko huko wamefurahi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa viongozi wa Kitaifa ndivyo walivyo. Makamu wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi si Mwakilishi lakini vile vile Mheshimiwa Mwenyekiti Lipumba kule kwao wala siyo Diwani. Kwa hiyo ndivyo ilivyo wala msione ajabu kwa hilo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kufuta Kodi ya Maendeleo. Suala la kodi ya maendeleo wala si sera ya Wapinzani. Ni sera ya CCM ya kuondoa kero pale ambapo Serikali inaweza kuondoa kero hiyo na yalikuwa yanafukuta haya kwenye CCM. Kwa ushahidi mimi mwenyewe Mbunge wa CCM nilimwandikia Waziri wa Serikali za Mitaa na nakala nikapeleka kwa Rais juu ya kumwomba kufuta kodi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Waziri wa Afya niliiona barua yake anamwandikia Waziri wa Serikali za Mitaa, nakala kwa Mheshimiwa Rais kuomba kufuta Kodi ya Maendeleo kwa sababu kuna uwezo wa kugharamia Serikali Kuu. Kwa hiyo, yalikuwa yanafukuta kwenye CCM siyo ya Upinzani, isipokuwa mlikuwa hamjui kwa sababu mambo yetu sisi tunafanya kimya kimya kwanza. Mnafanya mchezo nini? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kukarabati zahanati na vituo vya Afya vya Jimbo la Mtwara Vijijini na kuboresha elimu ya msingi ila kidogo kuna tatizo naomba Serikali irekebishe. Walimu wa shule za msingi ni wachache mno na watumishi kwenye zahanati na vituo vya afya vilivyokarabatiwa ni wachache sana kiasi ambacho mmoja au wawili wapo zahanati moja. Naomba Serikali iongeze walimu na iongeze watumishi hawa wa zahanati ili kazi ifanywe kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameomba fedha kwa ajili ya janga la Ukimwi. Nilikuwa nazungumza na Naibu Waziri wa Afya, nikimwomba asisahau kufanya utafiti wa dawa za kienyeji kama inawezekana. Wanadai zipo zinazoongeza muda kidogo, akaniambia Mheshimiwa Namkulala, ukimjua mganga mmoja mlete. Nikamwambia kuna Mganga mmoja anaitwa Eliashia, akasema mlete ili tuweze kuzungumza naye tuone kama kweli dawa zake zinaweza kuongeza muda na waganga wengine. Kwa hiyo na Wabunge wenzangu kama kuna waganga wengine mnawafahamu mpelekeeni Naibu Waziri na kama wapo humu vile vile waende. Dawa hizi za kitaalam ni ghali mno labda dawa za kienyeji zinaweza kuwa rahisi kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nilialikwa kwenye mkutano kwenye Jimbo langu uliofanyika Kijiji cha Mkahara na Vijiji takriban si chini ya kumi na tatu wakijadili juu ya kuondoa tatizo sugu la maji. Wakanieleza Mheshimiwa Mbunge, kaieleze Serikali kwamba sisi tumbaini kwamba mdudu huyu anayeitwa umaskini kwenye Jimbo la Mtwara Vijijini anapenya kwenye tundu la tatizo la maji. Kwa sababu kwa kukosa maji akina mama wanachukua saa tano mpaka sita kuhemea ndoo moja ya maji kwa siku. Kwa mantiki hiyo wanashindwa kupata muda wa kushiriki shughuli za maendeleo, pamoja na za uzalishaji kama vile kupalilia mikorosho, kulima mihogo na hatimaye wanapata mazao kidogo ya chakula na inasababisha kwenye Kaya kuwa na chakula kidogo, hatimaye kuwa na utapiamlo wa watoto na akina mama wajawazito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile kuna utapiamlo watoto wanakuwa dhaifu, hata wakienda shule wanakuwa dhaifu na hata akikua. Kwa hiyo, inakuwa afya zao hata

wakikua siyo nzuri kwa kuzalisha zaidi. Halafu vile vile kwa mazao ya biashara kwa sababu palizi inafanywa na mtu mmoja kwa sababu mwingine anakwenda kutafuta maji. Matokeo yake korosho zinapatikana chache, hatimaye fedha zinapatikana kidogo, zinashindwa kubeba gharama za kusomesha vijana wao na za kutibu familia. Kwa maana hiyo, umaskini unataga pale kwa sababu ya tatizo la maji. Kaiombe Serikali wawatume wataalam waje Mtwara Vijiji waangalie bwawa la Chipwalapwata. Waone uwezekano wa kusambaza maji katika Tarafa ya Nannyamba na Tarafa ya Kitaya, tunadhani maji yale yanatosha, tunaomba msaada huo. Leo nafikisha ujumbe hapa kwamba wanachini wa Mtwara Vijiji wanaomba Serikali iende Chipwalapwata wakaone uwezekano wa maji yale kusambazwa katika Tarafa ya Nannyamba na Kitaya. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kuhusu suala la barabara. Barabara ya Mangamba-Kitaya-Mnongodi mpaka Chikwaya ni mbaya sana. Barabara ya Nannyamba-Newala mpaka Masasi inastahili lami. Barabara inayounganisha Wilaya nne inakuwaje ya vumbi, hivi mlimsikia nani? Pale inahitajika lami bwana. Barabara ya Hiari-Dihimba-njengwa mpaka Nannyamba haipitiki. Siku moja nilikuwa natoka Msimbati usiku kwa bahati mbaya gari yangu ikazima taa ghafla, basi nilipiga honi kulipigia shimo nikifikiri tembo kumbe shimo barabarani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niliitwa na Umoja wa Akinamama waliokutana katika Kijiji cha Kihamba, nilipofika baada ya mazungumzo yao kukawa kuna akina mama mimi sikujua kwamba walijipanga makusudi, kama kumi na mbili hivi lakini wajawazito, mtaniwia radhi akina mama. Wakaniambia tulichokuitia ni hiki, hawa akina mama wajawazito roho zao zote zimeshikwa na Serikali kwa sababu iwapo kama hata kujifungua kwake mmoja wapo hakutakwenda vizuri, ikabidi aende Ligula kufanyiwa *operation*, basi *Wallahi* hofu kubwa ni kwamba inawezekana katikati ya *operation* umeme ukakatika, basi mama yule na mtoto kwaheri. Kwa sababu umeme Mtwara siyo wa uhakika, muda wowote unaweza ukakatika, kwa hiyo, tulichokuitia Mbunge wewe ukatoe shilingi kwenye bajeti zao huko, unajua wewe mwenyewe huko huko, tukusikie unatoa shilingi.

Mheshimiwa Spika, kuna ndege mmoja alikuwa kila akiangua watoto bwana mmoja anakwenda kuchukua anakula. Siku moja yule ndege akamwomba Mwenyezi Mungu, ewe Mwenyezi Mungu kwa nini humgharakishi huyu mtu anayekuja kuchukua watoto wangu? Mwenyezi Mungu akasema basi wewe taga safari hii nitamgharakisha. Yule bwana alipojua wale watoto wamekua akawa anakwenda kuwachukua, alipokuwa anakwenda akatoa sadaka shilingi moja kumpa maskini, akaenda kule na kuchukua wale watoto akaondoka nao. Ndege akamwuliza Mwenyezi Mungu mbona hukumgharakisha? Akasema ni vigumu sana kumgharakisha mtu aliye-*taswaddak*, yule wakati anakuja kuchukua wale watoto alitoa sadaka, kwa hiyo ikaniwia vigumu. Sasa Serikali ya CCM ime-*taswaddak* kwa kufuta kodi, kwa hiyo inaniwia vigumu mimi kutoa shilingi. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini Mheshimiwa Spika, wapiga kura wangu wameniambia nitoe shilingi na mimi nipo kwenye *dilemma*. Vigumu kutoa shilingi kwa sababu ya *taswaddak* na wapiga kura wangu wameniambia toa shilingi, hapo sasa! Kwa hiyo, naiomba Serikali ya CCM,

Mheshimiwa Yona, tafadhali unisaidie katika *dilemma* hii, katika hotuba yako suala la jenereta la Mtwara Mjini tafadhali kama halipo liweke ili mimi nisitoe shilingi. Suala la umeme la Nannyamba, *survey* tayari kutoka Tandahimba kwenda Nannyamba kama halipo tafadhali usiku huu na kesho fanya fanya vizuri ili hotuba hiyo itaje Nannyamba kuwa watapata umeme na jenereta za Mtwara kwamba zipo njiani na kwamba si muda mrefu zitapatikana ili mimi nisitoe shilingi. Kwa sababu mmetoa *swadaka* na ili wananchi wangu nisiswakose, tafadhali niko chini ya miguu yenu, chonde chonde. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali nzuri kama hii iliyofuta kodi kutoa shilingi wewe hauoni hatari na wapiga kura wale walionipa kura mimi kuniambia toa shilingi na nisitoe halafu sina maelezo ya kuwaeleza, huoni kwamba inatisha. Sasa hapa nifanyeje? Tafadhali naomba mniokoe jenereta la Mtwara nitafanyaje? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nniombe Serikali waanzishe Mfuko wa Maji wa Taifa, ambao utakuwa kama wa *Road Toll*. Wapeleke fedha huko Wilayani shilingi milioni hamsini kama wanavyofanya katika fedha za barabara ili zichimbe mabwawa na zikarabati miradi ya maji kwa sababu tatizo la maji ni gumu sana. Mkipeleka shilingi milioni hamsini au sitini kwa shughuli za maji kule Mawilayani, yaani CCM ndiyo basi itapita miaka yote hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii lakini tafadhali Mheshimiwa Yona, chonde chonde *kunnelenge*. Basi wekeni vizuri jenereta la Mtwara ili umeme upatikane Ligula na umeme katika ile hospitali ya *Mission* ya Nannyamba ili ifanye kazi na akinamama hawa niwe na sababu ya kuwaeleza kwamba sikutoa shilingi kwa sababu hotuba si mmeisikia, imesema hivi na hivi na jenereta si ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho ya leo hii na naamini ni busara zako ndiyo zilizokufanya uniweke mimi mwisho, kwa kuona hasa kwamba, Mafia ni sehemu moja ambayo inakabiliwa na matatizo makubwa kabisa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na wasaidizi wake, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib na Mheshimiwa William Lukuvi, kwa jitihada zao za kuiendesa Serikali hii kwa ufanisi kabisa. Naomba pia nichukue fursa hii haraka haraka kumpongeza Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, wote kwa bajeti zao, walivyozipanga na kuweza katuandalia mpango maalum hususan wa kuweza kupita kidedea mwaka 2005, hasa baada ya katuondolea hii Kodi ya Maendeleo ambayo ilikuwa kero na pia Serikali kubeba mzigo huu wa kuwalipa *VEOs* na *WEOs* katika Halmashauri zetu huku kwetu Tanzania Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya ni matokeo mazuri sana ya ushirikiano kati yao na wataalam walio chini ya Wizara zao. Hii inaonyesha ni dalili nzuri kabisa ya Serikali yetu ya Awamu ya Tatu, iliyokuwa chini ya Chama cha Mapinduzi, inayoongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na hii inaonekana kabisa ni moja ya dhana kubwa kabisa ya Serikali hii kutusikiliza sisi kama wawakilishi, yaani Waheshimiwa Wabunge, matakwa ya wananchi na kama ikiwa moja ya sehemu ya kuweza kupata taarifa tunazozitoa sisi Majimboni mwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutumia fursa hii, kuwapa pole wapiga kura wangu wa Wilaya ya Mafia, ambao wiki mbili zilizopita akinamama watatu walipata ajali ya kuangukiwa na mnazi na kufariki wakati wao walikuwa kwenye mazishi ya mwanamke mwenzao. Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi na wafiwa nao Mwenyezi Mungu, awape subira kwa sababu wao wametangulia na sisi tuko nyuma yao na hii ni kazi ya Mola. (*Amen*)

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni yetu sote na pale yanapotolewa maoni kutoka kwetu sisi Waheshimiwa Wabunge, basi naamini Serikali ndiyo huwa inajua na kuona nini la kufanya katika kutoa migao yao ya wapi wafanye nini na hapa wafanye nini.

Mheshimiwa Spika, wahenga walituachia methali moja inayosema "nyota njema huonekana asubuhi". Lakini kule kwetu Mafia pia tuna neno moja tunalosema kwamba, *madengo ntima*. *Madengo ntima* maana yake kaza moyo.

Hii yote ni kuonyesha kwamba, wananchi wa Mafia kwa kipindi kirefu kabisa toka tumepata uhuru wanakaza miyo kabisa kabisa na kuhakikisha kwamba, wanaienzi Serikali yao kwa kuititia Chama cha Mapinduzi, kwa kuipa ridhaa tangu tumepata uhuru wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia toka mwanzo wa bajeti ya Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha na hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sijui kwa hizo Wizara nyingine zinazokuja hasa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, japokuwa juzi tu tumepata majibu mazuri. Lakini bado haikutamkwa kabisa mpango maalum wa ujenzi wa gati ya Kisiwa cha Mafia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni kero na naamini Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, amesema hapa kwamba, toka mwaka 1977 suala la gati linazungumzwa na Serikali inalifahamu na hatimaye mwaka 1993 upembuzi yakinifu wa gati hilo ulifanywa na umeshajulikana kwamba, lijengwe Kilindoni kwa gharama za shilingi bilioni 3.5. Lakini mwaka 2002, Mwenyezi Mungu alijalia Mheshimiwa Basil Mramba yeche mwenyewe alikaa na kuamua kutoa Sh. bilioni 1.96 kwa ajili ya ujenzi wa gati hilo. Lakini mpaka dakika hii hakuna jambo lolote lile ambalo tunaona limeshaanza *ku-take action* katika ujenzi wa gati hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoomba kwa unyenyekevu mkubwa kuititia kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atoe katika fungu

lile ambalo alitoa mwaka 2002, basi na mwaka huu achukue kidogo aongezee na ujenzi uanze mara moja. Kwa sababu tukisubiri mwaka 2004 hali inazidi kuwa mbaya, jamaa hao ndiyo mnawaona, lakini sisi hatuwaogopi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mafia ina nafasi kubwa sana ya kuweza kuchangia pato la nchi hii. Hivi ninavyoongea tayari kuna Kampuni moja inaitwa *Karafi and Sons*, hawa watu wako tayari kuja kujenga kiwanja cha *golf* katika Wilaya ya Mafia na wamesema kwamba kitakuwa kiwanja cha tatu katika Afrika, cha kwanza sijui kiko *South Africa* na cha pili kiko Egypt, Misri na cha tatu wanataka kiwe Tanzania na wamechagua katika sehemu moja inayoitwa Tereni pale Mafia karibu na Kilindoni, kilomita kama 2 mbili tu kutoka mjini, watakuja kujenga kiwanja hicho na wamesema pia watajenga hoteli yenye vitanda 600 katika eneo lile, sasa ni faraja kubwa.

Lakini alipokuja Meneja wao alishangaa akasema jamani, tutajenga kweli hali kama hii, hao watalii wetu watakuja na nini, jaribu sana kuboresha miundombinu katika Wilaya hii. Kama tutapata gati la uhakika, mimi naamini Mafia itakuwa ni sehemu moja kubwa kabisa ya kuweza kuchangia katika Pato la Taifa kupitia Sekta hiyo ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba, siku moja Balozi wa Italy alitembelea Mafia, lakini hakwenda Kiserikali, aliamua yeye mwenyewe tu kwenda Mafia na bahati nzuri siku hiyo na mimi tulipanda ndege moja, yeye hakunitambua na mimi sikumtambua. Tulipokuwa pale *VIP Lounge* ndiyo nilipomsikia Mheshimiwa tayari safari, nikamwona na yeye anayanyuka, nikamwuliza wewe Mzungu unatoka wapi? Akaniambia mimi ni Balozi wa Italy nakwenda kutembelea Mafia, nikamfahamisha na mimi ni fulani twende zetu.

Kufika kule kwa bahati nikakuta gari la Mkuu wa Wilaya liko pale, nikatoa taarifa tukamuenzi akaenda kule akafika. Bahati mbaya siku ile mtoto wake aliibiwa au alipoteza madaftari kule shulen ikwao. Sasa mnajua hulka za wenzetu akawa anataka kuwasiliana naye. Yule Balozi anaitwa Marcelo, alikuwa anataka akae siku nne kule Mafia, siku ya pili mimi nilikuwa nimeenda kwa dharura na kurudi, nikakutana naye *Airport* tena akasema eeh bwana narudi kwa sababu akili imenichanganya nataka kuwasiliana na mtoto wangu nimeshindwa, hivi nimeamua nirudi nakwenda Dar es Salaam kwa kuwa mawasiliano yalikuwa mabovu. Bahati nzuri na mimi gari yangu ilikuja kunipokea nikamchukua yeye nikampeleka mpaka nyumbani kwake hakika alifarrijika.

Mheshimiwa Spika, lakini mawasiliano ni jambo muhimu sana katika *area* yetu, hasa mkizingatia kwamba, sisi ni Kisiwa. Watu wanalamika hapa Kigoma, lakini wenzetu wana treni, mbona hivi, hatusemi Mwenyezi Mungu, awajalie wote tunaitaka. Lakini tuoneeni huruma sisi watu wa Kisiwani hatuna nyenzo nyingine. Ukerewe leo namwonea huruma Mheshimiwa Getrude Mongella.

Tumepanga na Mheshimiwa Getrude Mongella, twende tukamwone hata Mheshimiwa Rais, tumwombe atupe kitu fulani cha kuweza kutustiri sisi watu wa Visiwani atutilie nguvu. Kwa hiyo, hili tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu

katika bajeti ya mwaka huu wa 2003/2004, suala la gati lianze na huduma hizi za simu ziweze kuboreshwa katika Wilaya ya Mafia. Mwaka 2004 ni mbali sana Mheshimiwa Dr. Maua Daftari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia kidogo suala la Kitengo cha Maafa. Tuna Kitengo cha Maafa ambacho kipo katika Wilaya zetu Mwenyekiti akiwa Mkuu wa Wilaya. Lakini wana nini kule cha kuweza kusaidia wakati dharura inapotokea? Mafia kila siku inatokea majahazi yanazama, watu kama hao wanaangukiwa na minazi, ndege imeanguka juzi, hakuna kitu chochote ambacho wanaweza kusaidia kukitokea dharura yoyote kutoka kwao.

Sasa nilikuwa naomba kwa kupitia nafasi hii, kuwaombea Wakuu wa Wilaya wote, watengewe kiasi japo kidogo cha fedha kwa ajili ya kuweka akiba angalau pale linapotokea tatizo la dharura, basi wao wawe wahimili wa kwanza wa kuweza kulitatua tatizo lile ili kukipunguzia mzigo Kitengo hiki cha Maafa cha Taifa.

La mwisho nilikuwa nataka kuzungumzia kwenye ukurasa wa 25 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, amelisifia sana hili suala la kuhudumia viwanda vidogo vidogo la Umoja wa Taifa na mimi naomba niungane naye.

Lakini hebu tuijulize hawa wanawake waliosaidiwa ni wanawake wa wapi, sisi kwetu Mafia mbona hatujapata misaada kama hiyo. Kwa hiyo, tunaomba misaada inapokuja na *NGOs* zinapokuja kutoka sehemu nyingine tofauti, basi tuonekane na sisi watu wa visiwani.

Nawashukuru ndugu zetu wa *Care* juzi juzi wameanza katuona na kuweza kufika katika Wilaya ya Mafia na wametoa mambo mengi tu na sasa hali ni nzuri na semina zinafanyika.

Pia naomba nitumie fursa hii kumshukuru Kadinali Pengo, kwa msaada wake aliotupa wa kuweza kukarabati jengo la Hospitali ya Wilaya ya Mafia kwa zaidi ya Sh. milioni 60.

Naomba sana Serikali pia ithamini mchango huo. Lakini nashukuru hata siku tuliyokwenda kupokea zawadi hizo niliongozana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia na kuomba yale yote niliyyoyazungumza, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kupitia Wizara zake, hasa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, aweze katuona sisi ndugu zake wa Mafia na tuweze kuondokana na kero kubwa kabisa tuliyokumbana nayo tangu Kisiwa hiki kimeumbwa na Mola. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ratiba ya kesho ni kwamba, tutaendelea na mjadala huu wa jumla hadi saa 6.00 mchana. Halafu nitawapa nafasi Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi wawili katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kila mmoja nusu saa hadi saa

7.00. Tukirudi saa 11.00 ndiyo mtoa hoja mwenyewe sasa atahitimisha hoja yake. Halafu tutaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima, inaitwa Kamati ya Matumizi, ili kupitia kifungu kimoja kimoja.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.42 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano
Tarehe 25 Juni, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*